

**KUCHUNGUZA DHAMIRA ZILIZOJENGWA KUPITIA TASHITITI  
KATIKA TAMTHILIA ZA KITANZANIA NA KIMISRI**

**ABDALLAH MASOUD SAAD AHMAD**

**TASINIFU ILIYOWASILISHWA KWA AJILI YA KUTIMIZA SHARTI PEKEE  
LA KUTUNUKIWA SHAHADA YA UZAMIVU (PhD. KISWAHILI) KATIKA  
IDARA YA LUGHA NA TAALUMA ZA FASIHI YA CHUO KIKUU  
HURIA CHA TANZANIA**

**2023**

## UTHIBITISHO

Waliotia sahihi hapa wanathibitisha kuwa wamesoma tasnifu hii inayohusu **‘Kuchunguza Dhamira Zilizojengwa Kupitia Tashititi katika Tamthilia za Kitanzania na Kimisri’**, na wanapendekeza ipokelewe na Chuo Kikuu Huria cha Tanzania kwa ajili ya kutimiza sharti pekee la kutunukiwa Shahada ya Uzamivu (PhD) ya Kiswahili katika Idara ya Lugha na Taaluma za Kiswahili ya Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.

---

Prof. Emmanuel Mbogo

(Msimamizi 1)

Tarehe \_\_\_\_\_

---

Dkt. Mohamed Omary Maguo

(Msimamizi 2)

Tarehe \_\_\_\_\_

**HAKIMILIKI**

Hairuhusiwi kuiga au kunakili kwa namna yoyote sehemu yoyote ile ya tasinifu hii kwa njia yoyote kama vile, kielektroniki, kurudufu nakala, kurekodi au njia yoyote nyingine bila ya idhini ya mwandishi au Chuo Kikuu Huria cha Tanzania kwa niaba.

**TAMKO**

Mimi, **ABDALLAH MASOUD SAAD AHMAD GOHAR**, nathibitisha kuwa tasinifu hii ni kazi yangu halisi na haijawahi kuwasilishwa katika Chuo Kikuu kingine chochote kwa ajili ya kutunukiwa shahada kama hii au nyingine yoyote.

---

Saini

Tarehe \_\_\_\_\_

## **TABARUKU**

Ninaitabaruku kazi hii kwa wazazi wangu, hasa Mama yangu aliyefariki Februari 24, 2022 Mwenyezi Mungu amlaze mahali pema peponi.

## SHUKURANI

Shukurani za dhati nazitoa kwa Allah Subhannahuu wataala kwa kuniwezesha kuwa na afya njema katika maisha yangu ya kila siku. Pia, namshukuru Allah kwa kuipa familia yangu afya njema na baraka tele. Nawashukuru walimu wangu, Prof. Emmanuel Mbogo na Dkt. Mohamed Omary Maguo ambao ni wasimamizi wangu wa kazi hii ya Tasinifu ya Shahada ya Uzamivu. Hakika, nimejifunza mambo mengi sana kutoka kwao na sasa nimekuwa mbobezi katika fasihi ya Kiswahili. Katika kunifundisha wamekuwa wakinikosoa na kunielekeza na kuweza kufanikiwa kufika katika hatua hii. Msaada walionipatia walimu wangu hawa ni mkubwa sana na ninawaombea kwa Mwenyezi Maungu aendelee kuwapa afya njema na maisha marefu.

Pia, Napenda kutoa shukurani zangu za dhati kwa walimu wangu Prof. Abdulhadi Hamed, Prof. Abdullhai Salem, Prof. Ayman Al-Asar, Prof. Wael Nabil, Dkt. Islam Faris na Dkt. Sameh Baeomy wote kutoka Chuo Kikuu cha Al-Azhar nchini Misri kwa kunilea kitaaluma na kuniwezesha kufika katika ngazi hii ya kitaaluma. Walimu hawa hawakuchoka katika kunihimiza kuhakikisha namaliza masomo yangu kwa wakati. Kila mara wamekuwa wakinipigia simu na kuniandikia jumbe katika barua pepe na simu wakiuliza maendeleo ya masomo yangu. Hakika walinitia moyo sana na kunifanya nifanye jitihada zaidi na sasa nimefika katika hatua hii ya kukamilisha masomo yangu.

Vile vile, napenda kutoa shukurani zangu za dhati kwa familia yangu kwa jumla nikianza na mke wangu na watoto wangu kwa uvumilivu wao katika kipindi chote

cha masomo yangu. Kutokana na uzito wa masomo ni dhahiri kwamba nilitumia muda mwingi katika masomo kuliko kuwa nao. Wakati mwingine nililazimika kuwa mbali nao ambapo mimi nikiwa Tanzania wao walikuwa Misri ingawa kuna kipindi tulikuwa sote pamoja nchini Tanzania. Nawaambia mke wangu na watoto wangu kwamba ninawapenda sana. Pia, nawashukuru sana wazazi wangu kwa kunizaa na kunilea katika misingi ya elimu ambayo leo inanifanya niweze kufika katika hatua hii ya juu katika elimu. Nasema asante sana kwa wazazi wangu na Allah awajaalie kila la kheir.

## IKISIRI

Utafiti huu ulihusu kuchunguza dhamira kupitia tashititi kwa kurejelea tamthilia teule za nchini Tanzania na Misri. Malengo mahususi ya utafiti yalikuwa mawili na lengo la kwanza lilihusu kuchambua dhamira zinazotokana na matumizi ya tashititi katika tamthilia teule. Lengo la pili lilihusu kuonesha kufanana na kutofautiana kwa dhamira zinazotokana na matumizi ya tashititi katika tamthilia teule (tamthilia teule za *Kaptula la Marx iliyoandikwa na Euphrase Kezilahabi* na *Embe Dodo iliyoandikwa na Dominicus Makukula* ambazo ni za watunzi wa Kitanzania na *Bwana Wetu Al-Muqadam (مولانا المقدم)* iliyoandikwa na *Walid Alaaeldin* na *Wananchi Wanapotoroka (الشعب لما يفسع)* iliyoandikwa na *Mahmoud Altokhy* za watunzi wa Misiri). Data za utafiti zilikusanywa kwa kutumia mbinu ya usomaji makini na kuchambuliwa kwa kutumia mkabala wa kimaielezo. Nadharia ya Fasihi Linganishi, Simiotiki na Usosholojia zimetumika katika uwasilishaji wa matokeo ya utafiti. Matokeo ya utafiti yanabainisha kwamba matumizi ya tashititi katika tamthilia teule yamesaidia kujenga na kuibua dhamira mbalimbali. Baadhi ya dhamira hizo zinahusu masuala ya ujamaa, ukosefu wa usawa, ufisadi, ukoloni mamboleo, matumizi mabaya ya madaraka, ukosefu wa demokrasia, ubaguzi wa kijinsia, nafasi duni ya mwanamke na malezi ya watoto. Tasinifu hii imeshughulikia suala la tashititi kwenye tamthilia ya Kitanzania na ya Kimisri. Tunapendekeza kufanya utafiti zaidi kuhusu Fasihi Linganishi baina ya tanzu za fasihi ya Kitanzania na ya Kimisri.

**Maneno Muhimu:** *Tashtiti, Tamthilia, Fasihi Linganishi*



## YALIYOMO

UTHIBITISHO .....	ii
HAKIMILIKI.....	iii
TAMKO.....	iv
TABARUKU .....	v
SHUKURANI.....	vi
IKISIRI.. .....	viii
YALIYOMO.....	ix
ORODHA YA MAJEDWALI.....	xiii

### **SURA YA KWANZA: UTANGULIZI .....** 1

1.1	Utangulizi.....	1
1.2	Usuli wa Tatizo la Utafiti.....	1
1.3	Tatizo la Utafiti .....	5
1.4	Malengo ya Utafiti .....	6
1.4.1	Lengo Kuu .....	6
1.4.2	Malengo Mahususi.....	6
1.4.3	Maswali ya Utafiti.....	6
1.5	Umuhimu wa Utafiti .....	7
1.6	Mawanda ya Utafiti.....	8
1.7	Mpangilio wa Tasinifu.....	8

### **SURA YA PILI: MAPITIO YA KAZI TANGULIZI NA MKABALA WA**

#### **KINADHARIA .....** 9

2.1	Utangulizi.....	9
-----	-----------------	---

2.2	Ufafanuzi wa Dhana.....	9
2.2.1	Dhana ya Tamthilia.....	9
2.2.2	Dhana ya Tashititi .....	10
2.2.3	Dhana ya Fasihi Linganishi .....	11
2.3	Historia ya Tamthilia Nchini Tanzania.....	12
2.3.1	Kipindi cha Kabla ya Ujio wa Ukoloni.....	13
2.3.2	Kipindi cha Ukoloni.....	14
2.3.3	Kipindi cha Baada ya Uhuru .....	16
2.4	Historia ya Tamthilia nchini Misri.....	16
2.4.1	Kipindi cha Kabla ya Ukoloni .....	17
2.4.2	Kipindi cha Ukoloni.....	17
2.4.3	Kipindi cha Baada ya Ukoloni .....	18
2.5	Tashititi Katika Tamthilia .....	20
2.6	Maudhui Katika Tamthilia Katika Kazi za Fasihi .....	25
2.7	Pengo la Utafiti .....	31
2.8	Mkabala wa Kinadharia .....	31
2.8.1	Nadharia ya Simotiki .....	32
2.8.2	Nadharia ya Usosholojia .....	36
2.8.3	Nadharia ya Fasihi Linganishi .....	39
2.9	Hitimisho.....	42
	<b>SURA YA TATU: MBINU ZA UTAFITI.....</b>	<b>43</b>
3.1	Utangulzi.....	43
3.2	Usanifu wa Utafiti.....	43

3.3	Uteuzi wa Sampuli.....	44
3.4	Vyanzo vya Data.....	44
3.5	Ukusanyaji wa Data .....	44
3.6	Uchambuzi wa Data.....	45
3.7	Usahihi na Kuaminika kwa Data .....	46
3.8	Maadili ya Utafiti.....	47
3.9	Hitimisho.....	47

## **SURA YA NNE: KUBAINISHA DHAMIRA ZILIZOJENGA KUPITIA**

### **TASHITITI KATIKA TAMTHILIA TEULE ..... 48**

4.1	Utangulizi.....	48
4.2	Uwasilishaji wa Data .....	48
4.2.1	Ufisadi.....	49
4.2.2	Udikteta.....	55
4.2.3	Ubaguzi na Nafasi ya Mwanamke .....	62
4.2.4	Uadilifu na Usawa.....	71
4.2.5	Haki na Demokrasia.....	75
4.2.6	Elimu.....	80
4.2.7	Malezi ya Watoto na Maadili.....	84
4.3	Hitimisho.....	91

## **SURA YA TANO: KULINGANISHA NA KULINGANUA DHAMIRA**

### **ZILIZOIBULIWA KWA KUTUMIA MBINU YA**

### **TASHITITI KATIKA TAMTHILIA TEULE ..... 92**

5.1	Utangulizi.....	92
-----	-----------------	----

5.2	Kulinganisha Dhamira Zilizoibuliwa kwa Kutumia Mbinu ya Tashititi katika Tamthilia Teule .....	92
5.3	Kulinganua Dhamira Zilizoibuliwa kwa Kutumia Mbinu ya Tashititi katika Tamthilia Teule .....	93
5.3.1	Ukoloni Mamboleo .....	94
5.3.2	Ujamaa na Kujitegemea .....	96
5.3.3	Ongezeko la Watu .....	97
5.3.4	Kodi ya Maendeleo .....	99
5.3.5	Nafasi ya Fasihi katika Jamii .....	102
5.3.6	Afya.....	106
5.3.7	Upendeleo na Urasimu.....	108
5.4	Hitimisho.....	112
<b>SURA YA SITA: MUHTASARI, MAPENDEKEZO NA HITIMISHO .....</b>		<b>113</b>
6.1	Utangulizi.....	113
6.2	Muhtasari wa Tasinifu .....	113
6.3	Utoshelevu wa Nadharia .....	113
6.4	Muhtasari wa Matokeo ya Utafiti .....	114
6.5	Mapendekezo .....	115
6.6	Hitimisho.....	116
<b>MAREJELEO .....</b>		<b>117</b>
<b>VIAMBATANISHO .....</b>		<b>129</b>

**ORODHA YA MAJEDWALI**

Jedwali Namba 4.1: Orodha ya dhamira zilibainishwa kutokana na matumizi ya tashititi katika tamthilia teule .....	49
Jedwali Namba 5.1 Orodha ya Dhamira zinazotofautiana katika Tamthilia Teule .....	93

## **SURA YA KWANZA**

### **UTANGULIZI**

#### **1.1 Utangulizi**

Tasinifu hii imechunguza dhamira kupitia tashititi katika tamthilia ya Kitanzania na Kimisri. Sura hii inahusu masuala ya kiutangulizi yaliyoelezwa katika tasinifu hii. Baadhi yake ni usuli wa tatizo, tatizo la utafiti, lengo kuu, malengo mahsusi ya utafiti na maswali ya utafiti. Pia, imeeleza umuhimu wa utafiti, mawanda ya utafiti na mpangilio wa utafiti mzima.

#### **1.2 Usuli wa Tatizo la Utafiti**

Tasinifu hii ililenga kulinganisha na kulinganua dhamira kupitia matumizi ya tashititi katika tamthilia teule mbili za Kimisiri na mbili za Kitanzania. Fasihi Linganishi ni taaluma inayohusisha uchunguzi wa maandishi ya wakati mmoja na aina moja na katika lugha mbalimbali kwa nia ya kumulika sifa zinazoyahusianisha (Wamitila, 2003). Bila shaka jamii yoyote, hasa jamii za Kiafrika zinatofautiana katika makazi, historia, eneo la kijiografia, lugha na tamaduni. Kwa mantiki hii, ni dhahiri kuwa Waafrika (Watanzania na Wamisri) wana namna yao ya kuyatazama mambo mbalimbali kutokana na mielekeo yao ya kijamii. Kutokana na hayo na kwamba fasihi ni kioo cha jamii kwa hivyo inatarajiwa kuibua na kuelezea hali halisi katika jamii, na fasihi ina majukumu makubwa, miongoni mwa majukumu yake katika jamii, ni kuelekeza jamii na kutoa maadili, kuonya, kuelimisha, kushauri kati ya majukumu mengine. Kwa hiyo, ipo haja ili tunaweza kujua fasihi kwenye hizo jamii inatoa maadili gani na kuonya na kuelekisha nini. Fasihi ya Kiswahili na ya Kiarabu zina historia ndefu kama fasihi yoyote duniani, na miongoni mwa matawi yake ni tamthilia. Tamthilia ya Kiswahili na ya Kiarabu

imeongea masuala tofauti ya kijamii, kiuchumi na kisiasa, na watafiti wengi walifanya kazi za kuchunguza tamthilia ili kuona ni kwa namna gani imebainisha hali ya jamii inahusika. Jamii hizo mbili imeingiliana kijamii kwa muda maalumu. Kwa hiyo, kutokana na sababu hizo, ilionekana ipo haja ya kufanya utafiti linganishi kwa kuchunguza kwa kina na kulinganisha tamthilia ya lugha hizo mbili yaani; kiswahili na kiarabu. Pia ipo haja ya kufanya utafiti linganishi baina ya fasihi ya Kitanzania na fasihi ya Kimisri ili tunaweza kuelewa hali halisi kwenye hizo jamii kupitia tamthilia, na hiyo kazi itakuwa kazi ya kwanza kwenye maktaba ya Tanzania ambapo itasaidia wahakiki na wataalamu wanapata picha halisi juu ya jamii hizo mbili.

Kwa hiyo, utafiti huu ulilenga kuchunguza dhamira katika tamthilia ya Kitanzania na Kimisri kupitia tashititi mifano kutoka katika tamthilia ya *Embe Dodo* iliyoandikwa na Dominicus Makukula na tamthilia ya *Kaptula la Marx* iliyoandikwa na Euphrase Kezilahabi na tamthilia ya *Wananchi Wanapotoroka* [الشعب لما يفلسع] iliyoandikwa na Mahmoud Altokhy (محمود الطوخي) na tamthilia ya *Bwana Wetu Almuqadam* [مولانا المقدم] iliyoandikwa na Walid Alaa Eldin (وليد علاء الدين). Tumechagua tamthilia hizo mbili kwa sababu tashititi zinapatikana katika hizo tamthilia. Tutaweza kuibua tashititi inavyoibua dhamira na inayowahusianisha wasanii wa tamthilia husika, kwa kushughulikia tashititi katika tamthilia husika kwa mkabala wa kiulinganishi.

Masuala yanayoangaziwa katika taaluma ya ulinganishi yanahusu siasa, uchumi na utamaduni. Baadhi ya masuala haya yanaelezwa kupitia mbinu ya tashititi. Tashititi ni mbinu inayotumiwa na wanafashihi kwa madhumuni mbalimbali. Tashititi ipo

kwenye fasihi zote duniani kwa sababu ina uwezo mkubwa kuwasilisha ujumbe wa fasihi kwa namna mbalimbali. Tashititi ni istilahi inayotokana na neno la Kiingereza *Satire* ambalo maana yake ya kimsingi ni tele, iliyojaa (Highet, 1962). Baadaye, *satura* imekuja kujulikana kwa maana ya mchanganiko uliojaa vitu mbalimbali. Tashititi inabeba maana mbalimbali kitu ambacho kinaonekana na kitu kingine haiko wazi. Tashititi ni mbinu inayotumiwa kupitia vichekesho na dhihaka kufichua uovu au ujunga fulani uliopo katika jamii.

Matumizi ya tashititi husababisha kicheko, furaha au ucheshi. Tashititi pia ni sanaa jumuiifu inayohusisha kejeli, kijembe, ubezaji na dhihaka (Wamitila 2003). Kwa mara nyingine, pamoja na maelezo haya kutuelekeza katika umahususi wa dhana ya tashititi. Lengo la tashititi ni kuhakiki vichekesho, kupiga picha maalum kuhusu tukio au mhusika au kundi la watu kwa njia ya vichekesho. Utafiti katika tamthilia na tashititi haujafanywa kwa kiasi kikubwa ikilinganishwa na uchunguzi wa maudhui katika tamthilia.

Wapo watafiti waliofanya utafiti katika eneo la ufutuhi na tashititi hata sitiari katika baadhi ya tamthilia za Kiswahili na za Kimisri. Ramadhan (2005) alichunguza sitiari katika tamthilia za *Mashetani* na *Ngoma ya Ng'wanamalundi* na kubaini kwamba kuna ufanano mkubwa wa matumizi ya sitiari katika tamthilia hizi hususani sitiari zinazohusika na masuala ya uchawi na ushirikina. Utafiti huu umesaidia kupata uelewa kwamba sitiari zipo za aina nyingi na sitiari zina nafasi kubwa katika kujenga tashititi zinazoshughulikiwa katika tasnifu hii.

Pia, Mrikaria (2010) anaeleza kwamba kejeli katika fasihi ni chombo cha kuibua maovu ambayo yamejificha katika jamii ili yatambuliwe na kukomeshwa.



Anaendelea kueleza kwamba, kejeli ni chombo ambacho kinatumika katika kujenga tashititi ambamo ndani ya tashititi ndimo kumefumbatwa dhamira mbalimbali zikiwemo dhamira za maovu na mambo mabaya yanayofanywa katika jamii. Utafiti wetu unakusudia kuchunguza dhamira katika tamthilia za Kiswahili na za Kimisri ili kuona zinafanana na kutofautiana vipi katika dhamira.

Fatma (2016) alifanya utafiti uliochunguza tashititi katika tamthilia ya *Ahmad Ridha Hoho*. Katika utafiti wake, aliweza kubainisha kwamba, tashititi ni mbinu ya kisanaa ambayo hutumiwa kwa lengo la kueleza mambo kwa lugha ambayo si rahisi kubanwa na mkono wa dola. Kupitia tashititi, tabaka tawala linaweza kukosolewa bila ya kuonesha waziwazi. Maelezo ya utafiti wa Fatma yametusaikia kuona kwamba utafiti tunaoufanya utaleta tija. Utafiti huu unakusudia kulinganisha na kulinganua dhamira kupitia tashititi katika tamthilia teule mbili za Kimisiri na mbili za Kiswahili.

Gwanko (2017) alifanya utafiti ambao ulilenga kutathimini mbinu za ufutuhi katika kuelimisha jamii kuhusu janga la UKIMWI akirejelea tamthilia za *Embe Dodo* na *Ushuhuda wa Mifupa*. Katika utafiti wake, alibainisha kwamba, mbinu za kifutuhi ni muhimu katika kufikisha ujumbe kuhusu suala ya UKIMWI ambalo ni janga linalogharimu maisha ya watu. Ufutuhi husaidia kufikisha ujumbe kwa namna ambayo jamii haipati huzuni. Ufutuhi na tashititi ni vitu vinavyotegemeana sana. Utafiti wa Gwanko umetusaidia kukuza zaidi maarifa kuhusu tashititi.

Calium (2018) alichunguza maudhui na fani katika tamthilia za *Mashetani* na *Kivuli Kinaishi* kama utafiti linganishi. Mtafiti alibaini kwamba, licha ya tamthilia hizi kuandikwa katika mazingira na muktadha tofauti, lakini zinaufanano mkubwa

katika fani na maudhui. Utafiti wake, kwa kiasi kikubwa, umesaidia katika kukuza uelewa wetu juu ya ulinganishi katika utafiti ambapo tumeona vipengele vya kifani na kimaudhui vikilinganishwa. Utafiti huu umelenga kutathmini namna tashititi inavyoibua dhamira katika tamthilia teule za Kitanzania na Kimisri za *Embe Dodo* (Dominicus Makukula), *Kaptula la Marx* (Euphrase Kezilahabi), *Wananchi Wanapotoroka* (Mahmoud Altokhy) na *Bwana Wetu Almuqadam* (Walid Alaa Eldin).

### **1.3 Tatizo la Utafiti**

Tatizo la utafiti huu ni kuchunguza dhamira kupitia tashititi kwenye tamthilia ya Kitanzania na tamthilia ya Kimisri ili tunaweza kujua hali halisi katika nyanja tofauti kwenye nchi hizo mbili na tunaziba pengo la maarifa kwenye maktaba ya Tanzania. Tunahitaji kufafanua dhamira zinazojitokeza kupitia tashititi na tunajadili kisha kueleza, dhamira za jamii hizo mbili yaani Misri na Tanzania kupitia tamthiliya teule. Jamii ya Waswahili na Wamisiri zimekuwa na mahusiano ya muda mrefu sana katika maeneo ya kijamii, kiuchumi, kisiasa na kiutamaduni. Katika kuthibitisha mahusiano hayo, nchi hizi mbili kila moja ina ubalozi wake katika nchi hizi kwa miaka mingi sasa. Harakati za ukombozi wa nchi hizi mbili na ukombozi wa bara la Afrika kwa ujumla zimefanyika katika mazingira ambayo kwa kiasi kikubwa yanafanana sana. Pia, nchi ya Misri ni moja kati ya nchi kubwa duniani ambayo inafahamika na kuheshimika kwa kuwa na gunduzi na bunifu nyingi katika masuala ya taaluma, utafiti na utamaduni. Kwa upande mwingine, Tanzania inatajwa kuwa ndiyo nchi ambayo ni chanzo cha mwanadamu ambapo fuvu la mwanadamu wa kwanza kuishi duniani lilipatikana katika eneo la Olduvai George.

Kwa hiyo, uhusiano wa jamii hizo unaweza kuchunguzwa kwa kurejelea kazi za kifasihi na hususani tamthilia. Tasinifu hii ililenga kulinganisha na kulinganua dhamira kupitia tashtiti katika tamthilia teule mbili za Tanzania za *Embe Dodo* na *Kaptula la Marx* na mbili za Misri za *Wananchi Wanapotoroka* na *Bwana wetu Almuqadam*.

#### **1.4 Malengo ya Utafiti**

Utafiti huu utaongozwa na lengo kuu na malengo mahususi.

##### **1.4.1 Lengo Kuu**

Lengo kuu la utafiti ni kuchunguza dhamira kupitia matumizi ya tashititi kwa kurejelea tamthilia teule za nchini Tanzania na Misri.

##### **1.4.2 Malengo Mahususi**

Utafiti huu una malengo mahususi mawili ambayo ni haya yafuatayo:

- i) Kuchambua dhamira zilizowasilishwa kwa kutumia mbinu ya tashititi katika tamthilia teule.
- ii) Kulinganisha na kulinganua (yaani kuonesha kufanana na kutofautiana) dhamira zilizoibuliwa kwa kutumia mbinu ya tashititi katika tamthilia teule.

##### **1.4.3 Maswali ya Utafiti**

Utafiti huu una jumla ya maswali mawili ya utafiti kama yalivyoorodheshwa hapa chini:

- i) Dhamira zipi zinazowasilishwa kupitia mbinu ya tashititi katika tamthilia teule?
- ii) Dhamira zilizoibuliwa kwa kutumia mbinu ya tashititi zinafanana na kutofautiana vipi katika tamthilia teule?

## **1.5 Umuhimu wa Utafiti**

Utafiti huu utakuwa na umuhimu mkubwa kwa kuwa utasaidia kuweka bayana kufanana na kutofautiana kwa matumizi ya kipengele cha dhamira katika tamthilia teule. Hali hii itasaidia kubainisha kukua na kukomaa kwa maendeleo ya tamthilia katika nyanja za kisiasa, kiuchumi na kiutamaduni katika jamii za Tanzania na Misri. Pia, uchunguzi wa dhamira hizo utasaidia kubaini uhusiano wa kihistoria uliopo baina ya jamii za Tanzania na Misri. Utafiti huu utaonesha masuala ya kiutamaduni katika jamii za Kitanzania na Kimisri kwa kuzibainisha tamaduni hizo itakuwa rahisi kwa msomaji au mhakiki kuzielewa kwa undani pale anapotaka kutumia tamaduni hizo kwenye maandishi yake. Utafiti huu ni muhimu pia katika kuimarisha nadharia ya Fasihi Linganishi. Nadharia hii itaimarika kutokana na utafiti huu kuyaeleza masuala ya muhimu kati ya fasihi ya nchi mbili tofauti.

Utafiti huu utakuwa ni rejeleo muhimu kwa wanafunzi ambao wanajifunza masuala yanayohusu historia na maendeleo ya lugha ya Kiswahili na fasihi yake, hasa uhusiano uliopo baina yake na jamii nyingine za nje ya Afrika Mashariki. Utafiti huu utawafaa wanafunzi kuanzia ngazi ya shahada ya kwanza, uzamili na uzamivu. Pia, tasinifu hii inaweza kubaini mada mbalimbali za kufanyia utafiti ili kukuza zaidi taaluma ya tamthilia katika fasihi ya Kiswahili. Kipekee, wahadhiri watautumia utafiti huu kama rejeleo muhimu katika shughuli zao za kitaaluma, pamoja na kuandaa maandalio ya masomo yao kwa wanafunzi wao.

Utafiti huu utasaidia kukuza tamthilia ya ndani ya Afrika Mashariki na nje yake kwa kujiegemeza kwenye kigezo cha dhamira na mtindo. Pia, utawezesha kuibuka kwa mitazamo mbalimbali kuhusu nafasi ya utanzu teule katika kuijenga jamii kimaadili,

kimaisha na kimazingira kwa kuyamulika yale yanayopaswa na yasiyopaswa kuendelezwa kwa manufaa mapana ya jamii za Kiafrika.

### **1.6 Mawanda ya Utafiti**

Tasinifu hii imechunguza dhamira kupitia tashititi katika tamthilia teule mbili za Tanzania za *Embe Dodo* na *Kaptula la Marx* na *Wanapotoroka* na *Bwana wetu Almuqadam* za nchini Misri. Tamthilia hizi zimeteuliwa kimakusudi kwa vile ni zina utajiri mkubwa wa matumizi ya tashititi. Matumizi ya tashititi yamechunguzwa namna yanavyoibua dhamira kwa kurejelea vitabu viteule. Nadharia za Simiotiki, Usosholojia na Fasihi Linganishi zimetumika katika uchambuzi na mjadala wa data zilizowasilishwa katika utafiti huu. Mbinu ya kimaelezo imetumika katika uwasilishaji wa matokeo ya utafiti.

### **1.7 Mpangilio wa Tasinifu**

Tasinifu hii ina jumla ya sura sita. Sura ya kwanza inahusu utangulizi, usuli wa tatizo la utafiti, tatizo la utafiti, malengo ya utafiti na maswali ya utafiti. Pia, kuna umuhimu wa utafiti, mawanda ya utafiti na mpangilio wa tasinifu nzima. Sura ya pili inahusu mapitio ya kazi tangulizi na mkabala wa kinadharia. Sura ya tatu imewasilisha mbinu za utafiti. Sura ya nne na ya tano zinahusu uchambuzi, uwasilishaji na mjadala wa data za utafiti. Sura ya sita inahusu muhtasari, matokeo na mapendekezo ya utafiti.

## **SURA YA PILI**

### **MAPITIO YA KAZI TANGULIZI NA MKABALA WA KINADHARIA**

#### **2.1 Utangulizi**

Mapitio ya kazi tangulizi katika tasnifu hii yanahusu maandiko mbalimbali yanayohusiana na mada iliyolengwa. Maandiko haya yanahusisha, vitabu, tasnifu na makala za kiuchambuzi na kiuhakiki. Mapitio ya utafiti yanasaidia kubaini pengo la kiutafiti katika utafiti unaohusika (Yin, 1994). Katika sehemu hii, vipengele vinavyohusiana na mada teule vimeelezwa kwa namna mbalimbali.

#### **2.2 Ufafanuzi wa Dhana**

Sehemu hii imetoa ufafanuzi wa dhana mbalimbali zilizohusika katika tasnifu hii kama zilivyoelezwa.

##### **2.2.1 Dhana ya Tamthilia**

Dhana ya tamthilia inaelezwa na wataalamu mbalimbali. Fathi (1986) anaeleza kwamba, tamthilia ni utungo wa fasihi ya kidrama inayolenga kuoneshwa mbele ya hadhira kupitia wahusika wanaofanya maongezi na matendo yaliyotungwa na mtungaji (tafsiri yetu). Kwa ufupi, tamthilia ni sanaa ambayo lengo lake kuoneshwa mbele ya hadhira kupitia maongezi na matendo ya wahusika. Ufafanuzi wa Fathi umesaidia kuelewa kuwa tamthilia fani ya utendaji.

Sallam (1993) anaeleza kwamba, tamthilia ni moja ya aina ya shughuli za kiakili za kibinadamu inayoeleza hisia zake, malengo yake, mahusiano yake, historia yake, maisha yake, mazingira yake na maadili yake. Kwa hivyo, tamthilia ni sanaa inayoelezea utamaduni na maendeleo; na ni sanaa inayosaidia katika ustawi wa

jamii katika nyanja zake zote za maisha. Maelezo haya yanaonesha kuwa tamthilia ni akisiko la jamii. Uakisiko huo umesaidia katika uchunguzi wa kipengele cha dhamira katika tamthilia teule.

Wafula (1999) anaeleza kwamba, tamthilia ni utungo wa fasihi unaowasilisha hadithi na migongano kwa kutumia maongezi na matendo ya wahusika. Pia, ule utungo, hasa ulioandikwa kwa ajili ya kuigizwa. Drama ni somo linalohusu uigizaji wa hali fulani iwe ni vitendo, tabia au hisia za binadamu kwa kufuata taratibu maalum. Utungo wa kisanaa huweka wazo fulani katika matendo na mazungumzo. Utafiti wetu umezingatia kuwa tamthilia ni fani changamani inayohusisha matendo na mazungumzo katika uwasilishwaji wake.

Pia, Wamitila (2003) anaeleza kwamba, tamthilia ni kazi ya kidrama na ya kimaongezi ambayo huigizwa mbele ya hadhira au kazi iliyoandikwa kusomwa, kimuundo, hugawika katika matendo, maonesho na mazungumzo huchukua sehemu kubwa katika uwasilishaji wake. Wamitila anasisitiza kuwa tamthilia ni utungo unaoweza kuwa umeandikwa au haukuandikwa. Ufafanuzi uliotolewa kuhusu dhana ya tamthilia umetujengea uelewa mpana katika uchunguzi wa mada tele kwa kurejelea tamthilia teule.

### **2.2.2 Dhana ya Tashititi**

Kazi yoyote ya sanaa, ikiwemo tamthilia, riwaya na hadithi fupi bila shaka lazima yapo matumizi ya lugha. Matumizi ya lugha ni kipengele muhimu katika kazi za fasihi. Miongoni mwa vipengele hivyo ni matumizi ya tashititi (Njogu na Chimerah, 1999). Wataalamu mbalimbali wanaeleza maana ya tashititi kwa namna

mbalimbali zilizoeleza maana moja ya msingi. Kwa mfano, Wamitila (2003) anaelezea kuwa tashititi ni dhana ya ucheshi inayotumika kuelezea uwezo wa kazi ya fasihi na sanaa ya maonesho na kusababisha vichekesho kwa msomaji au mtazamaji. Maelezo haya yamesaidia katika uchunguzi wa namna tashititi zinavyobeba dhamira katika tamthilia teule.

Pia, Wamitila (2002) anafasili dhana ya tashititi kuwa ni utanzu mwepesi unapolinganishwa na tanzia. Lengo la kimsingi la tashititi ni kuchangamsha na kuishia kwa namna ya kufurahisha. Lazima tukumbuke kuwa, kusema tashititi inafurahisha haina maana kuwa dhamira zake hazina uzito. Anaendelea kueleza kwamba, tashititi ni mbinu inayotumia vichekesho na dhihaka ili kufichua uovu fulani uliopo katika jamii. Ufafanuzi huu umesaidia katika uchunguzi wa dhamira zilizomo katika vitabu teule namna zinavyofichua uovu uliotamalaki katika jamii.

Kwa jumla, tunaweza kusema kwamba, tashititi ni matumizi ya lugha yaliyosheheni ucheshi ndani yake na kupitia ucheshi huo ndimo maudhui hujitokeza. Tashititi hujitokeza katika vipengele mbalimbali vya matumizi ya lugha pamoja na tamathali za semi kama vile tashibiha, tashihisi, sitiari, kinaya, kejeli, dhihaka, utani, picha, taswira na ishara. Katika utafiti huu, tumebainisha vema tashititi kupitia vipengele vya matumizi ya lugha kama ilivyotumika katika tamthilia teule.

### **2.2.3 Dhana ya Fasihi Linganishi**

Fasihi Linganishi ni taaluma pana iliyoandikiwa na wataalamu mbalimbali duniani kwa madhumuni mbalimbali. Fasihi Linganishi ni somo la fasihi nje ya mipaka ya nchi moja ili kujifunza uhusiano baina ya fasihi kwa upande mmoja na eneo lingine



la maarifa kama vile sanaa, falsafa, historia ya jamii, sayansi na dini (Warren&Wellek, 1988). Mawazo haya yanaungwa mkono na Jilala (2016) pale anapoeleza kuwa Fasihi Linganishi inasaidia kubainisha, kutofautisha, kufanana na kuhusiana kwa fasihi katika itikadi na mielekeo ya jamii mbalimbali ulimwenguni.

Ponera (2014) anaeleza kuwa dhana ya Fasihi Linganishi imewekewa misingi yake na wataalamu wa fasihi wa Uyunani ya kale na wataalamu hawa wa fasihi walikuwa wakijihusisha na ulinganishaji wa kazi mbalimbali za tamthilia kwa lengo la kupata kazi bora zitakazofaa kupelekwa kwa hadhira iliyolengwa. Kimsingi, Fasihi Linganishi ni dhana inayohusisha kulinganisha na kulinganua kazi za fasihi za jamii na mataifa mbalimbali ulimwenguni ili kuona ufanano na utofauti uliopo baina ya fasihi hizo. Hivyo, katika utafiti wetu, dhana ya Fasihi Linganishi imetumika kulinganisha na kulinganua fasihi ya Kitanzania na Kimisri kwa kurejelea tamthilia teule. Mtafiti hapo chini anatoa mwanga juu ya historia ya tamthilia nchini Tanzania na Misri ili msomaji aweza kupata picha kamili juu ya hali ya tamthilia na athari zake kwenye hizo nchi mbili.

### **2.3 Historia ya Tamthilia Nchini Tanzania**

Historia ya tamthilia yoyote imeanza kupitia kwa sanaa za maonesho za fani ya jadi, lakini tamthilia ya kisasa imeletwa nchini kupitia Ukoloni. Semzaba (1997) anakiri kwamba, kabla ya kuja kwa Wakoloni tamthilia haikuwepo nchini. Anaendelea kueleza kwamba, aina za sanaa za maonesho zilizokuwepo zilitofautiana na tamthilia iliyoingizwa na tamaduni ngeni. Tamthilia inapita katika kipindi cha mabadiliko mbalimbali, yakiwemo yanayotokana na masuala ya siasa

na elimu. Kwa hiyo, tunaweza kuigawa historia ya tamthilia kwa kipindi cha kabla ya ujio wa Ukoloni, kipindi cha Ukoloni, kipindi cha baada ya Ukoloni.

### **2.3.1 Kipindi cha Kabla ya Ujio wa Ukoloni**

Mulokozi (1996) anaeleza kuwa kabla ya Ukoloni tamthilia zilizoandikwa ili ziigizwe jukwaani hazikuwepo, badala yake zilikuwepo zisizoandikwa, zilizogeuzwa kwa ajili ya kuoneshwa kwenye shughuli maalumu kama vile katika sherehe za jando na unyago, mazishi, kutawazwa kwa mtemi, arusi na michezo ya watoto. Tamthilia hizo zilikuwa na sifa ya kuwa na hadithi, vitendo, wahusika na waigizaji wao na dayolojia. Hata hivyo, hazikuwepo na ploti ya Ki-Aristotle wala matini yaliyoandikwa na kuwa tamthilia simulizi.

Sanaa za maonesho zilikuwa zinatumiwa kama kwa ajili ya kutoa mafunzo kwa jamii. Michezo ya kuigizwa iliyojulikana kama tamthilia au drama ilikuwa inatumia sana ngoma, matambiko, hadithi, majigambo na nyimbo. Kiango (1973) anasisitiza kuwa michezo ya kuigiza si kitu kigeni miongoni mwa wasemaji wa Kiswahili kwani wao wamepata kuishuhudia michezo hiyo katika ngoma zao za kienyeji. Hivi leo ngoma za kienyeji zinaonekana kuwa ni hazina kubwa sana katika michezo ya kuigiza inayoandamana na ngoma.

Sanaa za maonesho za jadi zinatofautiana na tamthilia kwa msingi kuwa wakati sanaa za maonesho za jadi kama ngoma, majigambo, jando, unyago na matambiko (miviga) zina chimbuko lake katika mila na desturi za Watanzania, lakini tamthilia ina msingi ya chimbuko lake huko Ulaya. Kwa hiyo, tamthilia ya kisasa chimbuko lake ni sanaa za maonesho za jadi na kapata maendeleo kupitia uvumbuzi wa sayansi na teknolojia zilizoletwa na Wakoloni.

### 2.3.2 Kipindi cha Ukoloni

Ujio wa Wakoloni katika jamii za Afrika Mashariki imesababisha kuwepo kwa mabadiliko mengi katika tamthilia baada ya kuwepo kwa teknolojia ya maandishi. Wafula (1999) amebainisha kwamba ujio wa Wakoloni ulileta mapinduzi makubwa katika sanaa za maonesho za jadi na kuingiza tamthilia. Wakoloni walikuja na tamthilia zao za Kizungu na miundo ya kutunga tamthilia. Waandishi wa Kiafrika walizitumia zile njia za kutunga tamthilia na kuingiza baadhi ya vipengele vya fani ya jadi.

Mulokozi (1996) anaeleza kwamba katika wakati wa Ukoloni tamthilia ziliandikwa kwa lugha ya Kiingereza na zilizojikita katika utamaduni wa Kizungu kuanzia miaka ya 1920 hapa nchini. Lengo kuu ilikuwa ni kuburudisha maofisa wa Kizungu. Baadaye, viliibuka vikundi viwili vya kuigiza; Dar es Salaam Players (1947) na Arusha Little Theatre (1953). Kuanzia wakati huo, tamthilia ya Kiswahili ilianza kuhusishwa katika mashindano. Hali hii ilichochea utunzi wa tamthilia ya Kiswahili. Ujio wa Wakoloni umesaidia kuhamisha utunzi wa tamthiliaya Kiswahili.

Bertoncini (2009) anasema, Waafrika enzi ya Ukoloni walitawaliwa na fikra za Wamisionari. Hali hiyo iliwafanya wakubali mtindo wa tamthilia za Kimagharibi za Shakespeare, Sheridan na Moliere kama tamthilia bora zaidi na za kipekee ulimwenguni. Mtindo wa kidrama ukaingizwa katika mtalaa wa elimu, vikundi vya drama vya wakati huo na katika vikundi vya maonesho vilivyoongozwa na Wakoloni. Kuanzia wakati huo, michezo iliyoandikwa, matumizi ya jukwaa ya

kawaida na pazia ziliingizwa katika uigizaji. Katika kipindi hicho, sanaa ya uigizaji nchini Tanzania ilitawaliwa na mtindo wa tamthilia za Kimagharibi.

Kiango (1973) anaeleza kuwa michezo ya kuigiza iliyokuwa ikitendwa sambamba na sanaa za maonesho ilianza kuchukua sura mpya iliyoendana na matakwa ya Wakoloni. Badala ya kutendwa sambamba na sanaa nyingine za jadi kama vile ngoma, nyimbo na miviga, ilitendwa katika upekee wake kwa jina la drama. Wakoloni walianzisha jukwaa la ndani tofauti na matumizi ya uwanja kama ilivyokuwa ikifanyika kwa wenyeji ili kila mtu aone. Hali hii ilisababisha kuwepo kwa mabadiliko ya hali ya jukwaa pamoja na uhusiano uliokuwepo kati ya jukwaa, watendaji na watazamaji. Wakoloni walianza kutunga na kuonesha tamthilia kwa kurejelea fani za jadi.

Tamthilia ililetwa Tanzania na Waingereza na kuingizwa shuleni, ambapo wengi wa walimu walikuwa Waingereza (Mlama, 2003). Madhumuni ya kuingiza drama hayakuwa na uzito mkubwa kwani tamthilia zao zilihusu utamaduni wao na mila zao. Kwa hiyo, zilikuwa hazina uzito mkubwa kwa Watanzania. Waingereza waliitumia tamthilia kama chombo cha burudani, hasa wasipokuwa na shughuli maalumu ya kufanya. Waliona kuendesha tamthilia ni jambo bora kwao kwa sababu lilihusu utamaduni wao na waliweza kujitambulisha kiutamaduni.

Wafula (1999) ametaja kwamba, Graham Hyslop, hapa Afrika Mashiriki, ndiye alianza kuandika tamthilia (1957). Baadhi yake ni *Afadhali Mchawi* na *Mgeni Karibu*. Baadaye walikuja wanafunzi wake, akiwemo H. Kuria. Mwishoni tunaweza kusema kwamba, chanzo cha tamthilia ya Kiswahili ni masomo ya

kigeni, tafsiri za tamthilia za Ulaya na sanaa za jadi. Sanaa za kiasili zimechangia sana kukua tamthilia ya Kiswahili, hasa mwanzoni mwake. Tamthilia ililetwa na Wakoloni, lakini sanaa za jadi zilikuwepo hata kabla ya ujio wa Wakoloni.

### **2.3.3 Kipindi cha Baada ya Uhuru**

Utungaji wa tamthilia zenye maudhui ya kitamaduni na kijamii haukukoma wakati uhuru ulipopatikani. Katika kipindi hiki, waandishi wengi walianza kujitokeza na kutunga kazi nyingi za nathari juu ya maudhui mbalimbali. Kazi nyingi zenye maudhui ya utamaduni asilia zilizuka. Kutokana na uhuru, tamthilia muhimu za Kizungu zilianza kutafsiriwa na kuigizwa kwa lugha ya Kiswahili. Baadhi yake ni *Juliasi Kaisari* ya Shakespare na *Mabepari wa Venisi*. Tamthilia zilizotafsiriwa hazikuwa za Kizungu tu, bali zilihusisha hata zile za Kiafrika zilizoandikwa kwa lugha za kigeni na lugha nyingine za Kiafrika zilitafsiriwa kwa Kiswahili kama vile *Mtawa Mweusi* na *Masaibu ya Ndugu Jero*.

Baada ya Uhuru waandishi wengi chipukizi wa tamthilia ya Kiswahili walipata hamasa ya kuandika kuhusu jamii zao, akiwemo E. Hussein, Penina Muhando na G. UHINGA waliandika kwa kutumia foni za sanaa za maonesho (Mulokozi, 1996). Hali hii ilichangia waandishi wengi kuandika kuhusu hali halisi iliyopo katika jamii inayohusika badala kuutukuza utamaduni wa Kizungu kama tamthilia za mwanzo zilizopuuza utamaduni wa Kiafrika.

## **2.4 Historia ya Tamthilia nchini Misri**

Hadi leo, kuna mazungumzo baina ya wasomi kuhusu mwanzo wa tamthilia ya Kimisri. Baadhi yao walipitia matukio kadhaa katika urithi wa Kimisri na

wakawaona kama tamthilia ya aina maalum na wengine walikiri kwamba tamthilia haikuwepo katika urithi wa Wamisri. Hata hivyo, wanakiri kuwa ilikuwepo sanaa ambayo ilikuja na kampeni ya Ufaransa dhidi ya Misri mnamo mwaka 1798. Wamisri walisikia kupitia kwa Marawan Alnaqash katikati ya karne ya kumi na tisa.

#### **2.4.1 Kipindi cha Kabla ya Ukoloni**

Tamthilia ya Misri imepitia hatua nyingi, ambazo zote zinarejelea wazo kwamba tamthilia ya Misri ina maendeleo kila wakati. Baadhi ya watu wanaeleza kwamba kuwepo wa tamthilia katika enzi ya mafarao (Sadgrove, 2007). Vikundi vya tamthilia vya kale vilionesha maonesho mbele ya familia zinazotawala. Pia, kulikuwa na baadhi ya maandishi kwenye kuta za mahekalu ambazo zinaonesha kuwepo wa tamthilia wa Misri wakati huo. Kuhusu ukumbi wa michezo wa watu wa kawaida ulikuwa umeenea kati ya watu wa kawaida katika vijiji na miji ya Misri, iliwakilishwa na bendi za wasafiri, pamoja na wachezaji, wanamuziki na waigizaji. Waliwasilisha hadithi fupi ambazo hazizidi dakika 10 na kuvuta kwao kwa muziki na densi. Pia, walikuwa wakikusanya kutoka kwa watu hao ngano, mayai na chakula, kwa sababu, Mmisri wa zamani hakujua kushughulika na pesa kama ilivyo sasa.

#### **2.4.2 Kipindi cha Ukoloni**

Tamthilia ya Kimisri imeathiriwa sana na masomo ya kigeni, hasa kule Ulaya. Mwanzo wa kuwepo tamthilia ya Kizungu nchini Misri ni kupitia Ukoloni wa Ufaransa mwaka 1799 (Sadgrove, 2007). Lengo leke kuu ilikuwa ni kuwaburudisha wakazi wa Kifaransa na Wazungu wanafanya biashara nchini Misri. Kabla ujio wa

Ukoloni wa Ufaransa zilikuwepo baadhi ya sanaa ya maonesho barabarani na uwanja wa umma, pamoja na waigizaji wa kimya. Katika historia ya tamthilia nchini Misri, tamthilia ya Kifaransa na Kiitalia zilifikia kiwango chake cha juu kabisa. Serikali ilikuwa ikihimiza tamthilia ya Kizungu ili kuwatoza pesa wanaokuja kutoka Ulaya, wakazi wa Ulaya na Wazungu wengine na Wamisri wanaopenda Uzungu. Pia tamthilia katika Misri wakati huo ilikuwa haina uzito mkubwa kwani ilikuwa inaongea juu ya tamaduni za kigeni, na masuala hayakuhusu jamii ya Kimisri.

#### **2.4.3 Kipindi cha Baada ya Ukoloni**

Baada ya kampeni kutoka Misri mnamo 1801 BK, katika hafla ya ufunguzi wa Mfereji wa Suez mnamo 1869 BK, Khediwe Ismail alianzisha Opera House huko Ataba Square, ili kuwasilisha maonesho mbele ya wafalme na wakuu wa Ulaya ambao walikuwa wameazimia kusherehekea sherehe kuu. Hakuna mtu huko Misri aliyejua chochote juu ya sanaa hiyo. Khediwe Ismail amemwagiza mwanamuziki wa Italia, Verdi ili anafanya opera ambayo imetolewa kutoka kwa historia ya zamani ya Misri. Opera ilioneshwa ni opera Aida na opera ya Rigoletto na maonesho hayo yalikuwa kwa lugha ya Kiitaliano. Baada ya sherehe kumalizika nyumba ya opera ilifungwa kwa muda mrefu sana.

Katika kipindi hicho pia, Khediwe Ismail aliunda ukumbi wa michezo wa pili katika hifadhi ya Azbakeya mnamo 1870 na ulikuwa ukumbi wa kwanza wa kitaifa ulizaliwa. Mnamo 1885 BK, ukumbi wa michezo huu ulishuhudia msimu wa kwanza wa maonesho kwa kikundi cha Abu Khalil al-Qabbani huko Cairo na kikosi cha Iskandar Farah kilionesha kazi zao maarufu kwenye ukumbi huo huo kutoka 1891

hadi 1905. Pia, sanaa ya tamthilia iliingia Misri katika hali yake ya kisasa kupitia kwa msanii Yaqoub Sanoua mnamo 1876, ambaye alikuwa hodari kwa Kiitaliano na Kifaransa.

Khediwe Ismail alikuwa na furaha ya kuanzisha sanaa ya maonesho katika Misri kama alivyoona katika nchi za Ulaya na alihudhuria baadhi ya michezo yake na kuivutia na kumuita Molière wa Misri. Yaqoub Sanoua alikuwa jasiri na alikuwa na hamu isiyo na mipaka ya mabadiliko. Pia, aliwakosoa wakuu wa serikali, utendaji wa serikali na kushutumu udhalimu wa Khediwe Ismail na jeuri ya watawala wa nchi wakati wa utawala wake, hasa katika mchezo wa Nchi na Uhuru ambao ulikasirisha tabaka tawala likiongozwa na Ismail mwenyewe na aliamuru kufungwa kwa ukumbi wa michezo.

Tamthilia ya kwanza imeyofasiriwa ni *Helene Mwenye Urembo* (La Belle Helene) kwa mwandishi Offenbach kutoka Italiya 1869. Tamthilia ya kisasa ya Kimisri ilianza 1876 ambapo Yaaqub Sanoua ameandika wito wa kwanza katika jarida la Kiarabu kwa ajili ya kuanzisha tamthilia ya Kiarabu katika Misri. Sanoua alijifunza tamthilia kupitia masomo ya waandishi wakubwa wa Ulaya na tamthilia ya Kizungu nchini Misri.

Huko Alexandria, sanaa ya Maroun Naqqash na Salim Naqqash ilienea na nchi za Shawam ziliwasilisha maonesho yao mengi huko Beirut na Dameski. Kisha, wakaja kuwasilisha sanaa yao huko Misri mnamo 1876 BK; na Adib alishirikana nao kwenye tafsiri na uandishi. Mnamo mwaka wa 1888 BK, ukumbi wa michezo wa Misri ulishuhudia maendeleo makubwa kupitia kwa Ahmed Abu Khalil al-Qabbani na kikundi chake cha ukumbi wa michezo, kwa sababu aliamusha ukumbi wa



michezo kutoka kunukuu fasihi za ulimwengu kwenda kwa kuunda kwa tamthilia. Historia ya tamthilia ya Kimisri ilijaa kazi nyingi zilizowasilishwa na al-Qabbani kwenye kumbi za Kairo na Alexandria.

Katika miaka ya ishirini ya karne ya ishirini, maoni ya umma yakaanza kutaka uwepo wa ukumbi wa michezo wa kitaifa wa Misri mbali na fasihi ya kimataifa. Kwa hivyo, ukumbi wa michezo wa kitaifa ulianzishwa mnamo 1921. Baadaye, amejitokeza Tawfiq Alhakim ambaye ameandika tamthilia yake ya kwanza inayoitwa Watu wa Pango mwaka 1933.

Mwisho, tunaweza kusema kwamba historia ya tamthilia ya Kimisri inafanana kwa kiasi fulani na historia ya tamthilia ya Kitanzania, ambapo historia ya tamthilia hizi nchi mbili imeathiriwa sana na fani ya jadi na ujio wa ukoloni. Jambo ambalo tunahitaji kusesitiza kuwa tamthilia ya Kitanzania na Kimisri baada ya uhuru imepiga hatua kubwa kifani na kimaudhui.

## **2.5 Tashititi Katika Tamthilia**

Watalamu mbalimbali wamefanya utafiti katika uga wa tamthilia ya Kiswahili wakiwa na madhumuni mbalimbali. Miongoni mwao ni Ayondi na wenzake (2018) ambaye anaeleza kwamba tashititi ni mbinu ambayo inatumiwa na watunzi kutaja yasiyotajika bila kuchukiza, kuchukuliwa vibaya au kumuudhi msomaji. Tashititi huwasilisha maudhui nyeti kwa njia ya ucheshi. Tashititi haiibui tu ucheshi bali ni ucheshi wenye lengo la kurekebisha. Kwa mnasaba huo, Ligembe (1995) alichambua matumizi ya sitiari katika kazi ya tamthilia ya *Lina Ubani* ikiwa ni moja ya kipengele kinachojenga tashititi katika kazi za fasihi. Katika uchunguzi

wake, amejadili muundo na umbo la tamthilia ya Kiswahili. Amebainisha kiungo, kifananishi na kizungumzwa na kuelezea mchango wake katika uelewa wa tamthilia. Tofauti na watafiti wengine, Ligembe amejikita zaidi katika umbo la tamthilia ya Kiswahili na kubainisha aina za sitiari. Utafiti wa Ligembe umetusaidia kufahamu kwamba sitiari zina mchango mkubwa katika kujenga tashititi na ufutuhi katika kazi ya fasihi. Hivyo, maarifa haya tutayatumia katika utafiti wetu ambapo tukikutana na matumizi ya sitiari katika tamthilia teule tumeimakinikia ili kuweza kubaini kama kuna tashititi ndani yake.

Ramadhani (2005) alifanya utafiti wa matumizi ya sitiari katika tamthilia *Mashetani* ya Ebrahim Hussein na *Ngoma ya Ng'wanamalundi* ya Emmanuel Mbogo. Huu ni utafiti linganishi wa kielimu mitindo ambapo unalinganisha tamthilia mbili. Utafiti huu umechunguza sitiari ambapo ndani ya sitiari ndimo mnapatikana tashititi na pia ni utafiti linganishi. Hali hii imekuwa ni fursa kwetu kujifunza namna utafiti linganishi unavyofanywa ili baadae kazi yetu iwe rahisi. Utafiti wetu unahusu ulinganishi wa tamthilia teule za Kitanzania na Kimisri kwa kujikita katika kipengele cha tashititi.

Mrikaria (2010) katika makala yake ya kejeli na fasihi ya Kiswahili, amebainisha kejeli kama mbinu ya kifani inayotumiwa na wanafasihi kwa ajili ya kufichua ubaya uliopo ndani ya jamii. Katika kubainisha namna mbinu ya kejeli inavyotumiwa kwenye fasihi ya Kiswahili amechukua baadhi ya mifano kutoka tamthilia ya *Kijiji Chetu*, *Lina Ubani* na *Kaptula la Marx*. Makala ya Mrikaria imetusaidia kupata mwanga zaidi wa kuelewa nafasi ya kejeli katika kujenga tashititi katika kazi za fasihi. Kejeli na tashititi ni vitu ambavyo vinakaribiana sana

na hivyo ndani ya tashititi kejeli hujitokeza. Katika utafiti wetu tumekuwa makini kutazama tashititi unaojitokeza ndani ya kejeli na kisha kuweza kubainisha dhamira zilizofichwa ndani ta tashititi.

Boishi na Boibed (2014) wamefanya tasnifu kuhusu tamthilia ya Kifutuhi ya Algeria, na wametaja kwamba tamthilia ya kifutuhi ya kwanza katika Misri ni tamthilia ya *Tatizo la Utawala* ya mwaka 1939 kutoka kwa mwanafasihi maarufu Tawfiq Alhakim ambapo amefanya istihzai juu ya vyama vingi na mambo ya kisiasa nchini Misri. Pia, Alhakim ameandika tamthilia inaitwa *Mikono Laini* ambayo inaongelea ukosefu wa ajira kwa matajiri, hasa baada ya mapinduzi mwaka 1952. Ufutuhi ulikuwa kipengele kizuri katika drama na waandishi wengi wameitumia kama njia ya kukosoa mambo ya kijamii. Mawazo kuhusu ufutuhi ambayo tumeyapata katika kazi hii yatatusaidia kusukuma mbele utafiti wetu ambao umekusudia kuchunguza tashititi katika tamthilia teule za Kitanzania na Kimisri.

Naye, Kiloba (2014) alifanya utafiti kuhusiana na korasi katika tamthilia ya Kiswahili akirejelea tamthilia za Ebrahim Hussein, Emmanuel Mbogo na Frown Nyoni. Matokeo ya utafiti wake yanabainisha kwamba, watunzi hawa ni mahiri sana katika kutumia korasi kama kipengele muhimu cha kufikisha ujumbe kwa hadhira iliyokusudiwa. Utafiti huu umetusaidia kupata uelewa kwamba, korasi katika kazi ya fasihi inaweza kutumika kujenga tashititi yenye kuwasilisha dhamira maalumu kwa wasomaji wa kazi hiyo ya fasihi. Hivyo, tumeyachukuwa mawazo haya na yametusaidia katika kufahamu tashititi mbalimbali katika tamthilia teule kutokana na matumizi ya korasi katika tamthilia hizo. Ingawa hatukuwa tunatafiti

korasi, lakini kazi ya Kiloba imetusaidia katika kupanua zaidi maarifa kuhusiana na matumizi ya tashititi na ujengaji wa dhamira katika kazi za fasihi.

Shabani (2016) alifanya utafiti juu ya kutathmini mbinu za kifutuhi zilizotumika kuibua ucheshi katika tamthilia za *Kaptula la Marx* na *Ushuhuda wa Mifupa*, amedhihirisha kuwa utumizi wa mbinu za kifutuhi katika tamthilia teule umejitokeza kupitia mbinu ya utani, ubeuzi, utwezaji na majazi. Pia, katika upande wa dhamira utafiti wake umebaini kuwa dhamira zilizojitokeza ni nafasi ya mwanamke, anguko la ujamaa, ukoloni mamboleo, utawala wa kidikteta, mapinduzi, ugonjwa wa ukimwi, kulindana kwa viongozi, uchawi na ushirikina.

Utafiti wa Shabani, kwa kiasi kikubwa, umetusadia kuweza kubaini namna tashititi inavyojitokeza katika kazi za tamthilia. Mbinu alizozitaja za kuubaini tashititi zimetusaidia katika utafiti wetu ambapo kwazo tutapata mwanga wa kuweza kubainisha tashititi katika tamthilia teule za Kitanzania na Kimisri. Pia, katika utafiti huo ameweza kubainisha dhamira mbalimbali ambazo zimejengwa kutokana na mbinu za ufutuhi, hili pia limetupatia mwanga katika utafiti wetu. Utafiti wetu umevuka mipaka ya nchi yetu kwa kulinganisha tamthilia teule za mataifa mawili tofauti.

Gwanko (2017) alifanya utafiti wa kulinganisha mbinu za kifutuhi zilivyotumika katika kuelimisha jamii ya Watanzania kuhusu janga la ugonjwa wa UKIMWI katika tamthilia za Ufutuhi za *Embe Dodo* na *Ushuhuda wa Mifupa*. Utafiti huu unakaribiana na wetu na umetusaidia kuona kwamba kumbe jambo ambalo tunakwenda kulishughulikia linawezekana hususani kwa kulinganisha na kulinganua tashititi na dhamira katika tamthilia teule.

Abourweesha (2017) alichunguza mbinu za kisanaa na dhamira katika tamthilia ya *Morani* kwa kutumia nadharia ya Simiotiki na Korasi. Matokeo ya utafiti wake yalibaini kuwa ametumia mbinu za kisanaa kama vile tashibiha, mbalagha, nyimbo, wahusika, motifu na korasi katika kuibua dhamira zinazohusu unyonyaji, umasikini, rushwa, ushujaa na uongozi mbaya. Utafiti huu umekuwa na msaada mkubwa katika kufungua uelewa wetu kuhusu mbinu za kisanaa ambazo ndani mwake ndimo mnamofichwa tashititi. Maarifa haya tumeyafanyia kazi katika utafiti wetu uliochunguza dhamira kupitia tashititi katika tamthilia teule za Misri na Tanzania.

Kayombo (2019) alichunguza sitiari katika tamthilia za Emmanuel Mbogo na kubaini kuwa, mtunzi ametumia sitiari ya uchawi kwa lengo la kuwatesa wananchi. Ndani ya kuteswa huko wanapata ufahamu wa haki zao na kuanza kuzidai. Maelezo haya tunakubaliana nayo kwa msingi kwamba, ndani ya matumizi ya sitairi za uchawi na ushirikina ndimo humo tashititi unapojificha na kuwa na uwezo mkubwa wa kuibua dhamira mbalimbali kwa jamii. Mawazo haya yamesaidia katika utafiti wetu pale ambapo tutaona visa na matukio ya kiuhalisia ajabu tumeyamakinikia kwani ndani yake kutakuwa na tashititi.

Naye, Daniel (2019) alifanya utafiti unaohusiana na tashititi katika fasihi ya Kiswahili na katika matokeo yake ya utafiti alibainisha mbinu za mbalimbali ambazo husaidia katika kubaini tashititi katika kazi za fasihi. Mbinu alizozibainisha ni matumizi ya dhihaka, kejeli, ufyosi, matumizi ya tamathali za semi kama sitiari, tashibiha, ubeuzi, chuku, taswira, maudhui na ujenzi wa wahusika. Vilevile, ameongeza kwamba, dhima za matumizi ya tashititi katika kazi za fasihi zipo katika

makundi matatu ambapo ni dhima za kisiasa, kiuchumi na kijamii. Mawazo ya Daniel (ameshatajwa) ni muafaka katika kusukuma mbele utafiti wetu kwa sababu umetusaidia kufunguwa uelewa wetu juu ya ujitokezaji wa tashititi katika kazi za fasihi. Mawazo haya yamekuwa na msaada mkubwa kwetu katika kuwezesha kupatikana kwa data za utafiti katika tamthilia teule za Kiswahili zilizotafitiwa katika tasnifu hii.

Kwa ujumla, hakuna utafiti mwingi ambao umeshafanywa katika eneo la tashititi na ufutuhi ingawa zipo tafiti chache katika nchi zote mbili za Tanzania na Misri. Hivyo, kufanyika kwa utafiti linganishi kuhusu tashititi katika tamthilia teule za Tanzania na Misri kutasiadia kupata maarifa mapya na kukuza taaluma ya tamthilia na fasihi kwa jumla.

## **2.6 Maudhui Katika Tamthilia Katika Kazi za Fasihi**

Fasihi ya Tanzania na Misri zimejadili maudhui ya kisiasa, kiuchumi na kiutamaduni kutokana na mabadiliko ya maisha. Wamitila (2008) anaeleza kuwa maudhui ni dhana pana inayoweza kuelezewa kwa jinsi mbili ambazo kimsingi zinahusiana. Jinsi ya kwanza ni kuwa maudhui ni jumla ya masuala au mambo yanayoshughulikiwa katika kazi ya kifasihi. Masuala haya hutokana na jinsi mtunzi au mwandishi anavyoiteua mada ambayo ni msingi wa utunzi wa kazi yake. Jinsi ya pili ni kutumia maudhui kurejelea kiwango cha kimaana cha matini au kazi ya kifasihi. Maudhui hujumulisha vipengele vingine kadha: dhamira, itikadi, msimamo, maadili, mafunzo na falsafa japo sio lazima kwa kila kazi ya fasihi kuwa na vipengele hivi.

Abdelaal (1997) alichunguza athari za Kiarabu na kigeni katika tamthilia ya *Salah Abdulsabur*. Ametaja kwamba, zipo athari nyingi ndani ya tamthilia hiyo inayohusu utamaduni, desturi na mila za mataifa mengi dunaini. Kazi ya mtaalamu huyu imeendelea kukuza maarifa yetu kwa kutambua kwamba, tamthilia moja inaweza kueleza masuala ya jamii au mataifa kadhaa kwa wakati huohuo. Tamthilia za aina hii ni nzuri sana katika kukuza na kuhamsisha utalii, uwekezaji na kukuza ushirikiano baina ya jamii moja na nyingine. Mawazo haya tutayatumia katika utafiti wetu ambapo bila shaka ndani ya tamthilia teule ni jambo la kawaida kuona mifano ya jamii mbalimbali ikijitokeza.

Mahmoud (2004) ameandika tasinifu juu ya tamthilia ya kisiasa katika Misri kutoka 1980 mpaka 2000. Tamthilia ya kisiasa katika muda huu ilikuwa inaongelea demokrasia, tatizo la Mashariki ya Kati, utandawazi na udikteta. Pia, ametaja kwamba tamthilia katika muda huo zimeongelea sana kuhusu Ukoloni wa mamboleo kupitia uchumi na utamaduni. Sambamba na hayo, amegusia kuhusu vipengele vya fani katika tamthilia ya kisiasa kama wahusika, ploti, maongezi na mazingira. Utafiti wa Mahmoud ni muhimu katika kusukuma mbele utafiti wetu kwa msingi kwamba utaja mambo ambayo yanatupatia maarifa na mwanga wa kuweza kubainisha tashititi katika tamthilia teule za Kitanzania na Kimisri.

Fayez (2016) aliandika kitabu juu ya hadithi za jadi kwenye tamthilia ya kisasa ya Kimisri (1971- 2005), kataja maana ya hadithi ya jadi na asili yake; na kataja masuala ya kisiasa na kijamii kama uadilifu, utawala, upendo na amani. Fani jaadiya au haduthi za kijadi zina mchango mkubwa katika ujenzi wa tamthilia za Kiswahili. Inaelezwa pia, asili na chimbuko la tamthilia ni kutokana fani za kijadi

ikiwemo hadithi. Kwa muktadha huo, utafiti wetu tunapaswa kusoma kwa makini tamthilia teule za Kitanzania na Kimisri na pale tutakapoona hadithi ikijitokeza ndani ya tamthilia teule ndani yake kukawa na tashititi ambao tunautafiti katika kazi yetu.

Nicholaus (2011) aliandika tasinifu juu ya Ubuntu katika tamthilia za Penina Muhando na kufanikiwa kubaini kwamba, tamthilia hizo zimesheheni masuala ya ubuntu kama vile dhana kuhusu utu, ndoa, kuamini miungu, kuishi kijamaa na masuala ya kifo ambayo ni miongoni mwa masuala yanayopewa nafasi kubwa sana katika jamii za kibantu. Ingawa yeye hakuwa anatafiti kuhusu tashititi, lakini tuliposoma utafiti wake tuliweza kubaini kwamba, masuala hayo ya falsafa ya Ubuntu aliyoyabainisha yamejengwa kwa kutumia mbinu mbalimbali kiwemo tashititi. Kutokana na kulifahamu hilo na kupata maarifa ya kutosha kuhusu matumizi au ujitokezaji wa tashititi katika fasihi tumeweza kuchambua na kuwasilisha tashititi na dhamira katika tamthilia teule za Kiswahili na za Kiarabu kutoka Tanzania na Misri mutawalia.

Massoud (2013) amefanya utafiti juu ya maudhui na fani katika tamthilia za *Mashetani* na *Kivuli Kinaishi*. Utafiti wake uligundua kuwa, kazi hizi mbili zinafanana katika maudhui yanayohusu Ukoloni mamaboleo, ujenzi wa jamii mpya, rushwa, uongozi mbaya, matumizi mabaya ya madaraka na nafasi ya mwanamke. Utafiti huu umetusaidi kujua zaidi kuhusu Fasihi Linganishi na tunapata taarifa kuhusu maudhui muhimu yanashughulikwa na waandishi wa tamthilia katika Tanzania. Utafiti huo, umesaidia kupata uelewa na mwanga mpana katika vipengele vya fani ambavyo vinajitokeza katika kazi za tamthilia. Kupitia ufahamu huo



tutaweza kukamilisha malengo ya utafiti wetu ambao unakusudia kuchunguza dhamira kupitia tashititi katika tamthilia teule za Kitanzania na Kimisri.

Mwirabua (2014) alifanya utafiti kuhusu Ukoloni mamboleo na utandawazi katika tamthilia teule. Utafiti huu umechunguza jinsi Ukoloni mamboleo unavyodhihirika katika muktadha wa utandawazi kwa kurejelea tamthilia za *Posa za Bikisiwa* (2008) ya S. A. Mohamed na K. King'ei na *Sudana* (2006) ya Alamin Mazrui na K. Njogu. Tamthilia hizi mbili zimetumia mtindo tofauti wa kuwashilisha maudhui yake. Mchango mkuu wa kazi umeonesha kuwa utandawazi ni mbinu mpya ya kuendeleza Ukoloni mamboleo. Utafiti huu unabainisha maudhui muhimu na yanayozingatiwa zaidi kwenye tamthilia.

Pia, Mapunjo (2014) alifanya utafiti kuhusu usawiri wa mwanamke kama kiongozi katika tamthilia za *Kivuli Kinaishi* na *Nguzo Mama*. Katika matokeo ya utafiti wake, alibainisha kwamba, mwanamke anasawiriwa kama kiongozi mzuri ambaye anaweza kuleta maendeleo katika jamii yake kwa namna chanya hasa katika kuwaunganisha wananchi kuwa na umoja na mshikamano katika ujenzi wa taifa au jamii yao. Pia, baadhi ya wanawake hugeuka na kuwa wasaliti wa wananwake wenzao kwa kuwachukia na kuwazushia vitu vya uongo kwa chuki jambo ambalo linarudisha nyuma nafasi ya mwanamke katika uongozi na kujikomboa. Utafiti wa Mapunjo ni muhimu sana katika kusukuma mbele utafiti wetu ambao ni linganishi kama huu wake, isipokuwa utafiti wetu unahusisha tamthilia teule za mataifa mawili ya Tanzania na Misri. Suala la mwanamke na uongozi ni jambo mtambuka ambalo linajitokeza katika jamii mbalimbali duniani na hivyo basi tutaona ni kwa kiwango gani linajitokeza katika kazi teule za Kitanzania na Kimisri.

Vilevile, Muhando (2015) alichunguza dhamira za kijamii katika tamthilia ya *Hatia* ya Penina Mlama na kufanikiwa kubainisha dhamira za uongo, penye ukweli uongo hujitenga, nafasi ya mwanamke katika jamii, umasikini na matabaka. Pia, alibainisha mbinu za kisanaa ambazo zimetumika katika kuibua dhamira kwenye tamthiliya ya *Hatia* kuwa ni mbinu za matumizi ya nyimbo, takriri, tafsida na muundo wa moja kwa moja. Matokeo ya kazi ya Muhando (ameshatajwa) yametusaidia sana katika kuiona mbinu ya tashihiti inavyotumika katika kazi za fasihi kwenye kujenga dhamira. Ingawa yeye hakuwa anachunguza tashititi na wala hakuna popote alipoizungumzia, lakini tuliposoma uchambuzi wake wa data tuliweza kuona tashihiti zikijitokeza na kundelea kukuza uelewa wetu katika mbinu ya tashititi kwenye kuibua au kujenga dhamira.

Shemweta (2015) alifanya utafiti juu ya Itikadi katika tamthilia za Emmanuel Mbogo za *Ngoma ya Ng'wanamalundi* na *Fumo Liongo*. Katika utafiti huo, ameonesha kuwepo kwa itikadi ya ushirikina wa kichawi na kiganga, mapinduzi, ujamaa, ubepari, utamaduni, mapenzi na ndoa na dini zimejitokeza katika tamthilia ya *Ngoma ya Ng'wanamalundi*. Kwa upande wa *Fumo Liongo*, itikadi za masuala ya sihiri, utawala wa milele, mapenzi ya dhati kwa jamii na malezi na uzazi zimejitokeza. Pia, umeonesha kuwa itikadi katika tamthilia teule zinajengwa kwa kutumia mbinu mbalimbali za kisanaa kama tamathali za usemi za tashibiha, sitiari, kejeli, takriri na misemo tu ndizo zilizotafitiwa. Utafiti wa Shemweta umetusaidia kusukuma utafiti wetu kwa maana kwamba umetoa mchango katika kukuza uelewa wetu juu ya Fasihi Linganishi.

Nzilu (2018) alichunguza taswira katika tamthilia za Said Ahmed Mohamed za *Pungwa, Kivuli Kinaishi* na *Mashetani Wamerudi*. Katika utafiti huu, alibaini kwamba, taswira mbalimbali ambazo mwandishi amezitumia zina mchango mkubwa katika ujenzi wa maudhui ya tamthilia hizo. Miongoni mwa maudhui ambayo yameibuliwa ni pamoja na rushwa, uongozi mbaya, dhuluma, uonevu, kutozingatiwa kwa haki katika jamii, ujenzi wa jamii mpya, umoja na mshikamano katika jamii na Ukoloni mamboleo. Utafiti wa Nziku ni muhimili muhimu katika kusukuma mbele utafiti wetu kwa kuwa dhana ya ulinganishi wa kazi za fasihi tuliyokuwa nayo imeendelea kukua na kuimarika zaidi.

Didas (2019) alifanya utafiti kuhusu usawiri wa mwanamke katika tamthilia ya kimfumojike kwa kurejelea tamthilia za *Mama Mtakatifu* na *Kivuli Kinaishi*. Utafiti wake ulihusisha tamthilia mbili ikiwa ni moja kutoka Tanzania na nyingine kutoka Kenya. Matokeo ya utafiti wake yanaonesha kwamba kuna mfanano mkubwa katika usawiri wa mwanamke kwa jamii ya Tanzania na Kenya kuliko inavyotofautiana. Hii ni kwa sababu, Kenya na Tanzania ni nchi jirani na zote zipo katika ukanda wa Afrika ya Mashariki. Kufanyika kwa utafiti wetu ambao unahusu tamthilia teule za Tanzania na Misri kumesiadia katika kuibua mambo mapya.

Mwakanjuki (2022) ameandika tasinifu kuhusu motifu katika tamthilia za Emmanuel Mbogo na kufanikiwa kubainisha motifu za aina mbalimbali. Miongoni mwa motifu hizo ni ile ya safari ambapo wahusika wanasafiri kutoka sehemu moja kwenda nyingine na kujenga dhamira mbalimbali ndani ya tamthilia husika. hapana shaka kuwa ndani ya safari za wahusika ndiko ambako kunajengwa tashititi na dhamira. Utafiti huu umetusaidia kupanua mawazo yaetu na kukuza maarifa

kwamba tunapochunguza ujitokezaji wa tashititi na dhamira katika tamthilia teule za Kitanzania na Misri.

Kazi zote zilizopitiwa katika sehemu hii zinaonesha kwamba, utafiti linganishi umefanywa zaidi katika kazi za tamthilia za jamii moja au kazi za watunzi wa nchi moja na zile za nchi na nchi ni chache sana. Hivyo, yanayofahamika kuhusu ulinganishi wa tamthilia za Tanzania na Misri ni kwamba hayapo na kufanyika kwa utafiti wetu kumesaidia kutoa maarifa mapya ya kusukuma mbele taaluma ya tamthilia za Kitanzania na Kimisri.

## **2.7 Pengo la Utafiti**

Kutokana na mapitio ya tafiti tangulizi na machapisho mbalimbali zilizochunguzwa, mtafiti ameona kwamba, machapisho na tafiti nyingi zimeelezea maudhui yanayojitokeza kwenye tamthilia. Utafiti unaolenga kulinganisha dhamira kupitia tashititi katika tamthilia ya Kiswahili na ya Kiarabu kwa kadiri ya uelewa wetu, bado haujafanyika. Tasinifu hii imelishughulikia pengo hilo kwa kulinganisha na kulinganua dhamira kwa kurejelea tamthilia teule za nchini Tanzania na Misri.

## **2.8 Mkabala wa Kinadharia**

Nadharia ni utaratibu unaoeleza jambo lilivyo au linavyotakiwa kuwa kwa mujibu ya utamaduni, mazingira na kanuni za jamii inayohusika. Katika maisha, hakuna jambo linalofanywa bila ya kuongozwa na nadharia fulani; na inapotokea suala hilo limefanywa vibaya, ni rahisi wanajamii kubaini na kueleza kuwa limefanywa bila ya kuzingatia kanuni au utaratibu unaohusika. Katika utafiti huu, nadharia ya

Simiotikina nadharia ya Fasihi Linganishi na ile ya Usosholojia zimeongoza uchambuzi na mjadala wa data zilizowasilishwa.

### **2.8.1 Nadharia ya Simotiki**

Simiotiki ni nadharia inayotumika katika uchambuzi wa taaluma zinazohusiana na masuala ya lugha kama isimu na fasihi. Nadharia hii imeasisiwa na Ferdinand de Saussure katika kitabu chake kiitwacho *A Course of General Linguistics*, (de Saussure, 1966). Nadharia ya Simiotiki inahusishwa sana na matumizi ya lugha ya ishara na uashiraji ambapo watunzi wa kazi hutumia kitaja fulani kurejelea kitajwa zaidi ya kimoja au tofauti kabisa na kitaja.

Mtunzi wa kazi ya fasihi anaweza kutumia neno moja, lakini lina maana nyingi na tofauti. Baadhi ya wataalamu wanasema kwamba Ferdinand de Saussure na Charles Pierce ni waasisi wa nadharia hii ya Simiotiki. Saussure katika nadharia hii ameeleza dhima ya ishara katika jamii na Pierce amezungumzia maana halisi ya lugha ya ishara inavyohusiana kimantiki na utamaduni wa jamii fulani kwa madhumuni ya kutoa maana maalum.

Semiotiki ni nadharia inayoshughulika na ishara pamoja na uashiraji katika kazi za kifasihi. Ishara zinazojitokeza katika fasihi huundwa na mtunzi kwa kuzingatia muktadha wa jamii na binadamu ndiye mtengenezaji wa alama mbalimbali za ishara ambazo huzitumia katika mawasiliano yake ya kila siku. Semiotiki ni taaluma ya mfumo wa alama katika mawasiliano ya kutumia lugha (Wamitila, 2002). Hadhira inayolengwa hutengeneza maana mbalimbali kupitia ubunifu na tafsiri zao juu ya alama na ishara inazokutana nazo katika kazi za kifasihi inazosisikiliza au kuzisoma.

Katika taaluma ya lugha, kiashiria na kiashiriwa ni vitu viwili vinavyosaidia mawasiliano. Kiashiria ni alama, sauti au herufi zinazotumika kutaja jina la kitu fulani. Kiashiriwa ni kitu halisi kinachorejelewa na alama au herufi zinazotaja taarifa ya kitu hicho. Mathalani, neno ‘paa’ hurejelea vitaja mbalimbali kama vile ‘mnyama wa porini aliyefanana na mbuzi’ na ‘sehemu ya juu inayofunika nyumba’. Neno ‘paa’ linarejelea vitu viwili tofauti. Jambo hili linathibitisha kuwa hakuna uhusiano wa moja kwa moja baina ya kitaja na kitajwa. Inawezekana kabisa ikawa hakuna uhusiano kati ya kitaja na kitajwa, isipokuwa kama wanajamii wamekubaliana juu ya matumizi yake.

Binadamu ndiye mtengenezaji na mnyambulishaji wa ishara zinazotumika katika kazi za kifasihi (Wamitila, 2002). Hadhira hutengeneza maana kupitia ubunifu na tafsiri zao juu ya alama hizo. Binadamu hufikiri kwa kutumia alama ambazo zinakuwa katika mfumo wa maneno, picha, sauti na matendo. Kitu chochote kitakuwa alama kama watu watakifasiri kama kitu kitasimama kwa niaba ya kitu kingine badala ya chenyewe. Hivyo, watunzi wa kazi za fasihi huweza kutumia lugha ya picha na ishara kurejelea matendo na tabia za mwanadamu ili kuwafunza wanajamii masuala mbalimbali kulingana na mahitaji ya jamii yao.

Wamitila (2002) anaeleza kuwa matumizi ya ishara yanayoundwa na mtunzi wa kazi ya fasihi ni lazima yalandane na mazingira ya jamii ya kisiasa, kiuchumi na kiutamaduni. Nadharia hii imetumika sana katika uchambuzi wa kazi za kifasihi, ambapo inashughulikia ishara na uashiraji. Ishara zinazojitokeza katika kazi za kifashi huundwa na mtunzi kwa kuzingatia muktadha wa jamii wa kiuchumi, kisiasa, kijamii na kiutamaduni.

Barthes (1994) aliendeleza mjadala kwa kuigawa nadharia ya Semiotiki katika misimbo mitano. Misimbo hiyo ni ule wa kimatukio, kiseme, kihemenitiki, kirejelezi na kiishara. Kila msimbo ulipewa eneo maalumu la kushughulikia. Misimbo hiyo hutumika katika kazi za kifasihi kurejelea masuala mbalimbali yaliyomo katika jamii. Mihimili hiyo imejenga misingi yake katika kuzifumbua ishara zilizotumika katika kazi ya fasihi. Nadharia ya Simiotiki humsaidia mtafiti au mhakiki wa kazi ya fasihi kuweza kubainisha lugha ya ishara iliyotumika katika kazi ya fasihi na kuweza kusema hapa kuna dhamira fulani. Pia, imeteuliwa kutumika katika kuchambua data za utafiti huu kwa sababu inahusiana na mada ya utafiti wetu.

Msimbo wa kimatukio huu unahusika na kutazama namna matukio yanavyowasilishwa katika kazi ya fasihi kwa msimbo ambapo ndani yake ndimo mnakuwa na dhamira (Mark, 1995). Kwa mfano, inawezekana kukawa na tukio linafanywa na kiumbe sungura au fisi, lakini ujumbe unaotokana na tukio hilo unajenga dhamira maridhawa kwa jamii. Hivyo, msimbo wa kimatukio umemsaidia mtafiti katika kuchambua data na kujibu maswali ya utafiti wake kama ilivyokusudiwa.

Msimbo mwingine wa nadharia ya Simiotiki ni wa Kihemenitiki ambao wenyewe unahusu anuani ya kifasihi na namna anuani hiyo inavyojenga dhamira kwa wasomaji au wasikilizaji wa kazi ya fasihi (Solomon, 1988). Kupitia msimbo huu, mtafiti ameweza kupata uelewa mpana wa majina ya vitabu vya tamthilia husika na kuweza kuhusianisha na yaliyomo ndani ya kazi hizo na kisha kupata tashititi na dhamira zitokanazo na tashititi hizo.

Pia, kuna msimbo wa kiseme ambao huu unahusiana na elementi nasibishi ya kisemantiki ya maneno yanayotumika katika kazi ya fasihi. Katika kuibua baadhi ya tashititi katika tamthilia teule msimbo wa kiseme umemwezesha mtafiti kuzipata dhamira kwa kuhusisha maana ya msingi na maana nasibishi ya tashititi husika kama zilivyotumiwa katika tamthilia teule.

Msimbo wa kiishara kwa upande wake husaidia kuweza kubaini maana au dhamira katika kazi ya fasihi kwa kurejelea ishara na picha zinazojengwa katika kazi hizo (Chandler, 1992). Mtafiti aliweza kubaini tashititi mbalimbali zilizowasilishwa kwa lugha ya ishara ya picha na kueleza tashititi hizo zinawasilisha dhamira gani.

Msimbo wa kiutamaduni au kiurejelezi husaidia katika kubaini misimbo inayojengwa kwa kurejelea utamaduni wa jamii na kusaidia katika kujenga dhamira za kazi ya fasihi (Umerto, 1976). Masuala ya mila na desturi za jamii hutumiwa kimsimbo kwa lengo la kujenga dhamira maalumu na kuifikisha kwa hadhira. Msimbo huu umemsaidia mtafiti kuweza kubaini tashititi mbalimbali na namna zilivyosaidia katika kuibua dhamira katika tathiliya teule za Kitanzania na Kimisiri.

Hivyo, katika tasnifu hii, mtafiti aliitumia nadharia ya Simiotiki kuchunguza ishara, picha na taswira zilizomo katika tamthilia teule ili kubaini dhamira zilizojengwa kupitia tashititi. Pia, kitu chochote kitakuwa alama kama watu watakifasiri kwa niaba ya kitu kingine. Hoja hii ndiyo inayojenga msingi wa uteuzi wa nadharia ya Simiotiki iliyochunguza kipengele cha tashititi namna kinavyojenga dhamira katika tamthilia zilizolengwa.



### 2.8.2 Nadharia ya Usosholojia

Nadharia ya Usosholojia huikabili kazi ya fasihi kwa kuangali jinsi inavyohusiana na mazingira ya kijamii Msokile (1992). Wamitila (2003) anaeleza kuwa nadharia hii hutumiwa na wahakiki au wanahistoria ambao nia yao ni kuthibitisha jinsi kazi fulani ilivyoathiriwa na vitengo fulani vya mazingira kama vile tabaka la mwandishi, jinsia yake, matamano yake, mtindo wa uwazaji, muktadha wa kiuchumi, tabaka la kijamii ya hadhira na thamani za hadhira lengwa.

Kulingana na *Encyclopaedia Britannica Online* (2011) mwasisi wa nadharia hii ni Germaine de Stael (1766 – 1817) mwanzoni mwa karne ya 19. Kazi hizi zina wingi wa mawazo mapya na mielekeo mipya. Nadharia yake ya kimsingi ni kwamba, kazi ya kifasihi lazima ionyeshe uhalisi wa kimaadili na wa kihistoria, na hali ya kitamaduni, kimaadili, kiroho na kisiasa; na mitindo ya uwazaji ya taifa ambamo kazi ya kifasihi imetungwa. *Enclopaedia Britannica Online* (2011) wanaeleza kuwa mawazo ya de Stael yalichukuliwa na Hippolyte Taine (1828 – 1893), akayaunda upya na kuyakuza. Kwa sababu hii, anachukuliwa kuwa mwasisi wa nadharia ya Usosholojia ya fasihi.

Wellek na Warren (1978) wanasema kuwa, kwa kawaida, fasihi huibuka ikiwa na uhusiano wa karibu na asasi fulani za kijamii. Wanatoa rai kuwa fasihi ina uamilifu wa kijamii ambao hauwezi kuwa wa mtu mmoja binafsi. Kwa sababu hii, maswali mengi ambayo huibuka katika uchanganuzi wa kifasihi aghalabu huwa masuala ya kijamii. Uhusiano baina ya fasihi na jamii hujadiliwa kwa kutanguliza ufungamano wa fasihi na jamii. Wahakiki wa dhana hii wanadai kuwa ni makosa kuchukua fasihi kama kigezo cha kuashiria jinsi jamii yoyote ile ilivyo.

Pia walidai kuwa, kazi kama zile za mwandishi maarufu Shakespeare na tenzi za Milton au kazi ya Burke haziwezi kuchukuliwa kama kiashiria cha jamii zao. Jinsi mwandishi anavyowasilisha kazi yake hutegemea tajriba, uzoefu na mtazamo wake kuhusu maisha. Hivyo itakuwa si kweli kufikiri kuwa kazi ya mtu binafsi ni kiashiria cha maisha ya jamii kwa ujumla katika jamii anamotoka. Mtazamo wa fasihi kupitia nadhari hii, hutufanya tumchukue mwandishi kama zao la nguvu za kiUsosholojia za wakati wake na kuepuka kumpunguzia sifa za ubunifu asilia.

Kulingana na James Sutherland (1957), mwandishi hutegemea kipindi alichandika, tabaka ambamo alizaliwa, elimu aliyopokea pamoja na dini yake. Wahakiki wanashikilia dhana kwamba uchunguzi wa fasihi unahitaji tuwe na wazo kuhusu kile ambacho ni muhimu na kile ambacho si muhimu. Wahakiki wanaopinga mbinu ya kiUsosholojia hawapingi kuwepo uhusiano baina ya fasihi upande mmoja na hali ya kijamii, uchumi na siasa upande mwingine. Uchunguzi wa kijamii kuhusu kazi ya maandishi au mwandishi mwenyewe utatusaidia kumchunguza mwandishi kama mwanachama wa jamii, athari za kijamii zilizomwathiri na kumpatia msukumo wa kubuni kazi ya sanaa.

Wa Thiong'o (1978) anaeleza kuwa fasihi ina uhusiano na maisha ya kila siku ya jamii kwani haikui (fasihi) wala kuchipuka katika ombwe tupu. Anatoa rai kuwa, fasihi hupewa msukumo, umbo, mwelekeo na upeo na nguvu zinazotoka katika jamii. Pia, Njogu na Chimerah (1999) wameeleza kuhusu nadharia ya Usosholojia inayofungamanisha fasihi na jamii, hasa katika nchi zinazoendelea kwa sababu huthibitisha kuwa fasihi ni kielelezo cha ukweli uliopo katika jamii.

Wamitila (2005) anaashiria kupendelea nadharia ya Usosholojia ya fasihi kwani anasema kuwa, ni lazima kazi ya mwandishi yeyote iakisi mazingira yake, siasa ya nchi yake na mambo mengine ambayo yanamhusu. Kutokana na maelezo ya nadharia ya Usosholojia ya fasihi ambayo tumeyaeleza katika sehemu hii yatatufaa katika utafiti wetu. Kwa hiyo, tumeitumia nadharia ya Usosholojia ya fasihi kuihakiki dhamira ndani ya tamthilia teule. Fasihi inaweka wazi uhalisi uliopo katika jamii kwa kuyasawiri mambo vile yalivyo bila kuupendelea upande fulani.

Nadharia hii huitambua nafasi kubwa inayochukuliwa na muktadha wa kijamii katika uhakiki wa tamthilia teule kwa kuzingatia umithilishaji wa hali fulani za ulimwenguni tamthilia teule zimefasiriwa ndani ya muktadha wa jamii ya msanii na historia yake. Mtafiti alichunguza uhusiano uliopo baina ya jamii na mwenendo wa shughuli zao za kila siku na mitazamo yao. Pia, ulichunguzwa uhusiano wao, historia na maendeleo ya jamii yao katika nyanja zote za kijamii. Hali hii ilimwezesha kuvichunguza vitabu teule kwa kina ili kubaini dhamira zake kulingana na utamaduni, mazingira na hali halisi ya maisha.

Vitabu teule vilichunguzwa kwa kuyasawiri mandhari, wahusika na utamaduni wa mataifa teule unavyoaminika na kukubalika katika jamii ya wakati wake. Tamthilia zilizolengwa zilichunguzwa moja kwa moja kwa kurejelea uhusiano uliopo baina ya shughuli za kijamii, fasihi na mazingira. Vitabu teule vilichunguzwa kama sehemu kamili ya utamaduni wa jamii za Tanzania na Misri kwa kuzingatia hali ya maisha, utamaduni na mazingira yake. Uhusiano uliopo baina ya mataifa teule na tamthilia teule ndio unaoyachukua masuala yaliyomo katika jamii na kuyaweka kama yalivyo katika vitabu vyao.

Katika uhakiki na mjadala wa data, mtafiti aliwaweka waandishi wa tamthilia teule katika ulimwengu wao wa kawaida na halisi. Pia, walichunguzwa kwa undani namna walivyoyachora masuala ya kijamii na kuyaweka katika kazi zao kama yalivyo na kukubalika kupitia tamthilia zao. Vitabu vyao vilichambuliwa moja kwa moja bila chuku ili kufanya uhakiki wa ndani na wa kina. Nadharia ya Usosholojia iliteuliwa na kuwekewa misingi katika uchunguzi wa kipengele cha dhamira katika tamthilia teule. Eneo la utafiti lilipewa uzito ili kuonesha uhusiano uliopo kati ya nchi ya Tanzania na Misri na tamthilia zilizofanyiwa uchunguzi.

### **2.8.3 Nadharia ya Fasihi Linganishi**

Nadharia ya Fasihi Linganishi imeelezwa na wataalamu mbalimbali. Boldor (2003) akimnukuu Remak (1971) anaeleza kuwa, Fasihi Linganishi ni taaluma ya fasihi inayovuka mipaka ya zaidi taifa moja na kuonesha uhusiano uliopo baina taaluma ya Fasihi na taaluma nyenginezo kama sanaa, falsafa, historia, sayansi jamii, dini na nyenginezo. Wamitila (2003) anaona kuwa, Fasihi Linganishi ni mbinu ya kuchunguza na kuchambua sifa za mfanano na tofauti zilizopo katika matini ya fasihi. Ulinganishi na ulinganuzi hufanyika katika mihimili mikuu ya fani na maudhui. Jilala (2016) anashadidia; Fasihi Linganishi ni taaluma inayohusika na ulinganishi na ulinganuzi wa kazi za fasihi za mwandishi / waandishi wa ndani na nje ya mipaka ya kitaifa, kibara na kilimwengu. Kwa muhtasari, Fasihi Linganishi ni nadharia mahsusi ya uchambuzi wa kazi mbalimbali za fasihi, inayojihusisha katika kulinganisha na kutofautisha fasihi ya taifa au bara moja na taifa au bara jengine, mwandishi au waandishi wa jamii moja au tofauti, mwandishi mmoja kupitia kazi zake za vipindi tofauti kwa kuzingatia misingi mikuu ikiwemo ya fani na maudhui na katika utanzu stahiki (Wellek, 1988).

Miongoni mwa waasisi wa mwanzo wa nadharia hii ni pamoja na Paul Van Tieghem, Marius Franco na Hutchenson Macaulay Posnett. Steven Totosy de Zepetnek, kuanzia karne ya ishirini (20) ndio nembo na mtetezi katika nadharia hii. Zepetnek ameandika kazi za Fasihi Linganishi zaidi ya vitabu ishirini (20) na makala mia moja na hamsini (150) hasa akiwa Chuo Kikuu cha Martin Luther King. Miongoni mwa kitabu maarufuni: “*Comparative Literature: Theory, Method and Application* (1998)” Zepetnek alisaidia sana kuikuza na kuieneza taaluma hii kwa kiwango kikubwa ulimwenguni kote. Kwa sasa, taaluma hii imeundiwa jumuiya ya kimataifa: “*International Comparative Literature Association (ICLA)*” inayoshirikiana na vyama vya mataifa mbalimbali ulimwenguni: Kama; Ufaransa (FCLA), Marekani (ACLA); Urusi (RCLA); Ujerumani (GCLA); Uingereza (BCLA). Vyama hivi hushirikiana na baadhi ya mataifa madogo. Kwa mfano, Tanzania hushirikiana na Ujerumani na Uingereza (Ponera, 2014).

Nadharia ya Fasihi Linganishi nchini Tanzania, bado haijafikia katika kiwango cha juu sana. Licha ya hayo, baadhi ya vyuo vikuu vinafundisha taaluma hiyo, mfano wa Vyuo vikuu hivyo ni Chuo Kikuu Huria cha Tanzania (OUT), Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM), Chuo Kikuu cha Dodoma (UDOM) na Chuo Kikuu Kishiriki cha Elimu Mkwawa (MUCE). Vilevile, taaluma ya Fasihi Linganishi kama nadharia imeanza kuimarika. Tafiti kadhaa zinaendelea kufanywa zikitumia nadharia hii kwa lengo la kupitita kazi za mwandishi mmoja kwa vipindi tofauti, waandishi na tanzu tofauti. Miongoni mwa tafiti hizo ngazi ya Uzamili na Uzamivu ni utafiti wa Ligembe (1995), Ramadhani (2005), Massoud (2013), Mkuwili (2014), Fadhili (2014), (Jilala, 2016) na Massoud (2018), Calium (2018) na Ismail (2019).

Fakih (2017) akimnukuu Zepetnek (1998:15-18) amebainisha misingi kumi (10) ya Nadharia Fasihi Linganishi:

- i) Fasihi Linganishi ni nadharia inayofunza kutambua mbinu na stadi sahihi katika mafunzo ya uhusiano wa Fasihi Linganishi na tamaduni nyengine.
- ii) Fasihi Linganishi ni nadharia na mbinu inayodaiwa kujikita hasa katika uhusiano baina ya Utamaduni, Lugha, Fasihi na Maarifa.
- iii) Fasihi Linganishi ni nadharia inayomtaka mwana-Fasihi Linganishi kuwa na uwezo mkubwa wa kutambua Lugha na Fasihi za jamii mbalimbali.
- iv) Fasihi Linganishi ni nadharia inayohusishwa na stadi nyingine kama (Sanaa, Filamu, Utamaduni na Maigizo) na taaluma ya Sayansi Jamii katika fani zake kama (Historia, Usosholojia na Saikolojia)
- v) Fasihi Linganishi ni nadharia inayotilia mkazo kujifunza Fasihi na Lugha ya Kiingereza iliyokitwa katika taaluma nyingi za nasaba yake.
- vi) Fasihi Linganishi ni nadharia na mbinu inayolenga katika utafiti na uchambuzi kwa lengo la kutolea ushahidi juu ya ubora na udhaifu.
- vii) Fasihi Linganishi ni nadharia na mbinu inayohusishwa na mwamko wa kimawazo na kiitikadi ya siasa yake katika uchambuzi/uhakiki.
- viii) Fasihi Linganishi ni nadharia inayohusishwa na uhusiano wa kimaudhui baina ya kazi za sanaa kiuhalisia au udhanaishi kitaifa na kiulimwengu.
- ix) Fasihi Linganishi ni nadharia inayohamasisha matumizi ya mfumo wa mawasiliano ya Sayansi na Teknolojia katika utekelezaji wa maendeleo kwa ujumla na kuhadharika juu ya jamii, utaifa, jinsia, na mafunzo mengineyo.

- x) Fasihi Linganishi ni nadharia inayofunza kuwa mweledi / mjuzi wa matumizi ya kinadharia katika fasihi, sanaa kwa matumizi stahiki.

Sababu ya uteuzi wa nadharia ya Fasihi Linganishi ni kufanikisha vyema lengo mahsusi linalohusiana na kufanana na kutofautiana kwa dhamira katika tamthilia teule za Misri na Tanzania. Vilevile, nadharia ya Fasihi Linganishi imekuwa na historia yake katika kazi na tasnifu mbalimbali za watafiti. Watafiti wametumia nadharia hiyo kwa lengo la kufananisha na kutofautisha kazi husika kulingana na utanzu, misingi / mihimili ya nadharia, malengo, maswali na mada za utafiti. Hivyo, katika utafiti huu, nadharia ya Fasihi Linganishi imetusaidia kutimiza lengo mahususi la pili la tasnifu yetu ambapo tumeweza kulinganua dhamira zinazoibuliwa na tashititi katika tamthilia teule za Misri na Tanzania.

## **2.9 Hitimisho**

Sura hii imeshughulikia kazi tangulizi zinazohusiana na mada ya utafiti ili kupata maarifa na maoni ya wanazuoni waliotangulia. Pia, imeongezea taarifa na ujuzi katika mada iliyoshughulikiwa. Baadhi ya vipengele vilivyochunguzwa katika sura hii ni utafiti dhana ya tamthilia, chimbuko na maendeleo ya tamthilia na mapitio yanayohusiana na maudhui na tashititi katika tamthilia. Pia, nadharia za Usosholojia, Semiotiki na Fasihi Linganishi zilizoongoza mjadala wa data zilizowasilishwa zimejadiliwa katika sura hii. Nadharia hizi ziliteuliwa kwa sababu zinategemeana na kukamilishana ili kukidhi malengo mahususi utafiti.

## SURA YA TATU

### MBINU ZA UTAFITI

#### 3.1 Utangulzi

Sura ya tatu inahusu mbinu za utafiti zilizowezesha kupatikana kwa data za msingi zilizowasilishwa katika utafiti huu. Mbinu hizo huonesha na kueleza namna mtafiti alivyokusanya data, alivyozechambua na kuziandikia taarifa ya utafiti uliokwishafanyika (Cresswell, 2009). Baadhi ya mada zilizojadiliwa katika tasnifu hii ni usanifu wa utafiti, uteuzi wa sampuli, vyanzo vya data, mbinu za ukusanyaji wa data na maadili ya utafiti. Mbinu hizo zilitumika kumwongoza mtafiti katika ukusanyaji wa data zilizomwezesha kufikia malengo mahsusi ya utafiti.

#### 3.2 Usanifu wa Utafiti

Usanifu wa utafiti ni ramani inayoonesha namna utafiti utakavyofanyika tangu hatua za kukusanya data mpaka kuandika taarifa ya utafiti (Kothari, 2008). Ramani ya utafiti huonesha namna data zitakusanywa. Mbinu ya uchunguzi kifani ilitumika katika utafiti huu. Mbinu hii humruhusu mtafiti kuteua eneo maalumu atakalolichunguza katika utafiti wake. Katika tasnifu hii, tumeteua tamthilia ya *Embe Dodo* (Dominicus Makukula), *Kaptula la Marx* (Euphrase Kezilahabi), *Wananchi Wanapotoroka* (Mahmoud Altokhy) na *Bwana Wetu Almuqadam* (Walid Alaa Eldin). Uteuzi wa tamthilia teule ulimwezesha mtafiti kukusanya data za kutosha kwa muda mfupi kukamilisha utafiti uliolengwa. Pia, ulimwezesha mtafiti kupata muda wa kutosha kulichunguza jambo lililolengwa kwa kina na kwa mawanda mapana. Maelezo ya kina kuhusiana na usanifu wa utafiti yanapatikana katika kiambatanisho namba 1.



### 3.3 Uteuzi wa Sampuli

Sampuli ni sehemu ya watu au vitu vinavyotarajiwa kumpatia mtafiti data za utafiti ili aweze kutimiza malengo mahsusi ya utafiti anaokusudia. Sampuli katika utafiti huweza kuwa washiriki binafsi, kundi au wote ambao mtafiti huwatumia katika utafiti wake. Mbinu ya uteuzi lengwa inafaa kupata kundi dogo linalotakiwa liwakilishe kundi kubwa ili kupata data za uhakika (Robson, 2007). Tasinifu hii ilitumia mbinu ya uteuzi wa lengwa ili kupata tamthilia teule nne za *Embe Dodo*, *Kaptula la Marx*, *Wananchi Wanapotoroka* na *Bwana Wetu Almuqadam*. Tamthilia hizi zililengwa ili kukidhi malengo mahsusi ya utafiti. Mbinu hii ilikuwa muafaka kwani ilimwezesha mtafiti kupata data za msingi zilizowasilishwa katika utafiti huu.

### 3.4 Vyanzo vya Data

Data za msingi katika utafiti huu zilikusanywa maktabani. Data za msingi hurejelea data zilizokusanywa kwa mara ya kwanza katika utafiti fulani. Pia, ni zile ambazo hazijawahi kukusanywa kwa ajili ya utafiti kama anaofanya mtafiti wakati huo (Kothari, 2004). Kwa hiyo, data za msingi za utafiti huu zilipatikana kutoka katika tamthilia za *Embe Dodo*, *Kaptula la Marx*, *Wananchi Wanapotoroka* na *Bwana Wetu Almuqadam*. Tamthilia zilizolengwa zilimwezesha mtafiti kupata data zilizosaidia kukamilisha malengo mahususi ya utafiti. Mbinu ya usomaji makini wa matini teule ilitumika kupata taarifa zilizolengwa. Mbinu za kimaktaba na kieletroniki zilitumika kupata data za upili kwa ajili ya ufafanuzi data za msingi zilizowasilishwa katika utafiti huu.

### 3.5 Ukusanyaji wa Data

Katika tasinifu hii, mbinu ya usomaji makini ilitumika ili mtafiti kutimiza malengo mahususi ya utafiti. Data za msingi zimekusanywa kwa kutumia mbinu ya usomaji

makini kwa kurejelea tamthilia teule nne. Usomaji makini ni mbinu ya ukusanyaji wa data inayomruhusu mtafiti kupata taarifa zilizolengwa baada ya kusoma matini teule (Talcot, 2010). Mtafiti hupata data zinazohusiana na malengo mahususi ya uchunguzi wake kwa njia ya kusoma matini teule (Babbie, 1999). Mbinu hii ilitumika katika kukusanya data za msingi kwa kuandaa shajara iliyokuwa na mada iliyohusiana na malengo mahususi ya utafiti. Mtafiti alisoma tamthilia teule za *Embe Dodo*, *Kaptula la Marx*, *Wananchi Wanapotoroka* na *Bwana Wetu Almuqadam*, kisha kunukuu yale yote yaliyohusiana na malengo ya utafiti, tayari kufanyiwa uchambuzi na kuandaa ripoti ya utafiti.

### **3.6 Uchambuzi wa Data**

Baada ya kukamilika kwa mchakato wa ukusanyaji wa data, utaratibu wa uchambuzi unapaswa kuandaliwa. Uchambuzi wa data ni kitendo cha kupangilia data kwa namna inayoruhusu data zilizopatikana kujibu maswali ya utafiti (Yin, 1994). Uchambuzi wa data hufanywa kwa kuongozwa na mbinu zinazokubaliwa kwa ajili ya kazi hiyo. Pia, humrahisishia mtafiti kuelewa mantiki ya utafiti unaohusika. Baada ya kukamilika kwa hatua ya ukusanyaji wa data, mtafiti hutakiwa kuzichambua, kuzijadili na kuziwasilisha. Uchambuzi wa data katika utafiti huu ulifanyika kwa kuongozwa na mbinu ya kimaelezo. Mbinu hii hutumika kuchambua data kwa mfumo wa maelezo bila kufuata mbinu ya kitakwimu. Mtafiti alipata fursa ya kuzichunguza tamthilia teule za *Embe Dodo*, *Kaptula la Marx*, *Wananchi Wanapotoroka* na *Bwana Wetu Almuqadam*, kwa kurejelea malengo mahususi ya utafiti. Data zilibainishwa na kuainishwa katika makundi kulingana na malengo mahususi ya utafiti. Mwisho ilikuwa ni kuziwasilisha kwa kuzitolea maelezo.

Katika mbinu hii, mtafiti alizingatia hatua kadhaa. Kwanza, alikusanya data za msingi za utafiti kwa kusoma tamthilia teule. Pili, alizioanisha data zilizokusanywa kulingana na malengo mahususi ya utafiti ili kuona namna zinavyohusiana. Tatu, mtafiti alizipanga kulingana na malengo mahususi ya utafiti ili kukamilisha uchambuzi wa data. Data zote zilipangwa ili uchambuzi uwiane na malengo mahususi ya utafiti. Hatua ya nne ya mwisho, uchambuzi wa malengo mahususi ulizingatia namna yanavyowiana na nadharia zilizotumika katika utafiti uliofanyika.

### **3.7 Usahihi na Kuaminika kwa Data**

Usahihi wa mbinu za ukusanyaji na uchambuzi wa data ni utaratibu unaoweza kupatikana kwa data bora na za kuaminika (Ponera, 2014). Kuaminika kwa data za utafiti hutokana na uwezo wa mbinu za utafiti kutoa matokeo yale yale pindi utafiti unaporudiwa kwa kutumia mbinu zile zile. Mtafiti alitumia mbinu za ukusanyaji na uchambuzi wa data ili kufanikisha upatikanaji wa data bora, halali na za kuaminika. Usahihi na kuaminika kwa mbinu za ukusanyaji na uchambuzi wa data humwezesha mtafiti kupata data bora na za uhakika.

Data za utafiti huu zilikusanywa kwa mbinu ya usomaji na uhakiki wa matini teule. Uchambuzi wa data uliongozwa na nadharia za Usosholojia na Simiotiki. Mbinu ya kimaelezo ilitumika katika uchambuzi wa data zilizowasilishwa. Upungufu wa mbinu moja ulikamilishwa na ubora wa mbinu nyingine (Kombo & Tromp, 2006). Mjadala kuhusu usahihi, uhalali na kuaminika kwa mbinu zilizotumika ulifanyika kati ya mtafiti na wasimamizi wake, pamoja na wanataaluma wa fasihi katika ngazi ya uzamivu. Pia, usahihi wa data ulihakikiwa kwa kutumia mbinu za ukusanyaji, uchambuzi wa data na nadharia zilizoongoza mjadala wa data.

### **3.8 Maadili ya Utafiti**

Utafiti huu utazingatia taratibu na misingi sahihi ya kimaadili wakati wote wa utafiti huu kuanzia hatua ya ukusanyaji data, uchanganuzi wake na uandishi wa ripoti ya utafiti. Maadili ya utafiti huhakikisha usalama wa watafitiwa pamoja na udhibiti wa data zinazokusanywa (Talcot, 2010). Pia, hujumuisha mambo kama kuomba ruhusa ya kukusanya data, idhini ya watafitiwa, udhibiti wa data. Mtafiti alijitahidi kufuata maadili yote ya utafiti kadiri ilivyoweze kama kuchukua barua ya utambulisho kutoka Chuo Kikuu Huria ili kumtambulisha mtafiti katika maeneo yote aliyoenda kukusanya taarifa za utafiti katika maktaba. Mtafiti anatumza haki na maadili ya wataalamu waliomtangulia. Mtafiti alidurusu tasnifu, vitabu, majarida na machapisho mbalimbali yaliyohusiana na utafiti uliosaidia tasnifu hii kwa kuzingatia mwongozo wa udurusu.

### **3.9 Hitimisho**

Vipengele vilivyochunguzwa ni pamoja na usanifu wa utafiti, uteuzi wa sampuli, vyanzo vya data na mbinu za ukusanyaji wa data. Mbinu hizo zilizomwongoza mtafiti katika ukusanyaji, uchambuzi, mjadala wa data zilizowasilishwa na uandishi wa ripoti ya utafiti. Mbinu hizo zilitegemeana na kukamilishana katika ukusanyaji na mjadala wa data uliofanyika katika sura ya nne na tano. Sura ya nne inayofuata inahusu uwasilishaji wa data za utafiti.

**SURA YA NNE**  
**KUBAINISHA DHAMIRA ZILIZOJENGWA KUPITIA TASHITITI KATIKA**  
**TAMTHILIA TEULE**

**4.1 Utangulizi**

Sura hii inahusu mjadala na uwasilishaji wa data. Uwasilishaji wa data ni namna ya kuzipanga data ili ziweze kueleweka vizuri (Kothari, 2004). Katika hatua hii, mtafiti huwasilisha data zilizokusanywa na kufanyiwa uchanganuzi kwa kuzingatia mada kuu ya utafiti. Data zilizopatikana kutoka katika tamthilia teule zimewasilishwa katika sura hii kulingana na mahitaji ya malengo mahususi ya utafiti.

**4.2 Uwasilishaji wa Data**

Uwasilishaji wa data za utafiti katika sura hii umezingatia lengo mahususi la kwanza la tasnifu ambalo lililenga kubainisha dhamira zilizojengwa kupitia tashititi katika tamthilia teule za Tanzania na Misiri. Data zimewasilishwa kutoka tamthilia teule ambapo ndani ya madondoo yaliyodondolewa katika tamthilia teule mtakuwa na tashititi ambazo ndizo ndani yake mmefumbatwa dhamira mbalimbali. Mjadala wa data za utafiti katika lengo mahususi la kwanza la utafiti uliongozwa na nadharia ya Simiotiki na nadharia ya Usosholijia. Dhamira zimewasilishwa kwa utaratibu wa kupewa namba ili kurahisisha urejelezi katika hatua ya mjadala wa data na usomaji. Baadhi ya vifungu vimenukuliwa ili kuthibitisha hoja iliyolengwa katika tasnifu hii. Kimsingi, Senkoro (2006) anaeleza kwamba, vipengele vya kifani na kidhamira katika kazi za fasihi vimefungamana mno na hutegemeana kwa kiwango kikubwa. Wakati mwingine kuvitenganisha kwa ajili ya kiuchambuzi tu, lakini kiuhalisia ni kitu kimoja kilichoshikamana. Hivyo, tashititi ni mbinu ya kisanaa ambayo kutokana nayo ndiyo tunapata dhamira zilizokusudiwa.

**Jedwali Namba 4.1: Orodha ya dhamira zilibainishwa kutokana na matumizi ya tashititi katika tamthilia teule**

		Kaptula la Marx	Embe Dodo	Wananchi Wanapotoroka	Bwana Wetu Al-muqadam
1	Ufisadi	√		√	
2	Udikteta	√			√
3	Ubaguzi na Nafasi ya Mwanamke	√	√		√
4	Uadilifu na Usawa	√			√
5	Haki na Demokrasia	√		√	
6	Elimu		√	√	
7	Malezi ya Watoto na Maadili		√		√

(Chanzo: Mtafiti, 2023)

Jedwali hili limeonesha dhamira ambazo zimejengwa kwa kutumia mbinu ya tashiti katika tamthilia teule. Kwa kuwa lengo kuu la utafiti huu ni kulinganisha na kulinganua dhamira zilizojengwa kwa kutumia mbinu ya tashititi basi jedwali hili linatoa picha kamili ambayo itatusaidia katika kutimiza lengo hilo la utafiti. Uwasilishaji, uchambuzi na mjadala wa data umefanywa katika sehemu inayofuata kwa kupitia dhamira moja baada ya nyingine na namna inavyojengwa kwa kutumia mbinu ya tashititi.

#### **4.2.1 Ufisadi**

Ufisadi ni kitendo cha mtu au kikundi cha watu kujipatia mali kwa njia ambayo si sahihi au kutumia madaraka na mamlaka aliyonayo kujipatia mali ambayo si halali

(Mangare, 2002). Ufisadi ni tatizo linalopaswa kukomeshwa katika jamii. Serikali mbalimbali zimeanzisha vyombo vya kuzuia na kupambana na ufisadi, rushwa na matumizi mabaya ya madaraka. Katika tamthilia ya *Kaptura la Marx*, mwandishi ameeleza dhamira ya ufisadi kupitia tashititi inayosema ‘Mchezo ndani ya mchezo’. Tashititi hii imetumika kuonesha hali ya ufisadi ilivyokithiri hapa nchini. Ufisadi unawatesa wanachi wanyonge kwa kuwa tabaka la juu linahodhi mali za umma kwa njia zisizo halali. Wafungwa wanatumiwa kiishara kuonesha kuwa suala la haki halisimamiwi kwa vitendo katika mahakama zilizopo hapa nchini. Wafungwa wanaeleza:

**Mfungwa 4:** Huyo ndugu anashtakiwa kwa kosa la kuiba mkate kwenye duka la Mhindi.

**Mfungwa 6:** Unakiri kosa?

**Mfungwa 2:** Ndiyo, lakini nilikuwa na njaa.

**Mfungwa 6:** Jela miaka kumi na viboko 25 (uk.24).

Maelezo haya yanaonesha jinsi mahakama inavyoweza kutoa adhabu ambayo hailingani na kosa. Kwa mfano, mtu aliyeshtakiwa kwa kuiba mkate kwenye duka la Mhindi kwa sababu ya njaa, anafungwa miaka kumi na viboko 25. Pia, mfano mwingine unaonesha mshtakiwa aliyeiba pesa za shirika la ndege, kiasi cha shilingi milioni ishirini na moja akafungwa jela kwa muda wa siku moja tu. Wanafungwa wanaeleza:

**Mfungwa1:** Huyo anashtakiwa kwa kosa la kuiba pesa za shirika la ndege, kiasi cha shilingi milioni ishirini na moja!

**Mfungwa 6:** Unakiri kosa!

**Mfungwa 3:** Ndiyo, nakiri.

**Mfungwa 6:** Jela kwa muda wa siku moja! (uk.25).

Katika maelezo haya, maelezo ya kwanza ya mtu aliyeiba mkate kwa sababu ya njaa amehukumiwa kifungo cha miaka kumi na viboko ishirini na vitano. Kwa upande mwingine, mtu aliyeiba fedha za shirika la ndege kiasi cha milioni ishirini, anafungwa jela kwa siku moja tu. Tashititi hii inaonesha kukithiri kwa ufisadi katika jamii. Kwanza, kuna ufisadi wa kuiba mali ya umma ambayo ni fedha ya shirika la ndege, lakini pia kuna ufisadi mwingine wa watoa haki kutotenda haki kwa sababu ya ufisadi wa kupokea rushwa. Kwa kurejelea msimbo wa kimatukio wa nadharia ya Simiotiki tunapata kuiona vizuri tashititi ikijitokeza katika matukio yote mawili lile la kuiba mkate na hili kuiba milioni ishirini pamoja na hukumu iliyotolewa. Hakuna uhalisia katika matukio haya mawili jambo linaloashiria kwamba ufisadi umekithiri katika jamii kwa kiasi kikubwa.

Katika nukuu hizo, kwa mujibu wa nadharia ya Usosholojia, inatufunza kwamba, mara nyingi mtu mnyonge katika jamii ndiye ambaye huonewa na kunyongwa zaidi kuliko yule ambaye ni tajiri. Katika hali ya kawaida, mtu ambaye amekosa chakula na kufikia hatua ya kuiba chakula, alipaswa kutazamwa vizuri na kusaidiwa kuliko kufungwa kifungo cha miaka kumi jela na viboko ishirini na vitano juu. Hapa kuna tashititi nzito ambayo inawataka viongozi na wanajamii kwa jumla kulitazama jambo hili kwa jicho la umakini zaidi ili kuwasaidia wananchi kutatua changamoto zinazowakabili badala ya kuwaongezea matatizo zaidi. Hivyo, katika dondoo tajwa hapo juu, tunaona mahakama ikitajwa kitashititi kushuka kihadhi kwa kutotimiza wajibu wake ipasavyo.

Pia, dhamira ya ufisadi kama tulivyoiona ikijitokeza katika tamthilia ya *Wananchi Wanapotoroka*. Mwandishi ametumia tashititi kujenga dhamira ya ufisadi katika



jamii ambao husababisha wananchi kuishi katika maisha ya dhiki kwa kukosa huduma muhimu na za msingi katika maisha yao ya kila siku. Baadhi ya huduma zinazokosekana katika jamii ni pamoja na elimu bora na tiba sahihi kwa wananchi.

Mwandishi anaeleza:

*امراة: واحنا اللي خرينا الناس تفقد انتمائها لوطنها.  
مواطن: واحنا اللي خرينا العيال تنجح في المدارس وهي ما بتعرف تفك الخط.  
امراة: واحنا اللي خرينا اللي يعيا يموت عشان مش لاقى يتعالج.  
مواطن: واحنا اللي خرينا الشباب عنسوا وضاع عمرهم من غير بيت وونس وعيال.  
امراة: واحنا اللي خرينا المطربين يغنوا للحمير.  
مواطن: واحنا اللي نهينا المليارات وهرينا على بلاد الخواتم. (230)*

**Mwanamke:** Sisi ndio tuliowafanya watu wapoteze uzalendo wa nchi yao.

**Mwananchi:** Sisi ndio tunawaacha watoto kufaulu shuleni; na hawajui jinsi ya kuandika wala kusoma.

**Mwanamke:** Sisi ndio tunaacha yule aliye mgonjwa afe kwa sababu hajapata tiba.

**Mwananchi:** Sisi ndio tuliowafanya vijana wanapoteza maisha yao bila nyumba, mwanamke na watoto.

**Mwanamke:** Sisi ndio tunawaacha waimbaji waimbie kwa ajili ya punda.

**Raia:** Sisi ndio tuliopora mabilioni na kukimbilia nchi ya Kizungu.

Dondoo hili limetumia tashititi na kujenga dhamira juu ya ufisadi unaofanyika nchini na kusababisha wananchi kukosa huduma bora za elimu, afya na makazi bora. Pia imetumika tashihiti wananchi kusema wao ndiyo waliosababisha hali hii, lakini ukweli ni kwamba, viongozi ndiyo hukusanya kodi kwa ajili ya kuhakikisha wananchi wanapata huduma bora katika maisha yao ya kila siku.

Kwa upande mwingine, kama kodi inakusanywa na rasilimali nyingine za taifa nazo pia zinazalisha, lakini hali ya maisha ya watu ipo hivyo ilivyo, basi ni ufiisadi ndiyo sababu kuu ya hali hiyo. Wananchi wanalipa kodi ili walimu walipwe vizuri na wafundishe vizuri, ili miundombinu ya shule iimarishwe vizuri na wanafunzi waweze kumaliza shule wakiwa na elimu na maarifa yaliyokusudiwa. Wanafunzi wanaliza shule na wanafaulu mtihani, lakini hawajui kusoma na kuandika. Hapa, kuna tatizo na tatizo hilo linachangiwa na ufiisadi ambao upo katika jamii. Hali hii haipaswi kufumbiwa macho, vinginevyo hali ya huduma za msingi kwa wananchi zitazidi kuanguka kabisa.

Tashititi nyingine inayojengwa katika dondoo hili kuonesha ufiisadi upo katika jamii ni suala la wagonjwa kutopata huduma bora za afya na kupoteza maisha. Hii ni kazi ya serikali kuhakikisha huduma bora za afya ikiwa ni pamoja na kuwepo kwa wataalamu wa afya wa kutosha; madaktari na wauguzi, vifaa tiba, dawa, maabara za uchunguzi na vipimo na majengo ya kisasa ya kutolea huduma za afya vinapatikana kwa wananchi wote popote walipo mijini na vijijini. Inapotokea serikali inakusanya kodi na kupata fedha nyingi kutoka kwa wananchi masikini, lakini wananchi hawapati huduma bora za afya basi hapo kuna ufiisadi wa fedha za umma kutumiwa kwa faida ya watu wachache waliopo madarakani na washirika wao.

Kimsingi, tunaporejelea mawazo ya nadharia ya Simiotiki kupitia msimbo wa kimatukio, tunaona bayana matukio yanayotajwa kuhusu wanafunzi kumaliza shule na kufaulu, lakini hawajui kusoma na kuandika, wagonjwa kufariki kutokana na kukosa huduma bora, wananchi kukosa makazi mazuri na fedha kwenda kufichwa nje ya nchi na matukio hayo kutajwa kwa namna yalivyotajwa ni ya kimsimbo.

Wananchi hawawezi kufanya hayo, bali viongozi na wote wenye dhamana ndiyo walengwa na kama wameshindwa kutoa huduma bora kwa wananchi, basi kuna mahali fedha zinakokwenda. Mwandishi wa tamthilia ya *Wananchi Wanapotoroka* anapiga vita ufisadi. Anasema:

*بصصان: يا سيدي معاهمش كاش  
مواطن: وماله.. ماهم أكابر.. يخشوا المسارح ببلاش عشان معاهمش كاش.. يركبوا  
الطيارات والقطورات سفلقة عشان معاهمش كاش.. يملوا كروشهم في المطاعم وما  
يدفعوش عشان معاهمش كاش.. ما يدفعوش ضرائب عشان معاهمش كاش.. يا سيدي  
ملعون أبو الكاش.. مش عاوزين كاش.. نديها شيكات.. شيكات حلوة كده على بنوك سويسرا  
وأوربا.. دولار يورو إسترليني بين ماشي. (247)*

**Mwenye macho:** Hawana pesa taslimu.

**Mwananchi:** Ndio, kwa sababu wao ni viongozi... wanaingia ukumbi wa michezo bure kwa sababu hawana pesa taslimu... wanapanda ndege na treni bure kwa sababu hawana pesa taslimu... hujaza matumbo yao katika mikahawa na hawalipi kwa sababu hawana pesa taslimu... hawalipi kodi kwa sababu hawana pesa taslimu. Hatutaki pesa taslimu... Tunataka hundi... hundi ni nzuri, tunataka hundi nzuri kutoka benki za Uswisi na Ulaya... *Yen, sterling, dollars* zote sawa hamna shida.

Ufisadi mwingine unaonekana kuwepo katika jamii ni wa viongozi kupata huduma mbalimbali bila kulipia kwa sababu wao ni viongozi. Haya ni matumizi mabaya ya madaraka na yanapaswa kupigwa vita vikali ili wawe ni mfano bora kwa wananchi wao. Namna ya kukomesha suala hilo ni kuruhusu malipo yasiwe kwa taslimu pekee, bali hata kwa njia ya hundi malipo ya huduma yaweze kufanyika. Inakuwa ni ufisadi uliopitiliza, wananchi wa kawaida wanalipa kodi kila wanapofanya manunuzi, lakini viongozi wenye mishahara na marupurupu makubwa hawalipi kodi kwa sababu wanatumia huduma bila kulipia na hivyo kodi ya serikali hailipwi. Tashititi hii ni

mujarabu sana katika kuhakikisha kila mtu katika jamii anapaswa kulipa kodi kwa ajili ya maendeleo ya wananchi wote.

#### 4.2.2 Udikteta

Udikteta ni hali ya kuwa na utawala katika jamii ambao hautokani na wananchi, bali umejiweka madarakani kwa njia ya mabavu. Utawala wa kidikteta viongozi unakuwa juu ya sheria na wanaweza kufanya jambo lolote kwa mtu yeyote bila kuulizwa na mtu au chombo chochote kati ya vinavyosimamia masuala ya haki katika nchi. Pia, katika utawala wa kidikteta hakuna uchaguzi wa huru na haki na kama ukiitishwa uchaguzi, basi kundi moja litatumia kila hila kuhakikisha wao ndiyo wanaingia madarakani na kundi jingine halipati kitu hata kama ndilo linalopendwa na wananchi.

Vilevile, katika utawala wa kidikteta wananchi wanakuwa hawashirikishwi kwenye masuala ya maamuzi, bali watawala wachache ndiyo huamua kila kitu katika jamii. Matokeo ya utawala wa namna hiyo ni kukosekana kwa haki, usawa na demokrasia katika jamii. Pia, hali kama hiyo huchochea ghasia na mapinduzi ya kijeshi, wananchi ama makundi fulani huamua kupambana ili kusaka haki na usawa katika mataifa yao. Baadhi ya viongozi hupinduliwa na kuishia uhamishoni na wengine kuchukuliwa hatua kali za kisheria na kikatiba. Mwandishi katika tamthilia ya *Bwana Wetu Al-Muqadam* anaeleza:

*المحامي: (وقد أثاره احتمال إفلات الأمر من يده) شعب، والشعب من إمتى يفهم في أمور  
الحكم، الحكم للحكام...  
الأديب: (ساخرًا) دي نظرية جديدة خالص، طب والمحكومين!  
المحامي: عليهم السمع والطاعة.  
الأديب: أمرك غريب، إزاي المحكوم يطيع حاكم لم يشترك في اختياره....*

*المحامي: (ساخرًا بصوت ممطوط) يا سلام، وقفت في زورك دي أوي، وإيه الجديد في ده،  
الحاكم بينطاع لأنه حاكم، لأنه جالس على كرسي الحكم.. (33)*

**Wakili:** Wananchi, tangu lini wananchi wanaelewa mambo ya uongozi, uongozi kwa viongozi.

**Mwanafasihi:** (Kwa kejeli) Hii ni nadharia mpya kabisa na wanaongozwa?

**Wakili:** Lazima wanatii tu.

**Mwanafasihi:** Kivipi, kivipi wanaongozwa wanatii kiongozi hawajamchgua.

**Wakili:** (Kwa kejeli) Ooh, unapinga hiyo, kitu kipya gani sasa, kiongozi anataaiwa kwa sababu yeye ni kiongozi, na anakaa kiti cha uongozi.

Dondoo hili limejengwa kwa tshititi kujaribu kuonesha kwamba wananchi hawapendi kujishughulisha na masuala ya serikali na hata hawajui serikali yao inafanya nini na kwamba siyo kazi yao kujishughulisha na masuala ya serikali. Tashititi hii inaonesha dhamira ya udikteta unavyotawala katika jamii. Jambo la kushangaza kwamba serikali ipo kwa ajili ya kuhudumia wananchi, lakini eti wananchi hawapendi kujishughulisha na masuala ya serikali ambayo ndiyo inawahudumia. Hii ni njia ya waliopo madarakani kutaka kuendelea kutawala bila kufuata katiba na sheria zilizowekwa. Kauli hii kwamba ‘Tangu lini wananchi wakajua masuala ya uongozi, uongozi ni wa viongozi’, inaonesha kukithiri kwa udikteta unaofanywa na viongozi katika jamii. Katika utawala wa kidikteta, kiongozi anaweza kuingia madarakani bila ridhaa ya wananchi na akiwa madarakani anapaswa kuwatumikia wananchi na siyo mwenyewe na watu wachache anaotawala nao.

Katika dondoo hili, kuna maelezo kwamba, ‘Uongozini wa viongozi’, ni tashititi inayoashiria kwamba, katika utawala wa kidikteta huwa hakuna kufanyika uchaguzi.

Viongozi wanajiweka madarakani wenyewe na hutoka madarakani wenyewe wakipenda au wakiondolewa na Mwenyezi Mungu kwa kifo. Maelezo ya nadharia ya Usosholojia yanatufunza kwamba, utawala wa aina unakuwa haufanyi kazi ya kutatua kero na changamoto zinazowasibu wananchi. Wananchi wanahitaji huduma bora za elimu, afya, maji, umeme, makazi na miundombinu bora ya usafrishaji ili maisha yao yaende vizuri. Uongozi unapaswa kujengwa katika misingi imara ya utawala wa sheria na demokrasia kwa manufaa ya wananchi wote.

Daima uongozi upo kwa ajili ya watu na hakuna kiongozi anaweza kuwa madarakani wakati hakuna watu wa kuwaongoza. Ikitokea hivyo, basi hapo hakuna uongozi, bali kuna watu ambao wamejiweka wenyewe kwa maslahi yao na hili halikubaliki katika muktadha wa dunia ya leo. Utawala wa kidikteta mara nyingi hudai kuwa demokrasia haina haja kwani demokrasia haileti maendeleo. Kinacholeta maendeleo ni viongozi makini ambao wanajali maslahi ya wananchi hata kama hawajachaguliwa kidemokrasia. Mwandishi anaeleza:

*الأديب: لكن تسمح لي أقدم رأيي، أظن الديمقراطية تحتم ذلك.  
الرجل: (بدهشة) ديمقراطية!! إزاي يعني؟!  
المحامي: (ساحراً) الديمقراطية حاجة كده زي الفول والطعمية... (34)*

**Mwanafasihi:** Samahani naweza kutoa maoni yangu, nadhani demokrasia inasema hivi.

**Mwanamume:** (Anashangaa) Demokrasia!! Kivipi?

**Wakili:** (Kwa kejeli) Demokrasia ni kitu kama bagia na maharagwe.

Dondoo hapo juu linajenga tashititi ambayo inaonesha kwamba demokrasia ni kitu ambacho hakina faida na maana yoyote katika jamii. Demokrasia inafanishwa na bagia na maharagwe, yaani kitu kidogo tu hakiwezi hata kumshibisha mtu labda ale

bagia nyingi kwa wakati mmoja na kwa wananchi bajia na maharagwe ni chakula ambacho hakina thamani. Tashititi hii inaweza kutazamwa kwa namna mbili. Kwanza, ni kweli zipo jamii ambazo hufanya uchaguzi kila mara, lakini bado hazina maendeleo na watu wake bado ni masikini. Katika muktadha huu inakuwa ni vigumu kusema kwamba demokrasia ni kitu kizuri. Pili, tashititi hii inaweza kutazamwa kama ni msisitizo kwamba demokrasia imefanya kazi nzuri ya kuwaletea maendeleo watu wa mataifa mbalimbali. Kwa hiyo, jambo la busara kila taifa kujenga misingi thabiti ya kudumisha demokrasia.

Kwa maneno mengine, ni sawa na kusema demokrasia inaweza kufanya vizuri katika jamii fulani na isifanye vizuri katika jamii nyingine. Wapo watu wanapenda bagia na wapo ambao hawapendi bajia lakini wanaishi katika mgongo wa ardhi na maisha yao yanakwenda vizuri. Hapa, kuna msimbo wa kiishara na kiurejelezi wa nadharia ya Simiotiki ambapo demokrasia kufananishwa na bagia ni ishara kwamba wapo watu kwao demokrasia ni haina thamani; na ni chungu kutokana na kuwekwa pilipili na haiwasaidii kitu chochote katika maisha yao. Mfumo wowote mzuri katika maisha huwekwa na watu wote katika jamii na wanapoona kuna haja ya kubadilisha mfumo basi wanabadilisha tena kwa umoja wao. Ikiwa mfumo unaotumika katika jamii umewekwa na watu wachache, basi kutakuwa na malalamiko na mfumo huo hautafanya kazi vizuri kama ilivyokusudiwa.

Madaraka ni dhamana wanayopewa baadhi ya wanajamii ili kuongoza wananchi wenzao katika kusimamia serikali na rasilimali za taifa ili ziwanufaishe wananchi wote. Utaratibu wa matumizi ya madaraka umeelezwa na kuanishwa vizuri katika katiba ya nchi, sheria, kanuni, miongozo na taratibu mbalimbali za kuongoza nchi.

Katika nchi yenye kufuata sheria katika kuongoza, haitazamiwi kuona kiongozi au viongozi wakitumia madaraka yao vibaya (Msuya na Lupokela, 2010). Katika jamii kuna viongozi mbalimbali katika serikali kuu, serikali za mitaa, taasisi, mahakama, bunge, mashirika ya umma, wakala wa serikali na mashirika na taasisi zisizo za kiserikali. Mwandishi katika *Kaptura la Marx* anaeleza:

**Mfungwa 1:** ..... Huku nje ni fujo tupu. Hali ni mbaya zaidi kuliko ile tuliyoiacha. Watu wanakula mali ya umma ovyo! Rushwa imeshamiri! Viongozi na wakuu wa nchi wamezungukwa na mawaziri wanafiki na wabunge wenye njaa na uchu wa mali. Kaptula La Marx laveliwa mbwembwe; watu wanateswa na kunyongwa ovyo bila hata kufikisha kortini... sina mengi zaidi. Labda jambo moja. Leo jioni kuna mpira kati ya mawaziri na wabunge. Nitahudhuria (uk. 40).

Dondoo hili linataja baadhi ya viongozi katika jamii ambao ni mawaziri na wabunge ambapo inajengwa tashititi kwamba wameshindwa kutimiza wajibu wao vizuri na kutumia madaraka yao vibaya kwa kutokuishauri na kuisimamia serikali itekeleze wajibu wake. Wanatajwa kuwa ni watu wenye uchu wa njaa na mali jambo linaloashiria kwamba wanatumia vibaya madaraka yao. Badala ya kutumia madaraka waliyopewa na katiba katika kuwatetea wananchi, wao wanatumia madaraka waliyopewa kujinufaisha wao wenyewe. Kwa mujibu wa nadharia ya Usosholojia, inaelezwa kwamba, binadamu mara nyingi ni kiumbe ambaye hujifikiria yeye binafsi kwanza kabla hayamfikiria mtu mwingine. Hata hivyo, unapopewa kazi ya umma ni lazima umma ndiyo uwe kipaumbele kwa sababu viongozi hao wanatumia mali ya umma katika kutekeleza majukumu yao; na pia katika kulipwa mishahara na marupurupu mengine.

Katika dondoo hapo juu, kunajengwa tashititi nyingine kwamba viongozi hao tajwa hawana jambo la msingi ambalo wanaweza kusaidia wananchi kuondokana na adha



na kero mbalimbali ambazo wanakabiliana nazo katika maisha ya kila siku na kucheza mpira ndilo jambo ambalo wanaweza. Hii ni tashititi ambayo inaonesha kwamba, viongozi hawashughuliki na mambo ya msingi ya kuwainua wananchi kiuchumi bali wanashughulika na mambo ambayo si ya msingi. Hivyo, wananchi wanaonekana kukata tamaa na kusema ni bora kwenda kutazama mpira kati ya wabunge na mawaziri badala ya kuwasikiliza wakitoa hoja na kujibu hoja bungeni.

Pamoja na ukweli ambao upo katika tashititi na dhamira iliyowasilishwa, bado ni ukweli pia kwamba wapo wabunge na mawaziri ambao ni wachapakazi sana na wanatendea haki nafasi walizopewa za kuwahudumia na kuwaongoza wananchi. Maendeleo ambayo yamefikwa katika nchi nyingi za Kiafrika. Tanzania ikiwemo ni ishara tosha kwamba nchi hizo zina viongozi makini ambao wanasaidia serikali katika kutimiza wajibu wake vizuri zaidi. Pale viongozi wakuu wa nchi wanapokuwa hawaridhishwi na utendaji kazi wa baadhi ya mawaziri huwatoa katika nafasi zao na kuwateua wengine. Kwa upande wa wabunge, wananchi huacha kuwachagua kwa awamu nyingine baadhi ya wabunge ambao wanaonekana kutotimiza wajibu wao ipasavyo. Mwandishi katika *Kaptula la Marx* ameonesha udhalilishaji wa mawaziri kupitia rais. Maneno yanayofuata yanaashiria kejeli. Anaeleza:

**Rais Kapera:** Una ulimi wa nyoka? Lamba pua yako basi! (Waziri anapiga magoti akiomba radhi). Lamba pua yako! (Waziri anajaribu. Ulimi unakaribia, lakini anashindwa. Udende unamtoka) (uk. 11).

Maneno ya hapo juu yanaonesha hali ya uhusiano mbaya baina ya rais na waziri wake na lugha inayotumika ni ya dharau na inaonesha matumizi mabaya ya madaraka na udufu wa kimawazo wa viongozi walio mamlakani. Katika hali ya kawaida, kiongozi mkubwa anapozungumza na kiongozi wa chini; yaani msaidizi

wake hutumia lugha ya staha na si lugha ya kifedhuli kwa sababu kufanya hivyo ni kutumia vibaya madaraka. Viongozi wa aina hii mara nyingi hufika mahali na kukosa watu wa kufanya nao kazi na hivyo kuchelewesha maendeleo kwa wananchi. Nadharia ya Simiotiki kupitia msimbo wake wa kimatukio, inatueleza hapa kwamba, tukio hili linashusha hadhi ya viongozi wote wawili yaani yule anayetukana na yule anayetukanwa. Mambo kama haya hufanywa na vyombo husika vya kusimamia maadili pale kiongozi anapokosea na siyo kudhalilishwa hadharani kwa kejeli na dharau.

Katika jamii, wapo baadhi ya viongozi ambao hushindwa kutimiza wajibu wao kama viongozi na kuikosesha jamii maendeleo kwa sababu ya matumizi mabaya ya madaraka, lakini katika kujitetea huwasingizia viongozi waliotangulia kabla yao. Mwandishi anaeleza:

**Rais Kapera:** (Kwa masikitiko) Safari yote tuliyofanya, bure! Labda tulishindwa kufika kwa sababu waliotangulia walikuwa wamekwisha-haribu njia! (uk. 37).

Mwandishi ametumia tashititi kuonesha namna viongozi wa aina ya Rais Kapera, wanaposhindwa kuongoza nchi vizuri, huwalaumu viongozi waliowatangulia. Pia, ameonesha kwamba rais Kapera, mawaziri na mkulima wamesafiri ili kutafuta faida kwa nchi yao kupitia kuiga nchi nyingine na mwishowe safari ina madhumuni mema, lakini haina faida yoyote. Matumizi mabaya ya madaraka huwafanya baadhi ya viongozi kuwa na mipango na maamuzi ambayo si mazuri kwa ajili ya maendeleo ya wananchi na badala yake huwa na maamuzi ya kibinafsi ambayo husababisha wananchi kutopata maendeleo. Kitendo cha kiongozi kufanya safari ambazo hazina tija na faida kwa wananchi ni tashititi inayojengwa kuonesha matumizi mabaya ya

madaraka. Kupitia nadharia ya Usosholojia, ushirikishwaji wa viongozi wote pamoja na wananchi katika maamuzi ni njia sahihi ya kufikia maamuzi yenye tija kwa taifa na ndiyo matumizi mazuri ya madaraka ya uongozi.

### 4.2.3 Ubaguzi na Nafasi ya Mwanamke

Dhamira ya ubaguzi husawiriwa kwa namna tofauti tofauti katika kazi za fasihi zilizochunguzwa. Kuna ubaguzi wa rangi, kimadaraka, kitabaka, kidini, kimaeneo, kielimu na kikabila. Kuna watu wanaoabudu ubaguzi kwa kuwadharau watu wengine kwa kuwaona kuwa si lolote wala chochote. Hali hiyo haifai katika ujenzi wa taifa linalohitaji umoja na mshikamano thabiti. Ubaguzi unaweza kuchochea uasi, ghasia na vurugu katika jamii. Baadhi ya wanajamii wanaweza kukosa haki za msingi kutokana na kuimarika kwa ubaguzi. Mwandishi katika tamthilia ya *Kaptura la Marx* anaeleza:

**Rais Kapera:** (Akitingisha kichwa) Kazi nzuri, kazi nzuri! (Kimya).  
Vipi wale panya tuliowaweka huko jela?

**Waziri wa Mambo ya Ndani:** Kwa muda wa miaka tisa iliyopita hatujawaruhusu kutoka nje. Habari nilizo nazo ni kwamba akili zao zinaanza kuwa butu. Hawawezi kufikiri (uk.13).

Matumizi ya ‘panya’ katika dondoo hili ni ya kitashititi iliyotumika kwa lengo la kushusha hadhi ya wafungwa na wapinzani waliopo magerezani ambao wamefungwa kwa amri ya rais aliyepo madarakani. Kiongozi ametumia madaraka yake kuwafunga wapinzani wake na baada ya kuwafunga anawaita ‘panya’. Kuwaita panya ni ubaguzi wa hali ya juu. Tashititi hii inaonesha namna kiongozi alivyolewa madaraka mpaka anawaita wananchi wake kwa jina la ‘panya’. Thamani ya binadamu imeshushwa sana kiasi cha kulinganishwa na panya.

Panya ni mnyama mharibifu wa mazao, nguo na hata kula vifaranga vya kuku jambo linalofanya achukiwe mno katika jamii. Adhabu yake huwa ni kifo pale anapokamatwa au anapobainika kuwepo katika nyumba. Hivyo, kitendo cha kiongozi mkuu, rais Kapera, kuwaita wapinzani wake ‘panya’ ni ishara kwamba yupo tayari kuhakikisha wanakufa kama anavyofanya panya. Mwandishi anaendelea kueleza:

**Mkulima:** (Akinung’unika) Hii njia mnayonipitisha mimi siijui na mimi sijui mnanipeleka wapi!

**Rais Kapera:** Mimi ndiyo dira yenu. Aniaminiye hatapotea.

**Waziri wa Mambo ya Nchi za nje:** Wewe ndiye haki! Wewe pekee ndiye unayeweza kufikiri (uk. 28).

Dondoo hili pia lina matumizi ya tashititi yenye kujenga dhamira ya ubaguzi ambapo mtu mmoja anajiona yeye ni bora kuliko watu wengine katika jamii. Katika hali ya kawaida, kuona kiongozi ambaye anajielezea kuwa yeye ndiyo kila kitu katika maisha ni ubaguzi wa hali ya juu sana. Kiongozi anapaswa kutumia maarifa yaliyopo kwa wananchi wake wote ili kuliletea maendeleo taifa lake.

Kiongozi anajiona yeye ni bora kuliko watu wengine ni kiongozi mbaya ambaye ana damu ya kibaguzi na taifa lake haliwezi kupata maendeleo kwa sababu litakuwa linaendeshwa kwa kutumia mawazo ya mtu mmoja tu. Ukweli ni kwamba, mtu mmoja tu hawezi kufahamu kila kitu, bali hufahamu mambo machache tu na anapounganisha na mawazo na ujuzi wa watu wengine katika jamii hapo ndipo mawazo kuntu hupatikana na utekelezaji wake huzaa maendeleo. Maneno, ‘Mimi ndiyo dira yenu’ na ‘Wewe pekee ndiye haki,’ yametumika kisitiari kama ishara kwamba, rais Kapera, ndiye kiongozi pekee anayejua njia wapasayo kuiendea ili kuufikia usawa, haki na demokrasia nchini.

Pia, kuna ubaguzi kijinsia ambao ni hali ya wanawake kubaguliwa katika mambo mbalimbali ya kijamii, kiuchumi, kiutamaduni na kisiasa kwa madai kuwa wao ni viumbe wa ndani na siyo watu wanaoweza kuwa katika sekta ya umma kama kuwa viongozi nakadhalika (Koda, 2000). Hali hii inatokana na mfumo dume katika maisha ambapo wanaume huonekana kuwa ndiyo viumbe wa umma ambao wanaweza kila kitu na wanawake hawawezi vitu vingi, bali kutoa huduma za nyumbani peke yake (Mwaipopo, 1990).

Dhamira ya ubaguzi wa kijinsia imesawiriwa na waandishi wengi wa kazi za fasihi kwa namna mbalimbali ambapo huoneshwa kwamba ubaguzi wa jinsia huwaathiri wanawake kisaikolojia, kitamaduni na kimaadili. Udhalilishaji unakiuka haki za kibinadamu kwa kuwadhalilisha wanaobaguliwa. Athari hizi huwasukuma kuyakubali mabadiliko mengi katika jamii. Mwandishi wa tamthilia ya *Embe Dodo* ametumia mbinu ya tashititi katika kujenga mahusiano na maingiliano yaliyomo baina ya wanawake na wanaume. Anaeleza:

**Bw. Kifaru:** Wewe ulitaka huyu aende shule kama wewe, hiki chakula angalipika nani (uk. 14)?

Katika dondoo hili hapo juu, tunaona kwamba, baba anamlaumu mtoto wake wa kiume kwa kutaka dada yake aende shuleni na hali ya kuwa baba hakutaka kabisa. Msiamamo wake ni kwamba mtoto wa kike hatakiwi kupata elimu ya shuleni. Kupitia dhamira hii, kunajengwa tashititi ya kuonesha mawazo ya wazazi na mawazo ya vijana yaani watoto wao kuwa ni tofauti. Hii ni ishara ya mabadiliko katika jamii ambapo vijana wa kiume wanaona umuhimu wa watoto wa kike kupata elimu. Jitihada na harakati za kumkomboa mtoto wa kike zinaonekana kuzaa matunda

kwani mawazo ya kumuona mwanamke kama kiumbe wa ndani tu yanabadilika na sasa mwanamke anatazamwa kama kiumbe wa umma kwa maana ya kuweza kupata haki zote za msingi ikiwemo elimu kama anavyopata kijana au mtoto wa kiume.

Kwa kurejelea msimbo wa kimatukio wa nadharia ya Simiotiki, maelezo katika dondoo yanajenga tukio la kumtaka mtoto wa kiume aone kwamba ni sahihi dada yake kutokwenda shule na kukosa elimu kwa sababu asingepata mtu wa kumpikia chakula. Katika hali ya kawaida, mawazo haya hayana mashiko kabisa kwani mtoto wa kiume hawezi kupika chakula? Pia, kuna ubaya gani mtoto wa kike akipata elimu na akafanya kazi ya kupika chakula? Hivi chakula kupikwa na watu ambao hawana elimu ni sahihi? Majibu ya maswali haya tunayaona yakijitokeza katika dondoo hapo juu kupitia tashititi ya kwamba vijana wa kiume wameerevuka sana na kuona ni haki ya wanawake kupata elimu kama wao wanaume wanavyopata elimu.

Kwa nadharia ya Usosholojia, tunaweza kulitazama jambo hili katika muktadha wa mabadiliko katika maisha ambapo siku hizi mume na mke wote wanashirikiana katika kufanya kazi za kuingizia kipato familia zao. Hii ni tofauti na maisha ya jamii za zamani ambapo baba pekee ndiye aliyefanya kazi na kupata kipato cha kuendeshea familia. Kwa muktadha huu, inaonekana bayana kwamba, hivi sasa mahitaji ya familia yameongezeka na yamekuwa makubwa sana kiasi cha mume na mke kushirikiana kwa pamoja katika kufanya kazi na hapo ndipo umuhimu wa kumsomesha mtoto wa kike unajitokeza.

Mtoto wa kike akipata elimu anakuwa kwenye nafasi nzuri ya kupata kazi nzuri ya kumingizia kipato na kumwezesha kusaidiana na mumewe katika kuendesha

familia. Pia, mtoto wa kike anapopata elimu inakuwa rahisi kwake kupata maarifa yatamsaidia hata katika kujiajiri na kuanzisha shughuli mbalimbali za kiuchumi na kuifanya familia kuwa na maendeleo. Dhamira ya ubaguzi wa kijinsia inaelezwa:

**Mwali:** We Mshindi nisaidie basi kuondoa vyombo na kuviosha, mie nimefanya kazi zote hapa nyumbani, we umeenda shuleni na kupitia kucheza tu.

**Mshindi:** (Bila kumwangalia Mwali anaingia ndani mwake) Ndiyo maana mimi nikawa mwanamume na wewe ukawa mwanamke (uk. 15).

Katika dondoo hili tunaona tashititi inayojengwa inaonesha bado wapo baadhi ya vijana au watoto wa kiume wanawaona watoto wa kike kuwa wao ni wa kufanya kazi za nyumbani tu na hawastahili kupata elimu. Hii inatokana na ukweli kwamba, kwa kuwa wapo baadhi ya wazazi ambao wana imani hiyo basi ni dhahiri shahidi kwamba hata baadhi ya watoto wenye imani ya ubaguzi wa kijinsia watakuwepo. Nadharia ya Usosholojia, inaelezwa kwamba, wazazi huwa na nafasi kubwa sana ya kuwajenga watoto wao katika mtazamo fulani wa maisha ambao wao wanauamini kuwa ndiyo sahihi. Kauli kama ‘Ndiyo maana mimi nikawa mwanamme na wewe ukawa mwanamke’, inajenga tashititi kwamba, bado mfumo dume upo katika jamii na kwenye mfumo wa elimu.

Tukitazama majibizano katika dondoo hapo juu kisimiotiki hususani katika msimbo wa kimatukio tunabaini kwamba ipo tashititi inayojengwa ambayo inasisitiza uwepo wa ubaguzi wa kijinsia katika jamii. Kijana wa kiume anakwenda shule na baada ya kutoka shule anapitia katika michezo na anaporudi nyumbani hafanyi kazi yoyote. Kijana wa kike anashinda kutwa nzima akifanya kazi za nyumbani kwa muda mrefu

jambo ambalo ni hatari hata kwa afya yake. Tashititi hii ni halisi na hususani katika maisha ya jamii za vijijini kijana wa kike amekuwa akitumikishwa sana katika kufanya kazi za nyumbani tofauti na wa kiume. Ubaguzi wa namna hiyo unawafanya watoto wa kiume kuona si wajibu wao kufanya kazi za nyumbani na baadae wanapokuwa na familia zao wanaendeleza mfumo dume katika jamii. Elimu zaidi inahitajika kuendelea kutolewa kwani mahali ambapo elimu imefika kwa wingi hasa maeneo ya mijini kumekuwa na mabadiliko makubwa na ubaguzi wa kijinsia umepunguwa sana.

Dhamira ya nafasi ya mwanamke katika jamii imejadiliwa na kuwasilishwa na waandishi wengi wa kazi za fasihi na pia imefanyiwa tahakiki na utafiti maridhawa katika ushairi, tamthilia, riwaya, hadithi fupi na katika fasihi simulizi kwa ujumla wake (Lyatuu, 2011). Nafasi ya mwanamke katika jamii huwasilishwa kwa mbinu mbalimbali na msanii wa tamthilia ya *Embe Dodo* ameisawiri nafasi hiyo ya mwanamke kwa kutumia mbinu ya tashititi kama inavyojitokeza katika dondoo hapa chini:

**Bw. Kifaru:** “We hayawani, mshenzi, naongea na wewe halafu unaninyamazia na kuniangalia kama bundi mtoto? (uk. 7)

...**Bw. Kifaru:** (Akimrushia Bi. Kifaru begi) Haya jaza takataka zako zote humo na uondoke na kichwa chako kabla sijabadili mawazo yangu! (uk. 11)

Katika dondoo hapo juu kunajengwa tashititi kadha wa kadha ambazo zinajenga dhamira ya nafasi ya mwanamke kuwa ni kiumbe duni na dhaifu. Tashititi ya kwanza ni pale ambapo mwanamke anafokewa na mume wake kwa lugha ya dharau na kejeli kama kwamba mwanamke si chochote si lolote yaani hana thamani yoyote katika jamii. Mbaya zaidi analinganishwa na “bundi” ambaye ni ndege mwenye kuhusishwa



na majanga katika jamii pale anapolia usiku jirani na nyumba basi huaminiwa kuna mwanafamilia mmoja atakufa. Tashititi hii inashusha hadhi ya mwanamke katika jamii na kumuona kama ni kiumbe muovu asiyekuwa na mchango wowote katika jamii.

Tashititi ya pili tunaiona pale ambapo mwanamume au mume anapomtaka mwanamke aondoke nyumbani kwa kumtishia kumwandikia talaka. Maelezo haya, “(Akimrushia Bi. Kifaru begi) haya jaza takataka zako zote humo na uondoke na kichwa chako kabla sijabadili mawazo yangu!” yanajenga tashititi kwamba, mwanamke anaweza kufukuzwa na mumewe wakati na muda wowote ambao wanamume atataka kufanya hivyo. Tena anamuonya kwamba ni vema aondoke haraka akiwa hai kwani anaweza kutolewa uhai wake kabla hajaondoka. Kwa mujibu wa nadharia ya Usosholojia, inaelezwa kwamba katika maisha ya jamii ni jambo la kawaida kuona mwanamke amekaa na mumewe kwa miaka mingi na wamefanya kazi ya kujenga familia yao kwa muda mrefu wakiwa pamoja, lakini mwanamke anafukuzwa tu kama mbwa afukuzwavyo. Wapo baadhi ya wanawake katika jamii ambao wamefukuzwa na waume zao na kunyimwa haki zao za msingi ikiwemo mali waliyochuma kwa pamoja na kuwafanya kuishi maisha ya shida na umasikini. Hakika nafasi hii anayopewa mwanamke katika familia na katika jamii si nafasi yake kwa sababu katika familia nyingi mwanamke ndiye mtu ambaye anafanya kazi ya kutunza familia wakiwemo watoto, mume, ndugu wa mume na jamaa wa mume na kubwa zaidi ni kwamba wanawake wengi ni wazalishaji mali kwa kujishughulisha na kilimo, ufugaji, mama lishe na shughuli nyingine ndogondogo za uzalishaji mali katika maeneo ya mijini na vijijini (Mwaipopo, 1990).

Hadhi ya mwanadamu daima huwa ipo juu kutokana na uanadamu wake bila kujali maumbile au jinsi. Hadhi ya mtu hutajwa kuwa imeshuka kutokana na matendo yake ambayo huyafanya na hususani matendo ambayo ni kinyume na maadili ya jamii yake. Pia, hadhi ya mtu hutajwa kuwa imeshuka kutokana tu na jinsi yake na baadhi ya watu huwashusha hadhi wanawake kutokana tu na jinsi yao na siyo sababu nyingine yoyote ya msingi. Katika maisha ya ndoa, mwanamume ndiyo hutazamwa kama kiongozi wa familia na hivyo hadhi yake huwa ni kubwa na hakuna mtu katika familia ambaye anaweza kumsumbua mume. Mke na watoto humpatia baba wa familia hadhi ya hali ya juu kwa sababu yeye ndiyo kichwa cha familia. Tuone namna mwandishi wa tamthilia ya Bwana wetu Al-Muqadam anavyozungumzia suala la hadhi ya mwanamke katika dondoo lifuatalo:

الأديب: (محدثاً نفسه أكثر من مخاطبته للمحامي) الظاهر إنني نمت في المكتب ثاني،  
عدلية المرة دي مش هتعديهالي.

المحامي: عدلية مين يا جدع أنت!! (ص 8)

**Mwanafasihi:** (anajiongea mwenyewe) nadhani nimelala ofisini tena, mke wangu Adlia atanisumbua mara hii.

**Wakili:** Adlia ni nani wewe!

Dondoo hili linajenga tashititi ambayo inaonesha kwamba hadhi ya mwanamke katika ndoa au familia imekuwa kubwa kiasi cha mume kushindwa kurudi nyumbani na kuamua kulala ofisini kwa sababu ya usumbufu wa mke wake. Kwa mujibu wa nadharia ya Sosholojia, wanamume ndiyo ambao imezoeleka kwamba wanatumia mabavu na hata nguvu kufanya maamuzi mbalimbali katika familia na wanawake hutii na kutekeleza. Si jambo la kawaida kwa mwanamke kumthibiti mume wake kiasi hata cha kumfanya mume kushindwa kurudi nyumbani. Hapa tunaona hadhi ya

mwanamke imekuwa sana kwani angeweza kupigwa au kufukuzwa na mume akalala nyumbani na mke akarudi kwao.

Kimsigi, ingawa kinachotajwa na kujadiliwa hapa si kitu kizuri; yaani kumanya mume alale ofisini kwa kuogopa kurudi nyumbani kutokana na usumbufu wa mkewe, lakini ni funzo linatolewa kupitia tashititi kwamba wanawake pia ni watu kama walivyo wanamume na wanaweza kuwa na hadhi kama ya wanamume bila shaka yoyote. Tumeona haya yakitokea katika kipindi hiki ambacho kumekuwa na elimu ya kutosha kuhusu nafasi ya mwanake katika jamii. Jamii ya watu wa Misri wanaongozwa na misingi na mafunzo ya dini ya Kiislamu ambapo mwanamume ndiye kiongozi wa familia. Mke ni kumbe ambaye hapaswi kupaza sauti yake mbele ya mume lakini hapa tumeona ni kinyume chake. Hii ni ishara ya mabadiliko katika jamii. Hata hivyo, mabadiliko hayo hayapaswi kuharibu maisha ya wanandoa bali kuwaweka pamoja na kuwawezesha kuwa na maisha mazuri zaidi na kuishi kwa upendo na umoja. Na mwandishi hapa ametumia tashtiti ili ashushe hadhi ya mwanamke kwamba Maisha yake kama hukumu ya kifo.

الأديب: كانت حياتي معها زي العسكري والحرامي...

المحامي: وطبعًا سيادتك كنت بتلعب دور الحرامي بامتياز..

الأديب: ياريت، الحرامي بيقضي مدته وبعدين يشوف الدنيا، إنما دي كانت حكم بالإعدام، شخصيتها كانت صعبة بشكل غير عادي، وعندها كل القدرة على استخدام كل الأسلحة وفي كل الأوقات. (24: 25)

**Mwanafasihi:** Maisha yangu pamoja nae yalikuwa kama askari na mjambazi.

**Wakili:** Na wewe bila shaka ulikuwa unacheza kama mjambazi kwa uhodari mkubwa.

**Mwanafasihi:** Natamani, mjambazi anapomaliza muda wake gerezani anatoka na anaanza maisha mapya, lakini maisha yangu pamoja nae yalikuwa kama hukumu ya kifo, tabia yake ilikuwa gumu, na ana uwezo wa kutumia aina tofauti ya silaha wakati wowote.

Katika dondoo hili mwandishi kupitia tashititi anaonesha kwamba mwanamke alikuwa katika hadhi ya juu mno kiasi cha kumfanya mumewe amuaone kama ni kiumbe ambaye kuishi naye ilikuwa ni sawasawa na kujitakia kifo. Hapa mwanamke anaogopwa mno na ni kutokana na vitimbi ambavyo anavifanya kuwa ni vikubwa na kumpatia hadhi ya kuogopwa kama vile kifo kinavyoogopwa na watu katika jamii. Hadhi hii aliyonayo mwanamke inajengwa kwa tashititi ya hali hasi lakini inajenga ujumbe kwamba, yale mambo ambayo wanamume hutazamiwa kuyafanya katika ndoa na familia basi wapo baadhi ya wanawake huyafanya.

#### 4.2.4 Uadilifu na Usawa

Uadilifu ni sifa ya kiongozi bora katika jamii na pia ni sifa ya kila mtu mwema katika jamii. Mtu muadilifu anatekeleza wajibu wake kwa kuzingatia misingi ya haki na kwa kufuata kanuni za kazi au maisha ambazo zimeweka katika jamii yake (Haji, 2018). Mwandishi katika tamthilia ya *Bwana wetu Al-Mukadam* amesawiri dhamira ya ukosefu wa uadilifu katika jamii kupitia tashititi mbalimbali. Mwandishi anaeleza:

*المحامي: إيه الرعب ده، هما جيبيني هنا ليه! ومنين! تكونش دي الأخرة! يا نهار زي بعضه، يعني أنا دلوقتي ميت! جالك الموت يا تارك الصلاة... هي الصلاة بس!! إنما أنا مش شايف حاجة، يكونش أنا بس اللي دخلت النار. (ص 7، 8)*

**Wakili:** Oh shida gani hii, mbona wameniletea hapa! Na wameniletea hapa kutoka wapi? **Kumbe** ni akhera! Mungu wangu! Maana mimi sasa hivi nipo maiti! Adhabu imekuja kwa anaecha kuswali... kumbe sio kuswali tu!!! Basi mbona sioni kitu hapa, labda niko peke yangu motoni.

Katika dondoo hili, kunajengwa tashititi inayoonesha namna kukosa uadilifu kunavyoweza kumfanya mtu kupata adhabu katika maisha yake. Wakili ni mtaalamu wa sheria. Kazi yake ni kuwaongoza washtakiwa katika kujitetea kutokana na makosa wanayoshitakiwa. Mwakili huaminika kwamba, hutumia mbinu za kisheria katika kuwatetea wahalifu na wanashinda kesi licha ya kuwa ni kweli wamefanya makosa. Katika dondoo, wakili anasema kwamba, ameingia motoni na alikuwa ni mtu aliyekuwa akisali na kutekeleza ibada kama inavyopasa.

Baadaye, anatoa jibu kuwa motoni kwa kukosa uadilifu katika kazi ya yake ya uwakili. ‘Wakili anasema adhabu imekuja kwa anayeacha kuswali... Kumbe sio kuswali tu!!! Basi mbona sioni kitu hapa, labda niko peke yangu motoni’. Tashititi hii inaonesha kwamba, wakili alikuwa ni mcha Mungu, lakini alikosa uadilifu katika kazi yake. Wakili amejikuta yupo katika adhabu ya moto huko ahera.

Uadilifu ni kitu muhimu sana katika maisha kwani mtu anaweza kuwa mcha Mungu, lakini kitendo cha kukosa uadilifu kinamfanya kuingia katika moto wa jahanam katika maisha ya ahera. Uadilifu ni msingi wa ibada zote ambazo binadamu anazifanya. Kinachoelezwa katika dondoo hapo juu ni kwamba, kutokuwa mwadilifu katika maisha ni kosa kubwa ambalo husababisha mwenye haki kuikosa na asiye na haki kuipata. Katika mafundisho ya dini ya Kiislamu, inaelezwa kwamba, wanamume wameruhusiwa kuoza wake mpaka wanne, lakini ikiwa watashindwa kuwa waadilifu, basi mke mmoja tu anatosha. Hii inaonesha kwamba, uadilifu ni jambo kubwa sana katika maisha na linapaswa kuzingatiwa na kutekelezwa vizuri.

Madhara ya kukosa uadilifu kwenye suala la ndoa tulilotolea mfano ni pamoja na kusambaratika kwa ndoa na familia ambapo watoto hubaki na mzazi mmoja hasa

mama. Hii husababisha watoto kukosa matunzo na malezi stahiki kutoka kwa wazazi wote wawili na katika baadhi ya maeneo watoto hao huweza kuangukia katika kundi la watoto wa mitaani. Uadilifu ni jambo zito, lakini muhimu kwa kila mwanajamii kuhakikisha anazingatia na kuliishi katika maisha yake ya kila siku akiwa hai hapa duniani.

Usawa katika jamii ni miongoni mwa dhamira kongwe ambayo inajitokeza katika kazi nyingi za fasihi andishi na fasihi simulizi (Omary, 2011). Usawa ni suala la haki ambalo limepewa nafasi kubwa katika jamii kupitia katiba za nchi husika pamoja na maazimio mbalimbali ya kitaifa na kimataifa (Shivji, 2002). Katika tamthilia ya *Kaptula la Marx* dhamira ya kukosekana kwa usawa katika jamii ikijitokeza katika tashititi kama ifuatavyo:

**Korchnoni Brown:** Mtakwenda! Halafu mtapinda, mtapinda tena, halafu tena mtapinda. Mwishowe, mtapindapinda hadi mtakapofika mabonde yenye matope. Mtapita katikati ya matope. Halafu milima, halafu misitu yenye miiba hadi mtakapofika jangwani. Kutoka jangwani mtaingia tena bondeni chini kwa chini hadi baharini. Hakuna mitumbwi wala ngalawa. Mtaogelea, ingawa kuna papa wengi. Mkishavuka mtafika nchi itwayo Svoboda. Kabla...(uk.30).

Dondoo hili linaonesha namna ilivyokuwa ni suala gumu kuwa na usawa katika jamii. Kuufikia usawa ni safari ndefu sana ambayo imetawaliwa na kila aina ya dhiki. Ugumu wa safari unaoelezwa hapa ndiyo ugumu wa kufikia usawa katika jamii. Hapa inajengwa tashititi ambayo ndani yake kuna dhamira kuntu lakini kubwa ikiwa ni namna wananchi wanavyoishi katika maisha magumu yasiyokuwa na usawa katika maeneo mbalimbali na hapa eneo linaloonekana bayana ni miundombinu. Katika maeneo ya vijijini, ni jambo la kawaida kuwa na barabara mbovu ambazo hazipitiki katika majira yote na wakati wa masika hali huwa mbaya zaidi. Wakati

hali ikiwa hivyo katika maeneo ya vijijini sehemu kubwa ya maeneo ya mijini hali ya miundombinu huwa si mbaya, bali ni afadhali kidogo. Hapa ndipo usawa unapokesekana katika miundombinu baina ya mijini na vijijini. Tumeona nchini Tanzania, kwa mfano; serikali imefanya jitihada kubwa ya kuhakikisha kunakuwa na usawa katika eneo hilo la miundombinu baina ya mijini na vijijini kwa kuanzisha Wakala wa Ujenzi wa Barabara Mijini na Vijijini (TARURA) na kupangiwa bajeti ya kutosha katika mwaka wa fedha wa 2021/2022 na 2022/2023 (SJMT, 2022).

Pia mwandishi kaonyesha kwamba kwa nchi za Kiafrika ni vigumu kufika katika usawa na uadilifu kupitia mhusika Jitu (Korchnoi Brown) anayewaambia Rais Kapera na Mawaziri kuwa:

**Jitu:** ...sidhani kama mtafikia huko wakati wa uhai wenu. Hata robo tu ya njia bado! (Uk. 29).

Hii ni tashititi ambayo ni mwendelezo wa kile ambacho kimejadiliwa hapo juu, ikiwa na maana kwamba, bila mipango madhubuti haiwezekani jamii kufikia katika usawa wa kweli katika mambo mbalimbali. Tumeona serikali za mataifa mbalimbali ya Kiafrika zikifanya jitihada katika kufikia usawa katika nyanja mbalimbali kama vile elimu, afya, maji, miundombinu, jinsia nakadhalika ambapo sera na mipango ipo na inafanya kazi vizuri. Tashititi hii pamoja na mambo mengine inawakatisha tamaa viongozi na wananchi kwamba siku moja wanaweza kufikia katika usawa wa kweli lakini inavyoonekana ni kwamba hawawezi kufikia katika usawa huo unaokusudiwa. Mara nyingine, kutiana moyo ni njia ya kuhakikisha maendeleo yanapatikana na usawa katika jamii unafikiwa.

#### 4.2.5 Haki na Demokrasia

Demokrasia ni hali ya wananchi kuwa na uhuru wa kuchaguwa viongozi wao kwa njia ya uchaguzi wa huru na haki na kuwapatia mamlaka ya kuongoza serikali (Khalifa, 2013). Kuna demokrasia ya moja kwa moja na ya kuchagua wawakilishi wanaoingia katika vyombo vya maamuzi kwa niaba ya wananchi waliowachagua. Katika tamthilia ya *Kaptula la Marx*, mwandishi ametumia tashititi kuonesha ukosefu wa demokrasia kupitia kupima kiwango cha mwamko wa kisiasa katika jamii kama mwandishi anavyoeleza:

**Rais Kapera:** ... Nina wasiwasi sana na msimamo wa watu waishio katika nchi hii! Watu hawana msimamo! (Akionesha faili lilo mikononi mwa waziri) Waziri wa mambo ya ndani ameniletea ripoti akieleza kuwa mwamko wa kisiasa ni mdogo sana miongoni mwa wananchi. (Akimkazia macho daktari) Daktari! Nataka upime mwamko huu wa kisiasa. Tarishi atakuletea sampuli sasa hivi! (uk. 44).

Dondoo hili lina tashititi ndani yake ambapo katika uhalisia kiongozi huyo anayelitwa kwa jina la rais Kapera ni mtu ambaye hapendi demokrasia, lakini hapa anajifanya kusikitishwa na wananchi wake kutokuwa na mwamko wa kisiasa. Hali hii inaonesha ishara ya kuwepo kwa baadhi ya viongozi katika jamii ambao kazi yao kubwa ni kupinga demokrasia kwa kutokuwapatia wananchi wao uhuru. Viongozi hao hugeuka na kujifanya wao ni wapenda demokrasia. Katika uhalisi, demokrasia hushamiri na kustawi mahali ambapo imewekewa misingi ya kushamiri. Mahali ambapo demokrasia haijapewa nafasi haiwezi kushamiri. Jambo la ajabu kuona kiongozi mkuu anashangaa watu wake kutokuwa na mwamko wa masuala ya siasa na demokrasia. Mwandishi katumia tashititi ili kuonesha kwamba nchi zote za Kiafrika hazina demokrasia. Anaeleza:



**Mfungwa 4:** Mimi nisingejali kutawaliwa na nchi ya jirani. Serikali za Kiafrika ni zile zile za watawala wa maisha (uk.3).

Suala la viongozi kutawala kwa muda mrefu bila kuwapatia wananchi demokrasia ya kuchagua viongozi wanaowapenda kila baada ya muda maalumu ni ishara ya kukosekana kwa demokrasia katika baadhi ya nchi za Afrika. Hapa kunajengwa tashititi ya kwamba, kuna nchi bado viongozi wake hawajakubali kuwa na demokrasia ya kweli ya vitendo bali ya maneno tu. Hata hivyo, kwa sasa zipo nchi nyingi sana za Kiafrika ambazo zimeingia katika mifumo ya kidemokrasia na wananchi wanapata fursa ya kuchagua viongozi wao na pia kila mwananchi mwenye kupenda kugombea nafasi fulani ya uongozi anapata fursa ya kugombea bila kipingamizi.

Unyanyasaji ni hali ya wananchi au mwananchi kufanyiwa vitendo vibaya ambavyo si haki na kupata madhara ya kiafya, kiakili na kisaikilojia. Binadamu anapopata mateso kutokana na unyanyasaji hufika mahali akachoka na kuamua kufanya maamuzi mbayo ni mazuri kwa upande wake ili aondokane na manyanyaso anayofanyiwa. Mwandishi wa tamthilia ya *Wananchi Wanapotoroka* ametumia tashititi kusawiri dhamira hii. Anasema:

جوانيات: اه صحيح.. الميدان قاضي.. فين الشعب؟  
 بروباجندا: إحنأ أعلنأ في كل القنوات عن احتفال النهاردة.  
 بصصان: الشعب اختقى.. هرب.. بح.. فلسع (205)

**Wa ndani:** Ah sawa ... uwanja hauna kitu ... wananchi wako wapi?

**Propaganda:** Tulitangaza sherehe ya leo kwenye vituo vyote vya runinga.

**Mwenye macho:** Wananchi walipotea ... walikimbia, wametoroka.

Wananchi wanapoalikwa kwenye sherehe ya kitaifa huwa na shauku kubwa ya kuhudhuria katika sherehe hiyo na kutamani siku ifike haraka. Katika dondoo hili imekuwa ni tofauti, wananchi wote walioalikwa hawakufika katika uwanja wa sherehe ulioandaliwa. Tashititi imetumika kuashiria kwamba, wananchi wamechoka kutokana na manyanyaso wanayopata kutoka kwa viongozi wao. Kutokana na manyanyaso ya viongozi dhidi ya wananchi, wananchi hawakuhudhuria katika sherehe. Wananchi wamechoshwa na uongozi uliopo na wameamua kutoroka katika nchi yao. Wananchi hao wamekwenda kujipanga vizuri ili kuhakikisha wanawaweka madarakani viongozi ambao watakuwa wema kwa wananchi na wananchi wasikimbie tena nchi yao. Kitendo cha wananchi kuondoka nchini na kutoshiriki katika sherehe bila kusema chochote ni tashititi maalumu kwa viongozi waliopo madarakani kujitathimini na kuacha madaraka kwa watu ambao watachaguliwa na kupewa ridhaa ya kuongoza.

*حرب: والشعب اختفى كله؟*

*بصصان: كله كله*

*جوانيات: إزاي وإمتي؟ إحنا كلنا جينا هنا الصبح.. ملاحظناش حاجة.*

*بصصان: وانتو من إمتي بتلاحظوا.. كل واحد في عربيته.. منزل ستاير على الشبابيك..*

*وحرس قدامه ووراه. (207)*

**Vita:** Na wananchi wote walipotea?

**Mwenyemacho:** Wote wote.

**Wa ndani:** Vipi na lini? Sote tulikuja hapa asubuhi ... hatujaangalia chochote.

**Mwenye macho:** Tangu lini na nyinyi mnaangalia, kila mmoja kwenye gari lake ... anashusha mapazia ya madirisha ya gari ... na walinzi wapo mbele yake na nyuma yake.

Dondoo hili linatoa hakikisho kwamba, wananchi wote wametoroka nchi yao na kuwaacha viongozi bila watu wa kuwaongoza. Tashititi inaonesha kwamba, hata viongozi hao wameshapoteza sifa ya kuwa viongozi. Wananchi wa nchi nzima

wameamua kuondoka katika nchi yao na kwenda kuishi sehemu nyingine, viongozi watawala wa nchi hiyo wanakoma kuwa viongozi. Kiongozi anapata heshima pale anapowaongoza watu. Hali hii inatoa msisitizo kwamba, uongozi ni mali ya jamii na si mali ya kiongozi. Wananchi wanapoamua kuchukua uongozi wao wanaweza kuuchukua wakati wowote, ikiwa ni pamoja na kuamua kutoroka nchi yao na kwenda kuishi katika nchi nyingine. Viongozi wanatakiwa kuhakikisha wananchi wanaishi bila manyanyaso ili kujenga taifa lenye umoja na mshikamano.

Utabaka ni asili ya binadamu ambapo katika maisha kuna matabaka ya watu wa aina mbalimbali na si jambo baya kuwa na matabaka katika jamii au taifa. Kitu kibaya ni tabaka moja kunyonya tabaka jingine au kuwa na tofauti kubwa ya kipato na mali baina ya tabaka moja na jingine. Jamii za Kiafrika ziligawanywa katika matabaka katika kipindi cha ukoloni ambapo kulikuwa na watawala na watawaliwa. Kabla ya ujio wa wakoloni, Afrika hakukuwa na matabaka ya aina hiyo na wanajamii waliishi pamoja kwa kushirikiana katika kila jambo na hata rasilimali za uzalishaji mali zilimikiwa kwa pamoja. Kadri muda ulivyoziidi kusonga mbele, wananchi walichoshwa na watawala wa kikoloni na kudai uhuru kwa hiyo ikawa ni kupigana na tabaka la watawala. Mwandishi wa tamthilia *Wananchi Wanaporotoka* ametumia tashititi kusawiri dhamira hii na hapa chini kuna dondoo linaloshadadia dhamira ya utabaka kama ifuatavyo:

مذيعه: طول عمر الشعب ده نازل حب وتسقيف للحكام عمال على بطل.. عمره ما كره  
حاكم.

مذيع: يا ستي هو يعني من كترهم. (ص 194)

**Mtangazaji wa kike:** *Daima wananchi wanampenda kiongozi na wanamshangilia hata bila sababu za msingi, hawamchukii kiongozi kamwe.*

**Mtangazaji wa kiume:** *Wewe yaani viongozi ni wengi.*

Dondoo hili linajenga tashititi ya dhamira ya utabaka ambapo inaelezwa kwamba wananchi wanampenda kiongozi na wanamshangilia sana na kamwe hawamchukii kiongozi wao. Hii ni tashititi kwani inapokuwa viongozi wamejiweka katika maisha mazuri na kuwaacha wananchi wakiteseka na hali ngumu ya maisha, wananchi watawafurahia vipi viongozi hao? Ikiwa viongozi hawaitishi uchaguzi kwa muda uliopangwa wanakaa madarakani muda mrefu watu watawapenda vipi viongozi hao? Majibu ya maswali haya ni kwamba, wananchi hawawezi kuwapenda viongozi wa namna hii kwani ni watabaka ambao wanajijali wao na kujiona ni bora kuliko wananchi wengine. Kwa kurejelea msimbo wa kimatukio wa nadharia ya Simiotiki, tunapata uelewa kwamba, tukio la viongozi kushangiliwa na kupendwa na watu na hali ya kuwa viongozi hao ni watabaka ni tukio lililoundwa kimsimbo kuonesha namna utabaka baina ya viongozi na wananchi ulivyoshamiri katika jamii.

Vilevile, dondoo hili linajenga tashititi ya kwamba katika tabaka la watawala na watawaliwa huwa kuna kuwa na tabaka la katikati ambalo linanufaika kutokana na uongozi uliopo madarakani. Tabaka hili ndilo ambalo hutumia muda wake katika kuwasifu na kuwashangilia viongozi na katika sherehe huwa wanakaa mbele ili kuwasifu viongozi. Katika mazingira hayo, inaweza kuonekana ni jamii au watu wote katika jamii wanawapenda viongozi ambao wanadumu madarakani milele kumbe ni kikundi kidogo tu cha wanufaika wa uongozi ndicho kinachowashangilia viongozi hao katika mikutano ya hadhara. Hivyo, utabaka katika jamii unaonekana upo na wananchi wanakuwa hawapendi hali ya utabaka wa aina hii ambapo viongozi wachache ndiyo wananufaika na wananchi wengi wanaishi maisha duni.

#### 4.2.6 Elimu

Elimu ni silaha muhimu katika maisha ya binadamu. Jamii ikipokea elimu bora, inaweza kuwa katika nafasi nzuri ya kujikomboa na ndiyo maana serikali mbalimbali duniani zimechukua jukumu la kutoa elimu bure kwa watu wake katika ngazi za elimu ya awali, msingi na sekondari na katika ngazi ya vyuo vikuu kunatolewa mkopo kwa wanafunzi hasa wale wanaotoka katika familia masikini ili waweze kusoma katika ngazi hiyo ya elimu ya juu. Nchini Misri, serikali inatoa elimu bure kwa wanafunzi wote kuanzia ngazi ya shule ya msingi mpaka elimu ya juu pamoja elimu ya ufundi na mafunzo ya amali. Mwandishi wa tamthilia ya *Embe Dodo* ameisawiri dhamira ya elimu kwa kutumia mbinu ya tashititi Anaeleza:

**Bw. Kifaru:** Nitakuvuruga sasa hivi. (Ananyamaza kwa muda) Wao wanataka tuhudhurie vikao kila siku na kupeleka michango isiyokuwa na kikomo, hiyo hela mie nitaitoa wapi?! (Kama anayeongea peke yake) Vilevile, inashangaza, serikali ilitangaza elimu ni bure? Sasa hii michango isiyoisha inakwenda wapi? (uk. 14)

Katika dondoo hili, dhamira ya elimu bila malipo katika jamii ya Watanzania inasisitiza kwamba, elimu bila malipo ipo na inatolewa kwa Watanzania kupitia serikali yao. Mwaka 2021, kwa mfano, nchini Tanzania, kulijengwa madarasa mapya katika nchi nzima bila kuwachangisha wananchi kiasi chochote cha fedha. Pamoja na jitihada hizo za serikali, michango bado ipo. Maelezo haya yamejengwa kitashititi, kwamba, ‘inashangaza, serikali ilitangaza elimu ni bure? Sasa hii michango isiyoisha inakwenda wapi? upo ushahidi tosha kwamba, bado michango katika shule ipo, tena mingi’. Hapa inaelezwa kwamba, michango isiyokwisha, ikiwa na maana kwamba, ni michango mingi; na ni kero kwa wananchi.

Tashititi hii inaweza kutazamwa kwa namna kama tatu hivi; kwanza ni hali ya michango kuendelea kukusanywa na hali ya kuwa serikali ilishafuta michango yote shuleni. Hata hivyo, bado michango hiyo inakusanywa na kuwa ni kero kwa wananchi. Katika muktadha mwingine, zipo taratibu zinapaswa kufuatwa kama uongozi wa shule unaona kuna haja ya kuanzisha mchango fulani kwa ajili ya maendeleo ya shule na ustawi wa wanafunzi. Kwa mfano, suala la wanafunzi kula chakula shuleni limeachwa kuwa ni jukumu la wazazi na uongozi wa shule kuhakikisha wanapata chakula wakiwa shuleni. Pamoja na mambo mengine, wazazi ambao hawana uwezo wa kuchangia chochote hubainishwa na watoto wao hawalazimishwi kuchangia.

Upande mwingine wa pili wa tashititi hii kuhusu dhamira ya elimu bila malipo na suala la kuwepo kwa michango mingi inaweza kuwa ni ukweli kwamba wapo baadhi ya watu wakiwemo viongozi wa shule ambao wanawatoza wananchi michango mingi bila utaratibu na fedha zinazochangwa hazionekani zimetumika kwenye jambo gani la maendeleo ya shule na ustawi wa wanafunzi. Serikali inapokuwa na nia nzuri ya kufanya mambo ambayo yanatija kwa wananchi wake, baadhi ya watu, kwa namna moja au nyingine, watafanya mambo kinyume na utaratibu ili kujinufaisha wao binafsi. Ikiwa watu hao wapo na wanajulikana, basi huripotwa katika mamlaka husika na hatua stahiki za kinidhamu, kimaadili na kisheria huchukuliwa dhidi yao.

Upande wa tatu wa tashititi hii ni kuhusu ukweli kwamba, wajibu wa wazazi kuchangia elimu ya watoto wao. Ushiriki wa kila mzazi katika kuchangia elimu ya mtoto wake ni muhimu sana katika kuhakikisha jamii inaona umuhimu wa elimu katika maisha. Serikali ina majukumu mengi na fedha inazokusanya haziwezi zote

kupelekwa kwenye elimu kwa sababu kuna maji, afya, miundombinu ya barabara, umeme na matumizi mengine. Wananchi wanaposhiriki kuchangia maendeleo ya jamii yao husaidia kuleta maendeleo ya haraka. Pia, jamii huwa ni wamiliki wa maendeleo hayo na huyalinda pale wanapoona miongoni mwao wanaharibu mipango ya maendeleo.

Dhamira ya elimu inajitokeza karibu katika kila tamthilia kwa sababu elimu ni kitu muhimu sana katika maisha ya kila mwanajamii. Elimu inaweza kujenga jamii na kuimarisha uchumi wake, kuwezesha wananchi kuhifadhi mazingira yao na kuyafanya kuwa endelevu. Katika tamthilia ya *Wananchi Wanapotoroka* mwandishi ametumia tashititi kujenga dhamira ya elimu kwa kurejelea elimu ya juu. Mwandishi anaeleza:

*شقرء: مستوى التعليم في بلدكم عارفينه، ما فيش جامعة في بلدكم طلعت في قائمة أفضل  
خمسين جامعة في العالم.*

*بروباجندا: طبعاً... ما ينفعش نبقى من ضمن أحسن خمسين جامعة في العالم... ببساطة  
لإن مستوانا يفوق أحسن خمسين جامعة في العالم.. جامعاتنا أعلى من مستوى كل  
الجامعات في العالم. (279)*

**Mzungu wa Kike:** Tunajua kiwango cha elimu katika nchi yenu. Hakuna chuo kikuu kimoja katika nchi yako ambacho kimeonekana kwenye orodha ya vyuo vikuu bora zaidi ya hamsini ulimwenguni.

**Propaganda:** Kweli ... haitatusaidia kubaki kati ya vyuo vikuu bora vya hamsini ulimwenguni ... kwa sababu tu kiwango chetu kinazidi chuo kikuu bora cha hamsini ulimwenguni ... Vyuo vikuu vyetu ni vya juu kuliko vyuo vikuu vyote duniani.

Dondoo hili tunapolitazama kwa makini tunaona kwamba limejengwa kitashititi kuonesha kwamba elimu bora ni muhimu katika kuwaletea wananchi maendeleo kwa sababu kupitia elimu hiyo wananchi wanakuwa wamepata ujuzi na maarifa faafu na

wezeshi katika maisha yao ya kila siku. Tashititi inakwenda mbali zaidi na kuonesha kwamba, suala si kuwa katika orodha ya vyuo vikuu hamsini bora, bali ni kwamba, elimu inayotolewa inawafaa vipi wananchi katika kusukuma mbele maisha yao na maendeleo ya nchi kwa jumla. Upo uwezekano wa vigezo ambavyo vinatumika kuandaa orodha hiyo ya vyuo vikuu bora ikawa haifungamani na aina ya elimu ambayo inatolewa katika nchi kwa sababu kila nchi ina vipaumbele na malengo yake ya kutoa elimu kwa watu wake. Hivyo, hoja si kuwepo kwenye orodha, bali kuhakikisha elimu inayotolewa inakidhi mahitaji ya wananchi na nchi kwa jumla mara wahitimu hao wanapohitimu.

Maelezo katika dondoo yamejengwa katika msimbo wa kiishara na kiurejelezi wa nadharia ya Simiotiki ambapo mataifa yaliyoendelea huona kwamba, elimu yao ni bora zaidi kuliko elimu ya mataifa mengine. Jambo hili ukilitazama kwa haraka haraka unaweza kufikiri kweli kuwa ni elimu yao ni bora sana na ndiyo maana vyuo vyao vipo katika orodha ya vyuo vikuu bora hamsini. La hasha, si kweli hata kidogo, ukweli ni kwamba, elimu hutolewa kulingana na mahitaji na maendeleo yaliyofikiwa katika nchi fulani. Elimu inayotolewa katika nchi za Kiafrika kupitia vyuo vikuu vyake ni bora na hilo linategemea na mahitaji ya nchi husika. Hata hivyo, changamoto za maendeleo na gunduzi mpya ambazo kwa sasa zinajitokeza zinalazimisha elimu nayo itazamwe kupitia mitaala kuanzia ngazi za chini mpaka elimu ya juu iimarishwe zaidi ili kuendana na mahitaji ya sasa ya maisha katika jamii.



#### 4.2.7 Malezi ya Watoto na Maadili

Ustawi wa jamii yoyote ile duniani hutegemea malezi ya watoto kutoka kwa wazazi wao, shule kwa walimu wao na jamii kwa jumla hususani mafundisho ya dini. Pale inapotokea mtoto amepata malezi mazuri huwa na tabia nzuri ya kufurahiwa na wanajamii wote mahali anapoishi na sifa huwafikia wazazi wake kwa kuwa ndiyo walezi nambari moja (Sengo na Kiango, 2012). Wapo baadhi ya wazazi ambao hukwepa wajibu wao wa malezi kwa watoto wao. Mwandishi wa tamthilia ya *Embe Dodo* kwa kuthibitisha hilo. Anaeleza:

Mimi ni malaika mlinzi wa mti huu hapa. Kuna dodo bivu linalohitaji ulinzi wa mizimu... Sasa hata kama mimi nikienda itasaidia nini? Inabidi ungojee mpaka mama yenu arudi. Undi mtoto? Washenzi wakubwa, ningojeeni hapo hapo niwaonyeshe! Nakwambia lete hapa hiyo nguo, lazima uniambie hili ni gagulo la nani?

Katika dondoo hili, kunajengwa tashititi kadhaa kuhusiana na dhamira ya malezi ya watoto. Tashititi ya kwanza ni ile ambayo inahusu malezi ya mtoto kuwa ni jukumu la wazazi wote wawili. Baba anakwepa wajibu wake na kuwaeleza watoto kwamba, wasubiri mpaka mama yao aje na yeye anaondoka anawaacha peke yao. Tashititi hii inaonesha kwamba, kitendo cha baba kuwaacha watoto peke yao wakati mama hayupo, siyo sahihi na ni kitendo cha wazi ambacho kinaonesha baba akikwepa wajibu wake.

Tashititi ya pili inatoa msisitizo kwamba, katika jamii inaonekana kwamba kazi ya malezi ya watoto ni ya mama peke yake; na baba hausiki hata kidogo na masuala ya malezi ya watoto wake. Dhana hii inatokana na mfumo dume katika jamii. Jukumu la malezi ya watoto huachwa kwa akina mama peke yao. Dhana hii ni potofu kwani malezi ya watoto ni kazi ya wazazi wote wawili pamoja na wanajamii wengine.

Malezi ya watoto ni jambo la ushirikiano baina ya wazazi na watu wengine katika jamii. Wazazi wana nafasi kubwa katika malezi ya watoto wao. Leo katika jamii kuna watoto wa mitaani kutokana na kukosa malezi ya wazazi wawili. Baba au mama aliondoka na kuwaacha watoto hao na mzazi mmoja na mzazi huyo kushindwa kuwalea vizuri na kusababisha watoto hao kuwa watoto wa mitaani. Hivyo, malezi ya watoto ni jukumu la wazazi wote wawili na matokeo ya malezi mazuri ya watoto hutokana na ushirikiano mkubwa baina ya wazazi wote pamoja na wanajamii.

Tashititi ya tatu inayojengwa kuhusiana na dhamira ya malezi ya watoto ni kuhusiana na dhana kwamba mtoto wa kike ndiye ambaye anahitaji uangalizi wa karibu sana kuliko mtoto wa kiume. Tashititi hii tunaipata kutokana na matumizi ya “Embe dodo,” katika dondoo ambapo kwa kutumia msimbo wa kiishara na kiurejelezi tunapata kuelewa kwamba, anayezungumziwa hapo ni binti ambaye ndiyo kwanza amevunja ungo; na hivyo, macho ya vijana yanatua katika embe hilo na kutamani kulila. Watoto wa kike huonekana kuwa katika hatari zaidi kuliko wanaumume kwa sababu wanaweza kupatiwa ujauzito akiwa katika umri mdogo na kusababisha kuharibu maisha yake. Tashititi hii ina ukweli ndani yake, lakini ukweli zaidi ni kwamba watoto wote, yaani wa kike na wa kiume wanahitaji malezi ya karibu kutoka kwa wazazi wao kwa sababu siku hizi hata watoto wa kiume hulawitiwa na kuharibiwa maisha yao. Msisitizo wa malezi ya watoto kuwa ni jukumu si la wazazi peke yao, bali pia ni jukumu la familia. Mwandishi anaeleza:

**Manju:** .... Katu usihofie malezi ya mche dodo wako kwani wewe si mpweke ndugu yangu, jamaa na marafiki zako huwa pale kukusaidia. Aidha, kwa samadi au maji ya kumwagilia mche dodo wakati wa kiangazi. Nao mwembe dodo utakua bila shida yoyote (uk.1).

Katika dondoo hili, mwandishi anajenga tashititi yenye kuonesha umuhimu na nafasi ya familia katika malezi ya watoto. Tukio la kumwagilia mche ili ukuwe kama tukio halisi la malezi ya watoto ambapo mpaka mtoto awe mkubwa hukutana na watu wengi katika familia. Kila mtu ana mchango wake katika malezi ya mtoto husika. Hivyo, wazazi wanapaswa kuwa makini na aina ya wanafamilia ambao wanaishi katika nyumba yao ili kuhakikisha watoto wanapata malezi mazuri kutoka kwa watu wanaowazunguka. Manju anaonesha kwamba, mabinti wanapokua na wanakuwa wasichana watu wananza kuweka matego yao ili kuwaharibu. Wazazi wanapaswa kuwa makini ili kuwalinda mabinti zao. Mwandishi anaeleza:

**Manju:** (Kwa hisia kali) Dodo bivu mtini ni kishawishi kwa inzi, wadudu wengine na hasa kwa binadamu wenye pua zinusazo vyema na macho yaonayo vizuri, tuwe makini sana jamani (uk. 4).

Dondoo hili linajenga tashititi kwamba, binti anapovunja ungo na kuwa msichana baadhi ya watu humtamani kwa lengo la kufanya naye mapenzi. Watu hao wanaitwa wadudu ambao pua zao hunusa na kuipata harufu ya embe dodo kwa uzuri wake na kutamani utamu wake. Katika mazingira kama hayo ni rahisi mtoto wa kike kudanganywa na zawadi ndogondogo na fedha kisha kukubali kufanya mapenzi na watu hao waovu. Katika mazingira mengine, inawezekana binti akabakwa na kufanyiwa vitendo vibaya vya kulawitiwa na hata kusababisha kupoteza maisha yake. Inapasa watoto kupatiwa malezi mazuri ili wasidanganywe na watu waovu. Kuwalinda ni kazi ngumu sana kwa sababu hakuna mzazi anayeweza kuwa na mtoto wake kila wakati. Mwandishi anaeleza:

**Bi. Kifaru:** ..... Kufuga simba ni rahisi sana, lakini siyo binadamu, najua kama embe dodo bivu, kuna watakaokuangalia tu na kumezea mate wakaenda zao, na pia, wapo watakaotaka kutomasa ubivu wa

dodo lenyewe na wapo wale watakaotumia mbinu yoyote ile ilimradi tu waonje dodo (uk. 5).

Hapa, kunajengwa tashititi kwamba, malezi ya watoto ni kitu muhimu sana kwa sababu kupitia malezi bora watajitambua na wanaweza kukwepa vishawishi vya watu waovu. Kutowapatia malezi mazuri kutafanya wazazi kugeuka kuwa walenzi wa watoto muda wote jambo ambalo ni gumu ambapo katika dondoo hapo juu inaelezwa kwamba ni rahisi kumfunga simba, lakini siyo binadamu mwenye akili. Mtoto anapopata malezi mabaya na akaingia katika vishawishi vya watu waovu ni vigumu sana kumlinda kwa sababu tayari atakuwa ameshazoea mambo hayo na atafanya kila mbinu ili kuhakikisha anatimiza alichoshawishiwa. Mwandishi

Anaeleza:

Dodo lenyewe limeumbwa ili liliwe na watu tunasahau hilo; sidhani kama nafsi ya dodo huridhika linapoiva likaachwa tu 38 lianuke na kupasuka lenyewe ndipo liokotwe na kuliwa. Hizi ni zama za mapinduzi. Tabia za kila kitu zimebadilika. Hujasikia kuwa vyura wa Kihansi wanazaa kama watu?

Dondoo hili linajenga tashititi ya kurejelea mawazo ya watu waovu ambao hutaka kuhalalisha uovu wao kwamba wanawake wameumbwa kwa ajili ya wanamume. Utaratibu wa kumpata mweza wa kike upo wazi na siyo kuwatamani watoto wadogo kwa kisingizio kuwa wameumbwa kwa ajili ya wanamume. Tashititi hapa imejengwa kwa kutumia msimbo wa kiishara kwamba embe likiiva ni lazima lililiwe, vinginevyo litaoza au litapasuka. Hivyo, binti anapovunja ungo, lazima atumiwe kimapenzi na wanamume kwani akiachwa hivyo atachujuka na kupoteza uzuri wake.

Mawazo haya siyo sahihi hata kidogo kwani kuoza kwa embe hakuwezi kufananishwa na kuchujuka kwa uzuri wa msichana kwani embe huoza baada ya

muda wa siku chache tu baada ya kuiva, lakini msichana hapotezi uzuri wake kwa muda mfupi baada ya kupevuka. Mwanamke huendelea kuwa mzuri zaidi kadri siku zinavyokwenda kutoka siku alipopevuka. Jamii inapaswa kuhakikisha inatoa malezi mazuri kwa watoto wa kike na wa kiume pia ili kuwa na jamii yenye watu wenye maadili katika vizazi na vizazi.

Wema au kutendeanana wema ni jambo ambalo linafundishwa katika mafundisho ya dini zote na pia katika elimu ya darasani na ile ya jadi watoto na wanajamii kwa jumla hufundishwa kutenda wema kwa wenzao. Fasihi simulizi na baadae fasihi andishi, imekuwa ikifanya kazi ya kufundisha jamii kuwa ya watu wema kwa miaka mingi na mpaka kukawa na aina ya wahusika ambapo ni bapa kwa ajili ya kusisitiza kutenda wema na kuonyesha kwamba wema una nguvu kuliko uovu au ubaya (Mlacha na Madumulla, 1991). Hadithi za kale kuhusu wahusika sungura na fisi zimekuwa zikisimuliwa kwa mkondo huo wa mhusika mmoja kuwa mwema tu na mjanja na mhusika mwingine kuwa si mjanja. Utunzi wa Shaaban Robert katika riwaya zake, nao pia ni wa mkondo huu wa kusisitiza wema dhidi ya uovu (Madumulla, 2009). Katika tamthilia ya *Bwana Wetu Al-Muqadam*; pia kuna matumizi ya tashititi ambayo yanajenga dhamira ya wema katika jamii na hapa tuone mfano wa dondoo lifuatalo:

*المحامي: (مغنيًا) أنا من ضيع في الأوهام ... عمره.  
الأديب: (مدعيًا الإعجاب) .... يا سيدي.  
المحامي: (للرجل) لأ، دي أفهمالك بعدين.  
محامي بس عكسك تمامًا، لأنني طول عمري بأتمنى أكون محامي، وما تتخيلش مدى سعادتني  
لما حققت الحلم ده، صحيح المحاماة مش زي ما كنت متصور (بحسرة): صدق زائد قانون  
يساوي عدل، لأ... دي كانت حاجة تاني خالص، احتيال خداع غش... لازم تكون مقطع  
السمكة... زي ما بيقولوا، يعني بالعربي... لازم تكون إنسان بلا (يعتدل ثم يضع يديه في  
جيبه ويهتز ساخرًا) ... مبادئ. (26)*

**Wakili:** (anaimba) mimi ambae nimepoteza maisha yangu kwa ajili ya nyota.

**Mwanafasihi:** (Anajifanya kafurahi) Ndio.

**Wakili:** (Kwa mwanamume) Hapana, nitakueleweshwa baadaye, mimi ni wakili, basi si kama wewe, nilikuwa natamani kuwa wakili, na nimefurahi sana ninapokuwa wakili, kikweli uwanasheria si kama nilikuwa nadhani (kwa kujota): ukweli Pamoja na sheria inasawezesha uadilifu, hapana sio hivyo ilikuwa kitu kingene, udanganifu, ghushi, lazima unakuwa mjanaja, yaani lazima kuwa binadamu bila (anakaa vizuri na anaiweka mikono yake mfukoni na anasema kwa kejeli) Maadili.

Katika dondoo hili tunaona matumizi ya tashititi kuisitiza kwamba utu wema ni kitu cha msingi sana katika maisha. Wanasheria wanaonekana kukosa utu wema kwa sababu ya kutaka kupata fedha na hivyo kufanya kazi zao bila uadilifu na kuzingatia maadili ambayo ndiyo utu wema wenyewe. Kinachoonekana hapa kwenye dondoo ni kama sifa ambayo wanasheria wanajipatia kwamba wao wanafanya kazi zao kwa ujanja ujanja na kufunja maadili, lakini hii ni tashititi ambayo inakebehi hali hiyo. Kwa mujibu wa nadharia ya Usosholojia inaelezwa kwamba, binadamu ni kiumbe ambaye anatazamiwa kutenda wema kwa sababu amepwa akili ya kutambua jema na baya tofauti na wanyama. Hivyo, ni tunu ya binadamu kutenda wema. Mwanasheria kwa sababu yeye anafanya kazi ya kuhakikisha watu wanapata haki zao, basi anapaswa kufanya wema zaidi. Suala la wanasheria na wanajamii kwa jumla kufanya kazi kwa kughushi, udanganyifu na ujanja ujanja linapaswa kukomeshwa na wema ndiyo utawale katika maisha. Msisitizo wa kutenda wema unatolewa pia katika dondoo lifuatalo:

**المحامي:** يبجي واحد قاتل ويعترف لك بجريمته ويدفع عشان تطلعه براءة، وما أكثر الثغرات في القانون والإجراءات، فهلوي، جريء، تنجح، صاحب مبادئ وقيم... طظ وألف طظ.....

**الأديب:** وايه فايده القانون إذا كان بالشكل ده؟

**المحامي:** القانون متعملش غير عشان كده... القاعدة الشعبية: لا قانون موجود ما لم يُخرق يا سادة.

**الأديب:** بس في حاجة اسمها عدل، رحمة.

**المحامي:** (بثبات ويقين، يمط الكلمة) موجود يا أفندم.... (بسخرية) في الروايات والكتب.

(26:27)

**Wakili:** Muuaji aje kwako anakiri kwamba yeye kau ana analipa kawko ili umetolea kutoka kesi yake ili aachiwe, na mapengo yapo mengi kwenye sheria na ijraati, mjanja na hodari na moyo wake umepiga bonde unafaulu, mweneye maadili na misingi bure hamna kitu.

**Mwanafasihi:** Sasa faida ya sheria ni nini

**Wakili:** Sheria imewekwa kwa ajili ya mambo kama hayo. hamna sheria bila mapungufu.

**Mwanafasihi:** Basi ipo kitu kinaitwa uadilifu, huruma.

**Wakili:** (Kwa makini) Ipoo (kwa kejeli) kwenye vitabu na riwaya.

Maelezo ya hapo juu yanawasilisha mifano ya tashititi ambavyo imetumika katika tamthilia ya *Bwana Wetu Al-Muqadam* ambapo mwandishi ametumia tashititi kujenga dhamira ya kukosekana kwa wema katika jamii na kusababisha wenye haki kudhulumiwa. Tashititi hii inaonyesha kwamba fedha imekuwa ni sababu kubwa ya kupotea kwa utu wa mwanadamu na kugeuka kuwa mnyama. Haki inaonekana bayana, lakini haitolewi kwenye kustahiki, bali inatolewa kwa yule ambaye hastahiki kabisa. Tashititi hii pia inatoa wito kwa jamii kuhakikisha kuwa inawajenga wanafamilia katika misingi ya maadili ili baadaye katika utendaji wao wa kazi wawe ni watu wenye kutenda wema kwa wanadamu wenzao. Nadharia ya Usosholojia inatoa mafunzo na elimu kwa umma kwamba, msingi mzuri wa ustawi wa jamii na taifa lolote unapatikana kutokana na watu wake kuwa wema na kuacha mabaya. Vyombo mbalimbali vya dola, ulinzi na usalama vimewekwa katika jamii kwa ajili

kuhakikisha watu wote wanaishi maisha mazuri ya amani na utulivu na haya yote yanawezakana ikiwa jamii inaishi kwa wema na kila mtu anatekeleza wajibu wake kwa wema.

### **4.3 Hitimisho**

Sura hii imebainisha dhamira zilizojengwa kupitia tashititi kwa kurejelea tamthilia teule. Mjadala wa data ulikijita katika kubainisha na kufafanua namna tashititi zinavyoibua dhamira mbalimbali. Uchunguzi umebaini kuwa dhamira katika tamthilia teule zimejengwa kupitia tashititi. Baadhi ya dhamira zilizopatikana zinahusu kukithiri kwa ufisadi, ubaguzi, suala la elimu, udikteta na kukosekana kwa demokrasia katika jamii. Sura ya tano inayofuata imechunguza namna dhamira zinavyofanana na kutofautiana katika tamthilia teule.



## **SURA YA TANO**

### **KULINGANISHA NA KULINGANUA DHAMIRA ZILIZOIBULIWA KWA KUTUMIA MBINU YA TASHITITI KATIKA TAMTHILIA TEULE**

#### **5.1 Utangulizi**

Sura hii ya tano imewasilisha data zilizokamilisha lengo mahsusi la pili. Lengo hilo lilikusudia kulinganisha na kulinganua dhamira zilizoibuliwa kwa kutumia mbinu ya tashititi katika tamthilia teule. Tashititi ni kipengele muhimu cha kifani kinachotumika kuwasilisha dhamira. Nadharia ya Simiotiki na Fasihi Linganishi zilikuwa muafaka katika uchunguzi wa sura hii. Katika tasnifu hii, kipengele hiki kimetumika kuibua dhamira mbalimbali katika tamthilia teule. Sura hii imewasilisha data kwa kulinganisha na kulinganua dhamira katika tamthilia teule.

#### **5.2 Kulinganisha Dhamira Zilizoibuliwa kwa Kutumia Mbinu ya Tashititi katika Tamthilia Teule**

Kipengele cha kulinganisha dhamira zilizoibuliwa kwa kutumia mbinu ya tashititi katika tamthilia teule kilipaswa kuwasilishwa katika sura hii. Katika sura ya nne, jitihada za kubainisha na kufafanua dhamira katika tamthilia teule. Suala la ulinganisho lilijitokeza katika uwasilishaji wake. Ufanano wa dhamira ulijibainisha wazi katika tamthilia teule licha ya mwachano wa waandishi kijiografia, kihistoria, kiutamaduni na kimazingira. Baadhi ya dhamira zinazofanana zilizopatikana katika vitabu teule zinahusu ufiisadi, ubaguzi, suala la elimu, udikteta na kukosekana kwa haki na demokrasia. Kwa hiyo, kipengele cha ulinganifu wa dhamira hakijawasilishwa katika sura hii kwa kuwa kimewasilishwa katika sura ya nne. Hali hiyo imezingatia ili kuepuka uradidi wa taarifa katika kazi za utafiti.

### 5.3 Kulinganua Dhamira Zilizoibuliwa kwa Kutumia Mbinu ya Tashititi katika Tamthilia Teule

Sura hii imelinganua dhamira zilizowasilishwa katika tamthilia teule nne. Kutofautiana kwa dhamira zilizowasilishwa kunatokana na misingi ya tofauti za maandishi kijiografia, kiutamaduni, kihistoria na kiwakati. Licha ya tofauti hizo, masuala yaliyojitokeza katika vitabu teule ni akisiko la hali halisi iliyopo katika mataifa yaliyochunguzwa. Pamoja na kuwepo kwa mfanano mkubwa wa dhamira katika kazi teule, zipo dhamira chache zilizopatikana. Dhamira hizo zimeibuliwa kwa kutegemea muktadha mpana wa mwandishi uliofumbata harakati zake, falsafa yake, historia yake na hali halisi iliyopo katika taifa lililomkuza na kumlea katika shughuli za uandishi wake.

#### Jedwali Namba 5.1 Orodha ya Dhamira zinazotofautiana katika Tamthilia Teule

		Kaptula la Marx	Embe Dodo	Wananchi Wanapotoroka	Bwana Wetu Al-muqadam
1	Ukoloni Mamboleo	√			
2	Ujamaa na Kujitegemea	√			
3	Ongezeko la Watu			√	
4	Kodi ya Maendeleo			√	
5	Nafasi ya Fasihi katika Jamii				√
6	Huduma za Afya			√	
7	Upendeleo na Urasimio			√	

(Chanzo: Mtafiti, 2023)

Jedwali hili linaonesha dhamira ambazo zinatofautiana katika tamthilia teule kwa kuwekewa alama ya vema. Hii inakuwa ni njia rahisi kwa msomaji kuweza kuona ni dhamira ambazo zinatofautiana katika tamthilia teule. Uwasilishaji, uchambuzi na mjadala wake umefanywa kama ifuatavyo:

### 5.3.1 Ukoloni Mamboleo

Ukoloni mamboleo ni hali ya nchi moja kutawaliwa na nchi nyingine kifikira, kiuchumi na kiutamaduni na kuachiwa kuwa na uhuru wa kisiasa pekee ambao hujulikana kama uhuru wa bendera (Mpangala, 1997). Nchi za Kiafrika zilitawaliwa na mataifa mbalimbali ya Ulaya kuanzia mwaka 1884 baadaye kupatiwa uhuru kuanzia miaka ya 1960 na kuendelea. Uhuru uliotolewa ulikuwa ni wa bendera kwa sababu nchi hizo bado zimeendelea kutawaliwa kupitia Ukoloni mamboleo. Katika tamthilia ya *Kaptura la Marx*, mwandishi ametumia tashititi ili kuonesha Ukoloni mamboleo kupitia ‘Benki ya Dunia’ na kaonesha kwamba Wazungu wanazitumia taasisi hizo ili kuzikandamiza nchi za Kiafrika, kwa kudaiwa na kulimbikiziwa madeni yasiyolipika. Anaeleza:

**Mfungwa 6:** Lo! Si Wazungu hao! Wengi ajabu!

**Mfungwa 1:** Labda Waisraeli!

**Mfungwa 6:** Mmoja wao kama Hitler! Haikosi ni ndugu yake! Wote wameenea mikoba ya fedha! Mikoba yao imeandikwa, “Benki ya Dunia!”

**Mfungwa 2:** Wanaletea fedha au wanakuja kuchukua! Watazameni vizuri. Wameshibashiba kidogo au wana njaa!

**Mfungwa 6:** Matumbo yamevimba, lakini meno yao yako nje kama mbwa vichaa wenye njaa!

**Mfungwa 1:** Basi, hiyo ni shibe ya ugonjwa!

**Mfungwa 6:** Ala! Huko nje naona jela nyingine tena!

**Mfungwa 1:** Kumbe wafungwa tuko wengi ulimwenguni.

**Mfungwa 6:** Tena jela hiyo imeyoandikwa “Soko la Dunia!” (uk. 6:7).

Katika muktadha huu, Wazungu wanaowakilisha ‘Benki ya Dunia’ na ‘Soko la Dunia’ ni ishara ya Ukoloni mamboleo ambao unadhibiti uchumi na biashara ya nchi za Afrika. Nchi hizi zinaingia katika jela ya kudaiwa na kulimbikiziwa madeni yasiyomalizika. Wazungu wanaorejelewa hapa wamevimba matumbo na meno yao yako nje kama mbwa vichaa wenye njaa ili kuashiria tamaa waliyo nayo. Mbwa vichaa wenye njaa ni tashititi kwamba, Wazungu ni wanyonyaji wa nchi za Kiafrika kama vile mbwa kichaa walivyo hatari kwa binadamu.

Kimsingi, kwa kurejelea nadharia ya Simiotiki tunaona tashititi hii inaonesha namna benki ya dunia inavyotumia njia ya kuzikopesha nchi za Kiafrika kwa riba kubwa kiasi cha nchi hizo kulipa fedha nyingi na zenyewe na watu wake kubakia katika lindi la umasikini. Mikopo inayotolewa inalipwa karibu mara mbili ya fedha ya mkopo hali inayozifanya nchi za Kiafrika kuzidisha kukopa na kuzidi kutumia rasilimali za nchi kulipia riba ya mikopo. Soko huria linalotajwa, linatumika kunufaisha zaidi nchi zilizoendelea kuliko nchi masikini kwa sababu hizo ndizo zinazopanga bei ya bidhaa. Nchi za Kiafrika zinaweza kuwa zimezalisha bidhaa kwa gharama kubwa, lakini bidhaa hizo zinapofika kwenye soko la dunia zinapangiwa bei na kuuzwa kwa bei ya chini. Pia, bidhaa za mataifa hayo yaliyoendelea zinanufaika na soko huria kwa sababu wanayo nishati na teknolojia ya kuzalisha bidhaa nyingi kwa gharama nafuu ikilinganishwa na nchi zinazoendelea nyingi zikiwa ni kutoka Afrika. Suala la Ukoloni mamboleo linaendelea kuzitafuna nchi za Kiafrika na kuziacha katika umasikini usiomithilika.

### 5.3.2 Ujamaa na Kujitegemea

Ujamaa ni falsafa ya maisha ambapo jamii huishi pamoja kwa kumiliki kwa usawa njia zote za uzalishaji mali bila ya kuwepo kwa matabaka na unyonyaji baina ya wanajamii (Nyerere, 1967). Nchi ya Tanzania ilikuwa ni kinara kwa nchi nyingi za Afrika ambazo zilitumia falsafa ya Ujamaa na Kujitegemea mara tu baada ya kupata uhuru na falsafa hiyo iliwekewa misingi katika Azimio la Arusha la mwaka 1967. Baadaye, vilianzishwa kwa vijiji vya Ujamaa na Kujitegemea (Omary, 2011). Nchi za Kiafrika zilitekeleza ujamaa kulingana na mazingira ya Kiafrika kama inavyoelezwa katika *Kaptura la Marx*:

**Waziri wa Mambo ya Nchi za Nje:** Jinsi ninavyokutazama! Ho Chi Minh si Ho Chi Minh, Marx si Marx! Na Mao si Mao!

**Rais Kapera:** (Anadakiza)... Hiyo ndiyo siasa ya nchi hii! Siasa ya Ujamaa wa Kiafrika! Hatutangamani na nchi yoyote! Rudieni (Wote wanarudia) “Hiyo...” (uk.36).

Dondoo hii inaonekana bayana kwamba, nchi za Kiafrika zilikuwa na aina ya ujamaa ambayo ulikuwa ni tofauti na ujamaa ulioasisiwa na nchi nyingine zilizozingatia mawazo ya Karl Marx wa nchi za Magharibi. Hapa, pamejengwa tashititi kama mbili hivi. Kwanza, huonesha kwamba, nchi za Kiafrika zilikuwa na haki ya kuwa na ujamaa unaoendana na mazingira yake. Pili, inaonesha kuwa nchi za Kiafrika ziliiga falsafa ya ujamaa kutoka mataifa ya Ulaya na Uchina na mataifa hayo yakashindwa kutekeleza ujamaa kama ilivyokuwa imelengwa na waaanzilishi wa falsafa hiyo. Maelezo kwamba ‘Siasa ya Ujamaa wa Kiafrika! Hatutangamani na nchi yoyote’ ni tashititi inayoonesha kwamba, nchi za Kiafrika zilishindwa kutekeleza falsafa ya Ujamaa na Kujitegemea; na kisha, kutafuta sababu ya kujitetea.

Kwa hakika, tashititi zote mbili zinajenga mantiki kwamba, ni kweli mazingira ndiyo huifanya jamii moja kuchukua jambo fulani kutoka kwa jamii nyingine na kisha kulitengeneza katika muktadha wa jamii husika na kulitekeleza. Hivyo, tashititi hiyo inatoa dhamira kwamba, falsafa ya ujamaa ili iweze kutekelezwa vizuri, ni lazima iwekwe katika misingi na mazingira ya nchi za Kiafrika. Mazingira na utamaduni wa nchi za Kifrika, ni tofauti kabisa na nchi za Ulaya na hivyo kuchukua falsafa ya ujamaa kama inavyotekelezwa katika nchi za Ulaya na kuileta hivyo hivyo katika nchi za Kiafrika isingeliweza kutekelezwa vizuri.

Tashititi ile ya pili ya kwamba, nchi za Kiafrika zimechukua falsafa ya ujamaa na kuiweka katika mazingira yake, lakini bado ilishindwa kutekelezwa vizuri kama ilivyokusudiwa. Pamoja na ukweli kwamba, nchi za Kiafrika zilionekana kutekeleza ujamaa kwa namna yake, lakini haikueleweka vizuri na ndio maana ya maneno “Jinsi ninavyokutazama! Ho Chi Minh si Ho Chi Minh, Marx si Marx! Na Mao si Mao!” Hivyo, pamoja na mambo mazuri ya ujamaa, lakini siasa za Ujamaa zilishindwa nguvu na ubepari na mpaka hivi sasa hakuna nchi ya Kiafrika ambayo inatekeleza siasa hizo.

### **5.3.3 Ongezeko la Watu**

Ongezeko la watu duniani ni agenda katika vikao mbalimbali vya Umoja wa Mataifa pamoja na taasisi na mashirika yake. Pia, ni agenda katika mabunge na seneti za mataifa mbalimbali duniani. Lengo ni kuhakikisha kwamba, ongezeko la idadi ya watu duniani linakwenda sambamba na uhifadhi wa mazingira pamoja pia na kuwepo kwa makazi bora kwa wananchi. Hapana shaka kwamba, idadi ya watu inaongezeka kwa kasi sana na rasilimali zipo pale pale haziongezeki bali zinazidi

kupungua. Mwandishi wa tamthilia ya *Wananchi Wanapotoroka* ametumia tashititi kuwasilisha dhamira hii na ufuatao ni uthibitisho wa hoja hii:

*مذبة: ومعانا الان اعزائي المشاهدين أحد فرسان مرحلة التنمية السيد مأمور التعمير والايواء..*

*ايواء: شوفي يا ابنتي لا ايواء ولا نيلة ده شعب ناقص وعي... أنا أعملهم مساكن أو بيوت... فشر.. دي خيانة عظمي..*

*مذبة: خيانة عظمي؟*

*ايواء: معلوم خيانة عظمي.. أعملهم مساكن علشان يزيديوا. ونأكلهم منين؟ نعالجهم منين؟ أنا من هذا المنبر أطالب بمحاكمة كامامير الإيواء اللي كانوا قبلي.. كل اللي بنوا شقق عرايس وإيواء شباب.. اللي بنوا مساكن شعبية.. لازم يتحاكموا بتهمة الخيانة العظمي (201)*

**Mtangazaji:** Sasa watazamaji tuko pamoja na hodari mmoja wa kipindi cha maendeleo mr. Kamishna wa ujenzi na makazi.

**Mr. makazi:** Sikiliza dadangu, si makazi wala kitu kingine, hawa wananchi hawana elimu... Nawafanya makazi na nyumba... haiwezikani, hii ni uhaini mkubwa.

**Mtangazaji:** Uhaini mkubwa?

**Mr. makazi:** Ndio, uhaini mkubwa... nawafanya makazi ili waweze kuongezeka, na tunawalisha kutoka wapi? Tunawatibu kutoka wapi? Mimi kutoka mimbari hii, nadai kesi ya makamishna wote wa ujenzi na makazi ambao walionitangulia... wale wote waliojenga nyumba za wanandoa na hosteli... lazima wanaenda mahakamani kwa uhaini mkubwa.

Kama tulivyoona hapa juu kwamba, mwandishi katumia tashititi kwa ajili ya kuisitiza kwamba, serikali haijui kutatua matatizo ya nchi na hawajatafuta mapendekeo mazuri kwa ajili ya kuyatatua matatizo ya ongezeko la watu. Hapa, kuna matumizi ya tashititi ambayo yanaitaja serikali kuwa ni kichocheo cha watu kuongezeka katika nchi. Kitendo cha serikali kujenga nyumba na kuwapatia wananchi, inatoa hamasa kwa wananchi kuzaliana kwa wingi zaidi na hivyo idadi ya watu inaongezeka kwa kasi. Serikali haikupaswa kujenga nyumba na kuwapatia wananchi ambao wana nguvu ya kuweza kuzaliana, bali wangepanya hivyo kwa wazee na wastaafu.

Serikali inaweza kuwa na nia nzuri sana ya kuhakikisha wananchi wake wanapata makazi bora, lakini itazame ni watu gani hao ambao wanapewa nyumba za bure ili kuepusha watu kuzaliana kwa wingi wakiamini makazi yapo ya kutosha na kisha kusababisha hali ya ongezeko la watu duniani ikiongezeka. Taifa analotoka mwandishi wa tamthilia ya *Wananchi Wanapotoroka* kuna idadi kubwa ya watu, Hivyo, serikali inapaswa kuendelea kuchukua hatua za makusudi katika kukabiliana na hali hiyo. Kwa mfano, hapa chini kuna mapendekezo ya namna ya kukabiliana na ongezeko la watu, Mwandishi Anaeleza:

*بصصان: وانت مأمور صحة قبلها.. حظيت حبوب منع الحمل في شرايط الأسيرين..  
إيواء: ويأريته حوق.. سنتها زربوا إتناشر مليون عيل. (204)*

**Mwenye macho:** Na wewe pamoja na kamishna wa afya, mmeweka vidonge vya kudhibiti uzazi katika vipande vya aspirini.

**Mr. makazi:** Na haijafanya kazi. Mwaka huo wamezaa watoto milioni kumi na mbili.

Dondoo hili limetoa suluhisho la kukabiliana na tatizo la ongezeko la watu duniani kwa kutumia dawa za uzazi wa mpango. Dawa hizo ziwekwe katikati ya aspirini ili wazazi wanapotumia aspirini, hapo hapo wanapata dawa hiyo ya uzazi wa mpango. Hapa, inajengwa tashititi kwamba, kinachotakiwa ni elimu zaidi itolewe ili wanajamii wafahamu athari za idadi ya watu kuongezeka kwa kasi.

#### 5.3.4 Kodi ya Maendeleo

Serikali yoyote duniani huendeshwa kutokana na kodi ambayo hukusanywa kutoka wananchi kupitia shughuli mbalimbali ambazo wanakuwa wanazifanya katika sekta za ushalishaji kama kilimo, ufugaji, uvuvi, biashara, ajira na utalii. Serikali hutumia



kodi katika kuwaletea wananchi maendeleo katika afya, maji, barabara, umeme, elimu, kuweka ruzuku katika bidhaa na huduma mbalimbali. Bila kodi ya maendeleo, serikali haiwezi kutekeleza wajibu na majukumu yake kikamilifu. Kodi ni msingi wa maendeleo wa taifa lolote. Kila mtu anapaswa kulipa kodi kwa ajili ya maendeleo ya nchi yake. Hata hivyo, kodi inayolipwa haina budi kutumika kwa maslahi mapana ya umma.

Kodi inapozidi ni kero kwa wananchi kwani wanaanza kulalamika na wengi wao kukwepa kulipa. Kanuni ya kodi inaeleza kwamba, kodi ni lazima iwe ya haki, iwekwe kwa mujibu wa sharia, lakini pia iendane na hali halisi ya maisha ya jamii husika. Haiwezekani jamii ina kipato kidogo, lakini kunakuwa na utitiri wa kodi, hiyo si halali na wala siyo haki. Mwandishi wa tamthilia ya *Wananchi Wanapotoroka* ametumia tashititi kusawiri dhamira ya kodi ya maendeleo. Anaeleza:

*كاش: ..... واحد قال لمراته صباح الخير.. ردت عليه قالتله صباح الفل... يدفع ضرائب...  
قلنتيلي ليه؟ حاقولك ليه (وهو بيالغ في إخراج هواء من فمه) ص ب ا ح ا ل خ ي ر خرج  
هواء.. الهواء طالع من البطن.. البطن فيها بلاوي.. قول بصل جبنة قديمة رنجه توم كل دي  
ملوثات للجولازم ننضف الجو عشان نحافظ على البيئة طب نصرف منين؟ من ضريبة تحية  
الصباح.. دي بداية لسه ضريبة سلامو عليكم ضريبة مساء النور ضريبة أهلا وسهلا..  
مذيعه: بس كده ممكن الناس كلها تتغير وتبطل تصبح أو تسلم على بعضا. (200)*

**Taslimu:** Mume akimwambia mke wake habari za asubuhi na yeye kamjibu salama, basi lazima walipe kodi. Niulize kwa nini? Nakujibu (Anaongea na atoe pumzi) H-a-b-a-r-i z-a-a-s-u-b-u-h-I hapa imetoka upepo, upepo umetoka tumboni, kwenye tumbo vipo vitu vingi maharagwe, kitungu maji chese samaki kitungu thaumu, hivyo vyote ni chafu cha hewa. Kwa hiyo, lazima tunasafisha hewa ili tulinde mazingira. Na tunatoa hela ya usafi kutoka wapi? Tunatoa kutoka kodi ya makaribisho ya asubuhi na hiyo ni mwanzo tu. Baadaye tunatoa kodi ya asalamu alikum; kisha habari za jioni na kodi ya shikamoo.

**Mtangazaji:** Basi, watu watabadilika na watasimamisha kupeana salama.

Katika dondoo hii, kunajengwa tashititi kwamba, wananchi wanalipa kodi katika vitu mbalimbali. Kodi ya pumzi iliyotajwa hapa hurejelea utitiri wa kodi ambazo mwananchi anapaswa kulipa. Hata kupeana salamu tu kunapaswa kulipiwa kodi jambo ambalo halikubaliki kabisa kwani hewa ni huduma ya bure ambayo Mwenyezi Mungu ameitoa kwa watu pamoja na viumbe hai vyote. Hewa hailipiwi kodi, bali hewa humfanya binadamu aweze kuishi na anapoishi au kuwa hai ndipo anaweza kufanya kazi na kisha kulipa kodi kutokana na shughuli anazofanya, lakini si kulipia hewa au pumzi. Wananchi wanalalamikia kodi kuwa nyingi kwa kutolea mfano kodi kwa ajili ya kusafisha hewa au kuvuta hewa. Hii inaonesha kwamba, wananchi kutumia sehemu kubwa ya vipato vyao kwa ajili ya kulipoa kodi. Mwandishi anaonesha kwamba, wananchi wanalalamika kodi juu na malipo mengine ambayo hayaeleweki. Anaeleza:

*مواطن: بقول يعني طول عمركم مقالبينا ومفضيين جيوبنا.. ضرائب وتبرعات ودمغات  
وخصومات.. جت الفرصة اللي ناخذ فيها منكم. (244)*

**Mwananchi:** Namaanisha, maisha yenu daima yanatuiba na kumwaga mifuko yetu tupu... tax, michango, stempu na punguzo... basi nafasi yetu imefika kwetu kuchukua kutoka upande wenu. (244).

Dondoo hili limewasilishwa kitashititi ambapo wananchi wanalalamikia wingi wa kodi na kitendo cha kusema ‘Basi nafasi yetu imefika kuchukua kutoka upande wenu’ ni tashititi inayoonesha kwamba, viongozi ndio wananufaika na kodi inayolipwa na wananchi. Wananchi hawalipi kodi kwa ajili ya maendeleo yao, bali wanalipa kwa ajili ya maendeleo ya viongozi na siyo nchi. Hili ni jambo baya na ni kero kubwa kwa wananchi kwa sababu pamoja na kulipa kodi nyingi, bado hawawezi kuwa na huduma nzuri kwa sababu fedha za kodi zinaishia katika mifuko ya viongozi.

### 5.3.5 Nafasi ya Fasihi katika Jamii

Wanafasihi ni watu muhimu katika jamii ambao huyasawiri maisha ya jamii kwa lengo la kutoa elimu na mafunzo kwa wanajamii kupitia uandishi na usimulizi wa kazi za fasihi kama riwaya, tamthilia, hadithi fupi, ushairi na sanaa za maonesho (Senkoro, 1982). Fasihi ni miongoni mwa masomo ambayo yanasomwa katika mtaala wa elimu kuanzia ngazi ya msingi mpaka chuo kikuu katika nchi mbalimbali Tanzania na Misri zikiwa ni sehemu. Tangu kale, fasihi imekuwa ni kioo na chombo cha kufikisha ujumbe na kutoa maarifa kwa jamii (Njogu na Chimerah, 1999). Kabla ya ujio wa mfumo wa elimu ambao unatumika hivi sasa wa wanafunzi kukaa darasani na kupatiwa elimu, mfumo wa zamani ulitumia zaidi fasihi kama chombo kikuu cha kutoa elimu na mafunzo katika jamii. Katika tamthilia ya *Bwana Wetu Al-Muqadam* mwanadishi ametumia tashititi kusawiri dhamira ya nafasi ya fasihi katika jamii kupitia katika dondoo hapa chini:

*الأديب: ما هو النبي آدم كده، ما يآمنش غير باللي يشوفه، وما يشوفش غير اللي هو عايزه، باختصار ما يآمنش غير اللي يوجعه...*

*المحامي: هو ده وقت فلسفة، ناقصينك أنت كمان، هتبقى دنيا وآخره.*

*الأديب: (مستغرفاً) دي مش فلسفة، ده محور الرواية الجديدة اللي بكتبها.*

*المحامي: رواية! هو أنت من إياهم، (ساخرًا) أديب يعني!! عمومًا حضرتك تقصد، اللي كنت بتكتبها- إنما دلوقتي خلاص، بح، لا تكتب ولا تقرأ. ص 10*

**Mwanafasihi:** *Binadamu haamini kitu ila baada ya kukiona kwa macho yake, na haoni ila ambacho anachotaka kukiona, kwa kifupi, haamini ila ambacho kinachomumiza...*

**Wakili:** *Hii ni wakati wa falsafa, inatosha, wewe utakuwa duniani na akhera.*

**Mwanafasihi:** *(Anawaza) Hii sio falsafa, hii ni kiina cha riwaya ambayo naiandika.*

**Wakili:** *Riwaya! Wewe kutoka kwao, (anakejeli) wewe ni mwanafasihi!! Wewe unamaanisha riwaya ambayo ulikuwa unaandika, sasa hivi hamna, wewe huandika wala husomi.*

Katika dondoo hili mwandishi anajenga tashititi ya kuonesha kwamba, katika ulimwengu wa sasa kazi za fasihi hazina mashiko kama ilivyokuwa katika kipindi cha falsafa akiwa na maana ya zamani. Hii ndiyo tashititi ya kwanza ambayo inajengwa na mtunzi, kwamba anakubali na kuthibitisha kwamba kuna kipindi fasihi ilikuwa na nafasi kubwa sana katika kutoa elimu na maarifa kwa jamii na ilipewa heshima kubwa. Tashititi ya pili ni ile ya kuonesha mashaka kwamba, katika kipindi cha siku hizi fasihi inaonekana kukosa mashiko kwa sababu imekuwa zaidi ni biashara na kinachoandikwa au kusimuliwa katika kazi za fasihi ni kile ambacho watu wanapenda kusikia hasa mambo ya starehe za anasa na mapenzi. Masuala dhati hayapewi nafasi kubwa katika ulimwengu wa leo ikilinganishwa na ilivyokuwa katika miaka ya hapo nyuma.

Kimsingi, kwa kurejelea nadharia ya Usosholojia, kinachojengwa katika tashititi tunaweza kukitazama kwa namna mbili ya kwanza ni kweli kwamba wapo baadhi ya waandishi wa siku hizi huandika kazi kwa kufuata mkondo wa soko na hivyo kujikuta wanaandika juu ya maudhui pendwa na siyo masuala dhati. Pia, katika baadhi ya maeneo watu huandika kwa kuogopa mkono wa dola; na hivyo, kutowasilisha mambo kinaganaga. Hali hii ndiyo ambayo inaifanya jamii ione kwamba kazi za fasihi za siku hizi hazina mashiko sana. Hoja hii inaweza kutazamwa kwa namna tofauti pia, kwamba je, huo upendwa ambao unajitokeza kwenye maudhui ya kazi za fasihi, hakuna masuala dhati ndani yake? Inawezekana kabisa riwaya ikawa inazungumzia masuala ya mapenzi, lakini ndani ya mapenzi

kuna masuala dhata ndani yake na ikawa ni sehemu nzuri ya kutoa elimu kwa umma au jamii.

Namna ya pili ambayo tunaweza kulitazama dondoo hapo juu ni ile hali ya baadhi ya watu wa taaluma fulani kudharau taaluma nyingine. Jambo hili lipo katika jamii na tunaona namna lilivyojitokeza katika dondoo ni kwamba wakili anajiona yeye ni bora kuliko mwanafasihi. Katika uhalisia ni kwamba, mwanasheria hawezi kufikia ngazi ya kuwa wakili au msomi wa sheria kama hajasoma fasihi. Kutokana na fasihi, ndipo mwanasheria anajifunza hata namna ya kuandika hukumu yake kuanzia katika kusoma hukumu tangulizi mpaka kuandika hukumu anayotaka kutoa kwa wakati huo ni lazima asome maandiko mbalimbali ya hukumu zilizopita pamoja na vitabu vya sheria kwa ujumla wake. Kwa mujibu wa nadharia ya Usosholojia, hili ni jambo la kawaida ambalo lipo na ni sehemu ya maisha ya watu kujiona wao ni bora kuliko watu wengine.

Kwa njia nyingine, mwandishi hapa chini kajaribu kukaza macho juu ya hali ya wataalamu na wanafasihi, na kaonyesha pia hali ya wananchi kuhusu elimu na hali ya chini ya elimu nchini.

*الأديب: ... على العموم، أنا هبدأ بنفسي، إذا سمحتولي؟ (لا يجد اعتراضًا فيتحرك إلى منتصف الخشبة) أنا ... أديب، وعلى الرغم من كوني با مارس الأدب من سنين طويلة، إلا إنه منتشر ليش ولا عمل واحد، من خمستاشر سنة.*

*المحامي: خمستاشر سنة، أmaal بتاكل منين؟ (21: 22)*

**Mwanafasihi:** *Kwa jumla, mimi nitaanza mimi mwenyewe, mkiniruhusu? (hamna mtu kakataa, kisha ameanza kutembelea jukwaani) mimi Mwanafasihi, na angalau mimi nimeandika vitabu vingi tangu zamani ila hamna kitabu moja kimechapishwa tangu miaka kumi na tano.*

**Wakili:** *Miaka kumi na tano, unapata hela kutoka wapi?*

Dondoo hili linajenga tashititi kwamba kazi za fasihi hazipewi nafasi stahiki katika kuchapishwa na hali ya kuwa waandishi wanajitahidi kutumia muda na gharama kubwa katika kuandaa kazi hizo za kifasihi. Kwa asili, wanafasihi ni watu wanaofanya kazi kwa ridhaa, yaani siyo wafanyabiashara; na hivyo inatazamiwa serikali na wadau wa maendeleo watoe ufadhili wa kuchapisha vitabu vya fasihi ili vitumike katika kutoa elimu na mafunzo kwa wanajamii.

Kwa mtazamo wa pili, tashititi inayojengwa hapa inamkumbusha mwanafasihi kwamba, ulimwengu wa leo siyo ule wa ridhaa, bali fasihi ni kazi kama kazi nyingine za kuingiza kipato. Haya tunayapata pale mhusika wakili anapomuuliza mwanafasihi, “miaka kumi na tano, unapata hela kutoka wapi? Yaani, anamshangaa kwamba, bado mpaka leo mwanafasihi ana mawazo ya kufanya kazi kwa kusubiria ihisani kutoka kwa wafadhili ndiyo asaidiwe kazi yake iweze kuchapishwa. Hivyo, kupitia tashiti hii, wanafasihi wanakumbushwa kuandika kazi zenye ubora wa hali ya juu ili waweze kuchapisha wao wenyewe na wapate soko la kuuza na kupata faida ili waweze kulipia gharama za uchapishaji wao wenyewe na kupata faida ya fedha za kuendeshea maisha.

Mwandishi hapa kubeba ndani yake namna fulani ya kejeli ambayo huweza kusababisha hali furaha anayesoma au anayesikiliza. Mifano mbalimbali imetumiwa na mwandishi ili kufikisha ujumbe kwa njia ya tashititi, lakini lengo la mtunzi si kufurahisha tu.

*الرجل: أبداً والله يا سيادة الشيطان، بس أصلي كنت بالعب مصارعة، وبعدين في الجيش  
ادريت وجسمي شد...  
المحامي: مصارعة، مصارعة ايه؟ تيران لازم...  
الأديب: لازم كان هو التور (بضحكان) ص 19*

**Mwanamume:** *Kamwe Mr. Shetani, nilikuwa nacheza bondia, na baadae kwenye majeshi nimepata mazoezi na mwili wangu umekuwa na nguvu.*

**Wakili:** *Bondia, bondia wa nini? Ng'ombe bila shaka.*

**Mwanafasihi:** *Bila shaka alikuwa yeye ni ng'ombe. (wanacheka)*

Kimsingi, kazi ya fasihi si tu kueleza masuala dhati pekee bali pia na masuala ya burudani. Katika dondoo hapo juu tunaona tashititi ya ucheshi ikijitokeza ili kumfanya msomaji aburudike kidogo huku akiwa anatafakari juu ya masuala au dhamira dhati ambazo ametoka kuzisoma katika kurasa tangulizi za riwaya husika. Hii ndiyo nafasi halisi ya fasihi katika jamii ambapo pamoja na kupata tashititi ambayo imelengwa kwa ajili ya kuwaburudisha wasomaji, lakini ndani yake mna dhamira ambayo mwanadishi anataka hadhira yake ipate. Kwa mfano, katika tashititi hapo juu kuhusu huyo aliyejiita bondia lakini akaambiwa labda yeye ni bondia wa ng'ombe, hapa tunapata ujumbe kwamba, kila kitu katika maisha ili kifanyike vizuri ni lazima kuwe na maandalizi. Maandalizi mazuri ndiyo huwezesha jambo kufanyika vizuri kwa mafanikio.

### **5.3.6 Afya**

Afya bora katika jamii ni msingi wa maendeleo na ndiyo maana serikali nyingi duniani hufanya uwekezaji mkubwa katika masuala ya huduma za afya ili watu wapate huduma bora. Taifa lolote linahitaji watu wachapakazi ili liweze kupata maendeleo na hivyo huduma bora za afya ni kitu muhimu kwa ustawi wa maisha ya wananchi lakini pia kwa maendeleo ya taifa husika. Mwandishi wa tamthilia ya *Wananchi Wanapotoroka* ametumia tashititi katika kujenga dhamira ya huduma bora za afya kupatikana nchini. Anaeleza:

سمراء: أمال ليه نص اللي بيتخرجوا من بلدكم بيقوا رايعين يتعالجوا بره.  
 امرأة: دي بتبقى حالات بسيطة وتافهة.. أنفلونزا مثلا.. برد.. لوز.. كحه.. سخونيه..  
 حاجات هبله. (272)

**Samra:** Kwa nini nusu ya wale wanaotoka nchini kwenu wanaenda nje kwa ajili ya matibabu?

**Mwanamke:** Hizi ni kesi rahisi na ndogo ..., kwa mfano mafua.. baridi. kikohozi .. joto ... maradhi madogo tu.

Katika dondoo hili kunajengwa tashititi ya kutoa msisitizo wa dhamira ya huduma bora za afya kupatikana nchi. Wananchi husafiri kwenda kutibiwa nje ya nchi kwa kutumia gharama kubwa kwa ajili ya matibabu ya maradhi madogo madogo ambayo yanaweza kutibiwa ndani ya nchi. Maradhi kama mafua, joto, baridi na kikohozi ni maradhi madogo sana ambayo huweza kutibiwa nchini kwa sababu haihitajiki uwekezaji mkubwa wa vifaa tiba na wataalamu katika maradhi kama haya. Kukosekana kwa huduma za matibabu za maradhi haya madogo madogo ni tashititi inayoashiria kwamba matibabu ya maradhi makubwa hayapatikani katika nchi. Hivyo, wananchi wengi wanapoteza maisha au wanakwenda nje ya nchi kupata matibabu kwa gharama kubwa.

Suala la matibabu na huduma za afya kwa jumla ni gumu na zito sana kwa nchi nyingi za Afrika. Hii ni kutokana na uwekezaji wake kuwa unahitaji fedha nyingi sana katika maeneo mbalimbali hususani kutoa mafunzo kwa madaktari na wauguzi, kununua vifaa tiba, kujenga miundombinu ya afya, upatikanaji wa dawa na kuwalipa wahudumu wa afya mishahara na stahiki zao zote. Serikali za nchi mbalimbali zinafanya jitihada kubwa katika kuhakikisha huduma za afya zinapatikana kwa wananchi wake kuanzia katika ngazi ya vijiji, kata, tarafa, wilaya, mkoa na hospitali za rufaa.



Ushiriki zaidi wa wananchi pamoja na wadau wa maendeleo na masuala ya afya kwa pamoja unatakiwa ili kuhakikisha wananchi wanapata huduma nzuri bila kusafiri kwenda nchi za nje kutafuta huduma na kujikuta wakitumia gharama nyingi na kubaki katika umasikini. Maradhi yaliyotajwa katika dondoo hapo juu yametajwa kimsimbo wa kitashititi ambao lengo ni kuitaka serikali kufanya kila jitihada kuhakikisha huduma za afya zinaimarika.

Hakika, ni jambo ambalo linawezekana kabisa kuwa na huduma bora za afya kwani maradhi yaliyotajwa katika dondoo hapo juu yanashiria kwamba nchi za Kiafrika zimefanikiwa katika kufanya mambo makubwa mno iweje zishindwe katika kuimarisha huduma za afya? Bila shaka zinaweza kuimarisha huduma hizo na wananchi wakapata huduma wakiwa nchini mwao. Hapa nchini, kwa mfano, huduma za matibabu ya moyo zinatolewa katika nchi yao ambapo kabla wananchi walilazimika kusafiri kwenda katika nchi ya India kwa ajili ya matibabu ya huduma hizo. Hivi sasa, huduma hiyo inapatikana nchini kutokana na uwekezaji ambao umefanywa na serikali.

### **5.3.7 Upendeleo na Urasimu**

Binadamu ni kiumbe ambaye kwa asili ameumbwa kuwa na upendeleo kwanza kwa nafsi yake na pili kwa watu wake wa karibu ikiwa ni pamoja na mke, watoto, ndugu, jamaa na marafiki zake. Watu hawa wa karibu hupata upendeleo kwanza ndipo wanafuatia watu wengine ambao si wa karibu. Hali hii imefanya kuundwa kwa misemo mbalimbali na msemu maarufu ni ule wa “wema huanzia nyumbani,” ikiwa na maana kwamba, mtu anapotaka kutenda wema wowote katika jamii yake, kwanza;

aanzie nyumbani kwa maana ya watu wake wa karibu wawe wa kwanza katika kupata wema huo.

Dhana hii haihusiani na kiongozi aliyeteuliwa au kuchaguliwa na wananchi kuongoza nchi akawa naye anafanya maendeleo kwa upendeleo. Hili halikubaliki kwa sababu yeye ni kiongozi wa watu wote na fedha za serikali ni za watu wote. Ikiwa kiongozi atatumia mali ya umma au mamlaka aliyopewa na umma kufanya upendeleo kwa watu wa familia na marafiki zake hilo ni kosa. Mwandishi wa tamthilia ya *Wananchi Wanapotoroka* ametumia tashititi kusawiri dhamira ya upendeleo katika jamii kama anavyoeleza:

*بصصان: أنا عندي حل مؤقت، كل واحد فيكم يمسك تليفونه، يتصل بولاده وقرابيه بييجوا فوراً، دول يطلعوا كذا ألف.  
ايواء: ما جاييز هربوا همه كمان.  
بصصان: دول مش ممكن يهربوا، أصلهم مش شعب، دول واخدين البلد كلها تملك. (209)*

**Mwenye Macho:** Nina suluhisho la muda, kila mmoja wenu anashikilia simu yake, na anawapiga familia yake awaambie waje mara moja, hao peke yao ni maelfu.

**Mr. Makazi:** Labda hao pia walitoroka.

**Mwenye Macho:** Haiwezikani hao kutoroka, kwa sababu hao sio wananchi, hao ambao wanamiliki.

Data katika dondoo hili imejengwa kitashititi kuonesha kwamba kiongozi au viongozi katika jamii wamekuwa wakifanya upendeleo wa waziwazi kwa watu wao. Baada ya wananchi kutokuja kwenye sherehe kiongozi aliwataka wasaidizi wake wawapigie simu ndugu zao waje na inaonekana kuwa ni wengi wakija watajaza uwanja na sherehe itaendelea. Mtunzi anasema, “Nina suluhisho la muda, kila mmoja wenu anashikilia simu yake, na anawapiga familia yake awaambie waje mara moja, hao peke yao ni maelfu.” Hapa kunajengwa tashititi ya kutoa msisitizo kwamba,

katika jamii kuna watu wengi sana ambao wanapewa upendeleo. Kila kiongozi katika jamii anafanya upendeleo kwa watu wake. Katika msingi huu, itakuwa ni jambo gumu mno kwa wananchi kupata maendeleo ya kweli kwani ni wale wanaopendelewa tu ndiyowatakuwa na maisha mazuri na hawa wengine ambao siyo ndugu na ndiyo wengi nchini wataendelea kuwa masikini.

Katika dondoo hili, imetokea hofu kwa mhusika mmoja kwamba, huenda hata ndugu nao wametoroka na hivyo wakipigiwa simu hawawezi kuja. Haya tunayaona katika maelezo, ‘Labda hao pia walitoroka’, ambapo inatia shaka kwamba, hata ndugu wanaweza kutokukubaliana na dhuluma inayofanywa na viongozi wao. Katika jamii kunaweza kuwa na ndugu ambao hawakubaliani na dhuluma au upendeleo ambao unafanywa viongozi ambao ni ndugu zao. Hili ni tukio la kitashititi la kuonesha kwamba upendeleo si kitu kizuri wakati mwingine kinaweza kikamzindua anayendelewa na kuona anachofanyiwa si sawa na hivyo kugeuka na kumpinga huyo anayemfanyia upendeleo.

Kwa upande mwingine, inaonekana kwamba, wanaopendelewa hawawezi kuwapinga viongozi wanaowapendelea, bali huwapenda na kuhakikisha viongozi hao wanadumu katika madaraka. Hili tunaliona katika data hapo juu kupitia maelezo, “haiwezikani hao kutoroka, kwa sababu hao sio wananchi, hao ambao wanamiliki.” Hapa inajengwa tashititi ya kwamba, watu ambao wanapata upendeleo kutoka kwa viongozi wanakuwa wameshapoteza sifa ya kuwa wananchi na hivyo wao hawana jambo lolote la kulalamika au kuitaka serikali iwafanyie kwa sababu wanafnyywa kila kitu wanachotaka kwa fedha za wananchi wanyonge ambao ndiyo walipa kodi. Watu hao wanakuwa na na mali nyingi katika nchi na hivyo hawawezi kuondoka na

kuacha mali hizo. Hivyo, kitendo cha wao kuonekana kuwa si wananchi ni tashititi ambayo inaonesha umuhimu wa viongozi wa umma kuepuka upendeleo katika jamii kwa sababu upendeleo husababisha watu kugawanyika.

*جوانيات: إنطق أنا مأمور الجوانيات.*

*مواطن: سابقا*

*جوانيات: سابقا؟*

*مواطن: معلوم.. سابقا.. انت كنت مأمور جوانيات.*

*حرب: ايه ده.*

*مواطن: وجنابك ياباشا كمان بقيت عاطل، حضراتكم كلكم دخلتوا سجلات البطالة... الشعب*

*خلاص بئس منكم زهق طق روحه بقت في مناخيره سابها لكم مخضره احكموا بعض كلوا*

*بعض.. اكنتموا على نفس بعض قطعوا بعض. الشعب الغلبان خلع. (219)*

**Wa ndani:** Ongea mimi ni kamishna wa ndani.

**Mwananchi:** Zamani.

**Wa ndani:** Zamani?

**Mwananchi:** Ndio, zamani, wewe ulikuwa kamishna wa ndani.

**Vita:** Kivipi?

**Mwananchi:** Hata wewe umekuwa bila kazi, nyinyi wote wa serikali hamna kazi hamn ajira, wananchi wamekataa tamaa, wamekasirika, kwa hiyo wametoroka, sasa mtawala wenyewe kwa wenyewe, wananchi wametoroka.

Suala la upendeleo katika jamii ni kitu kibaya ambacho kinaweza kusababisha watu wakaikimbia nchi yao. Wananchi wanapoikimbia nchi maana yake viongozi wanakuwa hawana tena uhalali wa kuongoza kwa sababu hakuna watu wa kuwaongoza tena. Kiongozi anajitambulisha kuwa ni kamishna na mambo ya ndani na mwananchi anamwambia kwamba, wewe siyo kiongozi kwa sasa, bali ulikuwa kiongozi zamani. ‘Sasa nchi haina watu wewe siyo kiongozi tena, hivyo unapaswa kujiongoza mwenyewe na familia yako na siyo kuongoza taifa’. Maelezo na fikira

zilizopo kwa wananchi pale ambapo wanakuwa wamechoshwa na suala la upendeleo abalo linafanywa na viongozi wao.

#### **5.4 Hitimisho**

Sura hii imelinganua dhamira zilizowasilishwa katika tamthilia teule nne. Kutofautiana kwa dhamira zilizowasilishwa kunatokana na misingi ya tofauti za waandishi kijiografia, kiutamaduni, kihistoria na kiwakati. Licha ya tofauti hizo, masuala yaliyojitokeza katika vitabu teule ni akisiko la hali halisi iliyopo katika mataifa yaliyochunguzwa. Pamoja na kuwepo kwa mfanano mkubwa wa dhamira katika kazi teule, zipo dhamira chache zilizopatikana. Baadhi yake zinahusu malezi ya watoto, ujamaa na kujitegemea, Ukoloni mamboleo, ongezeko la watu na kodi ya maendeleo. Dhamira hizo zimeibuliwa kwa kutegemea muktadha mpana wa mwandishi uliofumbata harakati zake, falsafa yake, historia yake na hali halisi iliyopo katika taifa lililomkuza na kumlea katika shughuli za uandishi wake. Sura ya sita inayofuata inahusu muhtasari, mapendekezo na hitimisho la utafiti.

## **SURA YA SITA**

### **MUHTASARI, MAPENDEKEZO NA HITIMISHO**

#### **6.1 Utangulizi**

Sura ya mwisho ya utafiti huu inahusu muhtasari wa tasiniifu nzima. Matokeo ya utafiti yameelezwa katika sura hii. Baadhi ya vipengele vilivyoshughulikiwa katika sura hii ni muhtasari wa tasiniifu, matokeo ya utafiti na mapendekezo ya utafiti. Pia, kuna hitimisho la utafiti.

#### **6.2 Muhtasari wa Tasiniifu**

Utafiti huu umechunguza dhamira zilizojengwa kupitia tashititi kwa kurejelea tamthilia teule za nchini Tanzania na Misri. Sura ya kwanza inahusu utangulizi, usuli wa tatizo la utafiti, tatizo la utafiti, malengo ya utafiti na maswali ya utafiti. Pia, kuna umuhimu wa utafiti, mawanda ya utafiti na mpangilio wa tasiniifu nzima. Sura ya pili inahusu mapitio ya kazi tangulizi na mkabala wa kinadharia. Sura ya tatu imewasilisha mbinu za utafiti. Sura ya nne na ya tano zilijikita katika uwasilishaji na mjadala wa data ulioongozwa na nadharia za Simiotiki na Usosholojia na Fasihi Linganishi. Sura ya sita ilihusu muhtasari wa tasiniifu, utoshelevu wa nadharia zilizotumika katika uchambuzi, mjadala na uwasilishaji wa data, matokeo ya utafiti, mapendekezo na hitimisho la utafiti.

#### **6.3 Utoshelevu wa Nadharia**

Nadharia za Usosholojia na Simiotiki zilitumika katika uchambuzi na mjadala wa data zilizowasilishwa. Nadharia ya Semiotiki ilitumika kubaini namna tashititi zilizotumika kuibua dhamira katika tamthilia teule kwa kurejelea lengo mahususi la kwanza. Nadharia ya Usosholojia na nadharia ya Fasihi Linganishi zilikuwa muafaka

katika uchunguzi wa lengo la pili lililolenga kulinganisha na kulinganua dhamira katika tamthilia teule. Dhamira zilichunguzwa kwa kuzingatia hali halisi ya maisha, siasa, uchumi, utamaduni na mazingira ya jamii zinazohusika. Nadharia teule zimefaa katika kuwezesha kukidhi mahitaji ya malengo mahususi ya utafiti huu.

#### **6.4 Muhtasari wa Matokeo ya Utafiti**

Tasinifu hii inahusu kuchunguza dhamira kupitia tashititi kwa kurejelea tamthilia teule za nchini Tanzania na Misri. Tasinifu hii iliongozwa na malengo mahususi mawili kama yalivyobainishwa katika sura ya kwanza. Mjadala wa data zilizowasilishwa uliongozwa na nadharia za Usosholojia na Simiotiki na Fasihi Linganishi. Matokeo ya mjadala wa data za utafiti yameelezwa katika sehemu hii.

Lengo mahususi la kwanza na la pili ya utafiti huu yalihusu kufafanua, kulinganisha na kulinganua dhamira zilizowasilishwa kwa kutumia mbinu ya tashititi katika tamthilia teule. Katika utafiti huu, tashititi zimetumika kama chombo thabiti kilichotumika kuwasilisha dhamira katika tamthilia nne zilizoteuliwa na kuchunguzwa. Pia, zimeonesha kuwepo kwa uhusiano mahususi wa kutegemeana na kukamilishana baina ya kipengele cha tashititi na dhamira. Msuko wa kisanaa ulitumika kuunda tashititi una mchango mkubwa katika kuwasilisha dhamira na kuongeza nguvu na kujenga mvuto wa kifani unaolenga kusisitiza na kuihamasisha jamii kupata udhati wa jambo linaloelezwa.

Dhamira katika tamthilia zilizochunguzwa zinafanana na kutofautiana kutokana na mwachano wa kijiografia na kiutamaduni wa mataifa yaliyolengwa. Baadhi ya dhamira hizo zinahusu ukosefu wa uadilifu na uaminifu, ubaguzi wa kijinsia na hadhi

ya mwanamke, udekteta na ukosefu wa demokrasia, ongezeko la watu, haki za binadamu, ukoloni mamboleo, matumizi mabaya ya madaraka na malezi ya watoto. Dhamira hizo zilizobainishwa zinaonesha hali halisi ya taifa linalohusika kihistoria, kiutamaduni, kisiasa na kiuchumi. Dhamira zimeeleza tajriba za kijamii za kila siku katika maisha halisi. Pia, zimeweza kuyaangazia maisha ya jamii inayohusika katika kipindi maalumu kilichosawiriwa na mwandishi ambaye ni zao hali la taifa lake. Dhamira hizo huakisi mifumo ya maisha ya kila siku katika mataifa yaliyochunguzwa. Hali hiyo inaupa utanzu huo hadhi ya kutazamwa kama kipimo joto cha maendeleo na hali halisi iliyopo katika jamii.

## **6.5 Mapendekezo**

Utafiti huu umeshughulikia kulinganisha na kulinganua dhamira zilizojengwa na matumizi ya tashititi kwenye tamthilia ya Kitanzania na ya Kimisri. Tunapendekeza kufanyika utafiti zaidi wa Fasihi Linganishi baina ya tanzu za kifasihi baina ya fasihi ya Kitanzania na ya Kimisri. Utafiti zaidi unapaswa kufanywa kuhusu namna tashititi zinavyoibua dhamira katika tanzu nyingine za riwaya na ushairi. Uchunguzi unapaswa kufanywa kutumia nadharia mbalimbali ikiwemo ya Uhalisia na Ufeministi.

Pia, tunapendekeza kufanya utafiti linganishi kwa kurejelea kigezo cha uhalisi wa masuala yanayoendelea katika jamii za Kiafrika katika kipindi hiki cha utandawazi. Athari za utandawazi katika nyanja za uchumi, siasa na utamaduni zinahitaji kulinganishwa katika mataifa ya Misri na Tanzania kwa kurejelea kazi za fasihi ya Kiswahili na Kiarabu nchini Misri. Uchunguzi unapaswa kujengwa katika misingi na nadharia ya Uhistoria Mpya na Uhalisia.



## **6.6 Hitimisho**

Sura ya sita ya mwisho imewasilisha matokeo ya utafiti, mapendekezo na hitimisho la utafiti. Sura imeanza na kipengele cha utangulizi kinachoeleza muhtasari wa utafiti uliofanyika. Muhtasari huo umeonesha yale yaliyoshughulikiwa katika kila sura ya utafiti. Utoshelevu wa nadharia zilizotumika katika mjadala wa data umeelezwa, pamoja na matokeo yaliyopatikana kwa kuzingatia malengo mahususi ya utafiti. Pia, katika sura hii tuwasilisha mapendekezo ya utafiti na hitimisho linaloonesha mambo yaliyoshughulikiwa katika sura nzima. Matokeo ya utafiti yameonesha kwamba, licha ya kuwa nchi za Tanzania na Misri zipo mbali kijiografia lakini zipo dhamira ambazo zinafanana katika tamthiliya teule za Kitanzania na Kimisri. Hii ni kutokana na uhusiano wa karibu uliopo baina ya nchi hizo mbili na pia mifumo ya maisha katika jamii hizi mbili ni sababu ya kufanana kwa baadhi ya dhamira. Vile vile matokeo ya utafiti yamebainisha kwamba zipo baadhi ya dhamira ambazo zimetofautiana katika tamthilia teule ambacho ni kitu kilichotazamiwa kwa sababu jamii hizi mbili ni tofauti katika masuala mbalimbali.

### MAREJELEO

- Abourweeshah, A. M. A. (2017). Kuchunguza Matumizi ya Mbinu za Kisanaa na Dhamira katika Tamthilia ya *Morani*. Tasinifu ya Uzamili, Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.
- Ayodi, N. K, na wenzake (2018). Tashititi na Washititi: maana, umuhimu na vipengele vyake. Katika *Mulika Na*. 33:46-57.
- Babbie, E. (1999). *The Basics of Social Research*. Belmont: Wadsworth Publishing Company.
- Bakharessa, S. K. (1996). *Kamusi ya Maana na Matumizi*. Nairobi: Oxford University press.
- Bathes, R. (1994). *The Semiotic Challenge*. Berkely: University of California Press.
- Bertoncini, E. (1989). *Outline of Swahili Literature; Prose, Fiction and Drama*. E.J.Brill.
- Boldor, A. (2003). *Perspective on Comparative Literature*. A Thesis of Master of Arts in The Interdepartmental Program in Comparative Literature, Louisiana State University. USA.
- Chandler, D. (1992). *Semiotics: The Basics*, London: Routledge Press.
- Daniel, Z. L. (2019). Ujitokezaji wa Tashititi katika Fasihi ya Kiswahili: Uchunguzi wa Kazi Teule. Tasinifu ya Shahada ya Uzamivu ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

- Didas, M. (2019). Usawiri wa Mwanamke katika Tamthilia ya Kimfumojike: Mifano kutoka *Mama Mtakatifu na Kivuli kinaishi*. Tasinifu ya Uzamili ya Chuo Kikuu cha Nairobi.
- Fadhili, I. (2014). Dhima ya Mtindo katika Tamthilia za Kihistoria: Utafiti Linganishi wa tamthilia ya *Morani na Kinjekitile*, Tasinifu ya Shahada ya uzamili. Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.
- Fakih, S. J. (2017). Kutathmini Mabadiliko ya Usawiri wa Mwanamke katika Riwaya ya *Utengano na Kamwe Si Mbali Tena*: Utafiti Linganishi. Tasnifu ya Shahada ya Uzamili Kiswahili; Chuo Kikuu Huria ca Tanzania (Haijachapishwa)
- Gwanko, L. C. (2017). Kutathimini mbinu za ufutuhi katika kuelimisha jamii kuhusu janga la Ukimwi katika tamtiliya ya *Embe Dodo na Ushuhuda wa Mifupa*. Tasinifu ya Shahada ya Uzamili, Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.
- Haji, M. I. (2018). Uhalisia wa utabaka katika tamthilia za Janga la Werevu na *Kitumbua Kimeingia Mchanga*, Tasinifu ya Shahada ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Taifa Zanzibar.
- Highet, G. (1962). *The Anatomy of Satire*. Princeton: Princeton University Press.
- Hussein, E. (1983). *Hatua Mbalimbali za Kubuni na Kutunga tamthilia Kufuatana na Misingi ya Ki – Aristotle*”. Katika Makala za Semina ya Kimataifa ya Waandishi wa Kiswahili. Dar es Salaam. TUKI. Kur. 197– 205.
- Ismail, H. H. (2019). Kuchunguza Mtindo katika tamthilia ya Mondlane na Samora. Tasinifu ya Shahada ya Uzamili ya Kiswahili, Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.

- James Sutherland (1957). *On English prose*. California: University of Toronto Press.
- Jilala, H. (2016). *Misingi ya Fasihi Linganishi: Nadharia, Mbinu na Matumizi*. Dar es Salaam: Daud Publishing Company.
- Kayombo, P. (2019). Sitiari katika Tamthilia za Emmanuel Mbogo. Tasinifu ya Shahada ya Kwanza, Chuo Kikuu cha Ruaha.
- Khalifani, M. Y. (2013). Masuala ya Kisiasa katika Ushairi wa Kandoro: Mifano kutoka Katika Mashairi Yake. Tasinifu ya Uzamivu, Chuo Kikuu Huria Cha Tanzania.
- Kiango, K. (1982). Tamthilia za Kiswahili: Dhamira Chapwa na Usuli katika Uchapwa. Katika *Kiswahili Juzuu Na. 49*2.
- Kiango, S. D. (1973). Maendeleo ya Fasihi ya Kiswahili Upane wa Michezo ya Kuigiza. Katika *Kiswahili, Juzuu Na. 2*: 88 – 97.
- Kiloba, L. Y. (2014). Korasi katika Tamthilia ya Kiswahili: Mifano toka Tamthilia Teule za Ebrahim Hussein, Emmanuel Mbogo, na Frowin Nyoni. Tasinifu ya shahada ya Uzamili ya Kiswahili ya Chuo Kikuu cha Dodoma.
- Koda, B. (2000). The Gender Dimension of Land Rights in Tanzania: Case Study of Msindo Village, Same District. Unpublished *Ph.D Thesis*, UDSM.
- Kombo, D. K. and Tromp. D. L. A (2006) *Proposal and Thesis Writing: An Introduction*. Nairobi: Pauliness Publications.
- Kothari, C. R. (2008). *Research Methodology: Methods and Techniques*. New Delhi: Wiley Eastern Limited.
- Kothari, C. R. (2004). *Research Methodology: Methods and Techniques*. New Delhi: New Age International Publishing Ltd.

- Ligembe, N. E. G. (1995). *The Uses of Methaphors in Penina Muhando's Lina Ubani: A stylistic Analysis*, M.A Dissertation of the University of Dar es Salaam.
- Lyatuu, J. (2011). *Usawiri wa wanawake katika Fasihi ya Kiswahili: Ulinganifu wa Waandishi wa Kike na wa Kiume – Uchunguzi Katika Riwaya teule. Tasnifu ya Uzamili Kiswahili; Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (Haijchapishwa).*
- Madumulla, J. S. (2009). *Riwaya ya Kiswahili: Nadharia, Historia na Misingi ya Uchambuzi*. Nairobi: Phoenix Publishers Limited.
- Makukula, D. Z. (2015). *Embe Dodo*. Dar es Salaam: Taasisi ya Taaluma za Kiswahili.
- Mangare, F. A. (2002). *Uhakiki wa Tamthilia ya Amezidi kama kazi ya Kibwege. Tasinifu ya shahada ya uzamili ya Kiswahili ya Chuo Kikuu cha Nairobi.*
- Mapunjo, G. C. (2014). *Usawiri wa Mwanamke Kama Kiongozi Katika Tamthilia: Uchunguzi wa Kivuli Kinaishi na Nguzo Mama*. Tasinifu ya Uzamili, Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.
- Massoud, S. M. A. (2013). *Maudhui na Fani katika tamthilia za Kiswahili: Utafiti Linganishi wa tamthilia za Mashetani na Kivuli Kinaishi, Tasinifu ya Uzamivu ya Kiswahili ya Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.*
- Masoud, H. S. (2018). *Kutathmini Usawiri wa Mwanamke katika Riwaya ya Mfadhili, Tasnifu ya Uzamili ya Kiswahili ya Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.*
- Mhando, R. E. (2015). *Kuchunguza dhamira za Kijamii katika Tamthilia ya Hatia ya Penina Mlama. Tasinifu ya Uzamili ya Kiswahili ya Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.*

- Mark, G. (1995). *Postmodern Semiotics: Material Culture and the Forms of Postmodern Life*. Oxford: Basil Blackwell.
- Mbaabu, I. (1985). *New Horizons in Kiswahili: Asynthesis in Developments Research and Literature*. Nairobi: Bureau First Published.
- Mhando, P. (1976). *Fasihi na Sanaa za Maonyesho*. Dar es Salaam: Tanzania Publishing House.
- Mkuwili, O. (2014). Fani na Maudhui katika Tamthilia ya Ngoma ya Ng'wanamalundi na Kivuli Kinaishi: Utafiti Linganishi. Tasinifu ya Shahada ya Uzamili ya Kiswahili ya Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.
- Mlacha, A. K. S. & Madumula, J. S. (1991). *Riwaya ya Kiswahili*. Dar es Salaam: DUP.
- Mlaga, K. W. (2017). *Misingi ya Ufundishaji na Ujifunzaji wa Fasihi*. Dar es Salaam: Heko Publishers Limited.
- Mlama, P. (1983). 'Utunzi wa Tamthilia Katika Mazingira ya Tanzania'. Dar es Salaam: TUKI.
- Mlama, P. (1983a). Hali ya Sanaa za Maonesho Tanzania, katika *Makala za Semina ya Kimataifa ya Waandishi wa Kiswahili*. Dar es Salaam. TUKI. Kur. 186 – 196.
- Mlama, P. (1983b). "Utunzi wa tamthilia katika Mazingira ya Tanzania", katika *Makala za Semina ya Kimataifa ya Waandishi wa Kiswahili*. Dar es Salaam. TUKI. Kur. 206 – 225.

- Mohamed, S. A. (1995). *Kunga za Nathari ya Kiswahili: Riwaya, tamthilia na Hadithi Fupi*. Nairobi: English Press Ltd
- Mpangala, G. P. (2007). "The Role of Civil Society in the 2005 General Elections in Tanzania," In, *Tanzania Journal of Development Studies*, Vol. 7, No. 2 Pp. 1-18. Dar es Salaam: IDS.
- Mrikaria, S.E. (2010). Kejeli na Fasihi ya Kiswahili-Tanzania, Katika *Swahili Forum 17 (2010): 104-125*.
- Msokile, M. (1992). *Kunga za Fasihi na Lugha*. Dar es Salam: Educational Publishers and Distributors.
- Msuya, M.B. & Lupokela, A.P. (2012). Dhima ya Bongo fleva katika Maadili na malezi Kwa jamii, Katika *Mulika. Na. 10*, Dar es Salaam TATAKI.
- Mulokozi M. M. (1996). *Utangulizi wa Fasihi ya Kiswahili*. Dar es Salaam: Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.
- Mulokozi, M. M. (2017). *Utangulizi wa Fasihi ya Kiswahili*. Dar es Salaam: KAUTTU.
- Mutembei, A. K. (2006). Nadharia ya Fasihi Simulizi na Maendeleo katika Sayansi na Teknolojia, katika *Mulika Juz. Na. 27: 1-17*.
- Mwaipopo, R. N. G. (1990). The Impact of Commodity Relations on the Role and Status of Women in Peasant Households: A Case Study of Rungwe District. M. A Thesis, University of Dar es Salaam.

- Mwakanjuki, N. (2022). Kuchunguza Motifu katika Tamthilia za Emmanuel Mbogo. Tasinifu ya Uzamivu, Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.
- Mwenda, M. (2001). *Kamusi ya Fasihi*. Nairobi: Standard Textbooks Graphics and Publishing.
- Nicholaus, A. (2011). Ubuntu katika Tamthilia za Penina Mhando. Tasinifu ya Uzamili ya Kiswahili, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.
- Njogu, K., (1993). *Misingi ya Uhakiki wa Fasihi*. Nairobi: East African Educational Publishers.
- Njogu, K., & Chimerah, R. (1999). *Ufundishaji wa Fasihi, Nadharia na Mbinu*. Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.
- Njogu, K. na Wafula, R. M. (2007). *Nadharia za Uhakiki wa Fasihi*. Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.
- Ntarangwi, M. (2004). *Uhakiki wa Kazi za Fasihi*. Rock Island: Augustana College.
- Nyerere, J. K. (1967). *Ujamaa: The Basis of African Socialism*. Dar es Salaam: Tanganyika Standard.
- Nzelli, J. (2018). Taswira katika Tamthilia za Said Ahmed Mohamed za *Pungwa, Kivuli Kinaishi na Mashetani Wamerudi*, Tasinifu ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Nairobi.
- Omary, M. (2011). Siasa katika Ushairi wa Kezilahabi: Uchunguzi wa *Karibu Ndani* (1988) na *Dhifa* (2008). Tasinifu ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.



- Ponera, A. S. (2014). *Utangulizi wa Nadhalia ya Fasihi Linganishi*. Dar es Salaam: Karljamer Print Technology.
- Remark, H. H. (1971). *Comparative Literature: Its Definition and Functions*. Corbondale: Southern Illinois.
- Ramadhani, D. (2005). The Uses of Metaphors in Mbogo's Ngoma ya Ng'wanamalundi and Hussein's Mashetani. A Stylistic Comparison, Tasinifu ya Umahiri, University of Dar es Salaam.
- Richard, M. & Wafula, F. (1999). *Uhakiki wa Tamthilia, Historia na Maendeleo Yake*. Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.
- Robson, C. (2007). *How to Do a Research Project: A Guide for Undergraduate Students*. Cariton Victoria: Blackwell Publishing
- Sadgrove, P. (2007). *The Egyptian Theatre in the Nineteenth Century: 1799-1882*, Ithaca Press.
- Said, A. M. (1995). *Amezidi*. Nairobi: East African Educational Publishers.
- Said, A. M. (1995). *Kunga za Nathari ya Kiswahili*. Dar es Salaam: East Africa Educational Publishers Ltd.
- Semzaba, E. (1997). *Tamthilia ya Kiswahili*. Chuo Kikuu Huria cha Tanzania, Dar es Salaam. Tanzania.
- Senkoro, F. E. M. K. (1982). *Fasihi*, Dar es Salaam: DUP.

- Senkoro, F. E. M. K., (2006). Fasihi ya Kiswahili ya Majaribio: Makutano Baina ya Fasihi Simulizi na Fasihi Andishi. Katika, *Kioo cha Lugha*, Juzuu, 1. Idara ya Kiswahili Chuo Kikuu Cha Dar es Salaam uk. 61-68.
- Shabani, S. (2016). Kutathmini Mbinu za kifutuhi zilizotumika kuibua Ucheshi katika Tamthilia za *Kaptula la Marx* na *Ushuhuda wa Mifupa*: Utafiti Linganishi. Tasnifu ya Uzamili ya Kiswahili ya Chuo Kikuu Huria Cha Tanzania.
- Shemweta, G. (2015). Itikadi katika tamthilia za Emmanuel Mbogo: Utafiti Linganishi wa *Ngoma ya Ng'wanamalundi* na *Fumo Liongo*. Tasnifu ya Uzamili Chuo Kikuu Huria Cha Tanzania.
- Senyamanza, C. (2014). *Misingi ya Kazi za Kubuni: Nadharia, Mbinu na Mifano ya Kazi Bunilizi*. Dar es Salaam: Karljamer Print Technology.
- Shivji, I. G. (2002). Makuadi wa Soko Huria (Chachage, S. Chachage), Hotuba ya Uzinduzi wa Kitabu, katika *Mulika namba 26, 2000-2002*, TUKI, Kur. 93-97.
- Solomon, J. (1988). *The signs of our times: The Secret Meanings of Everyday Life*. New York: Harper & Row.
- Talcot, M. (2010). *Research: From theory to Practice*. Canada: Apprentice Hall.
- Umberto, E. (1976). *A theory of semiotics*. Bloomington: Indiana University Press.
- Wa Thiong'o, N. (1995). *Decolonising the Mind: The Language of Literature in Afrika*. London: Currey Publishers.

- Wafula, R. M. (1999). *Uhakiki wa Tamthilia: Historia na Maendeleo yake*. Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.
- Wamitila, K. W. (2002). *Uhakiki wa Fasihi, Misingi na Vipengele Vyake*. Phoenix Publishers Ltd.
- Wamitila, K. W. (2003). *Kamusi ya Fasihi Istilahi na Nadharia*. Nairobi: Focus Books.
- Wamitila, K. W. (2010). *Kanzi ya Fasihi, Misingi ya Uchanganuzi wa Fasihi*, Vide-Muwa Publishers Limited.
- Wamitila, K. W. (2012). *Kichocheo cha Fasihi, Simulizi na Andishi*. Nairobi: Focus Book.
- Wellek, R. (1988). The Crisis in Comparative Literature Literature. Concepts of Critisms. Ed. Stephen, G. Nichols Jr. New Haven: Yale University Press, 282-295.
- Wellek, R., na Warren, A. (1948). *Theory of Literature*, New York, Harcourt, Brace and Company.
- Yin, R. K. (1994). *Case Study Research: Design and Methods*, (2<sup>nd</sup> eds.) thousand Oaks Calif: SAGE Publishers.

### MAREJEO YA KIARABU

TAQRID MAHMOUD MOHAMMAD, TAMTHILIA YA KISIASA KATIKA MISRI KUTOKA 1980 MPAKA 2000, TASNIFU YA MASTA, CHUO KIKUU CHA AIN SHAMS, KITIVO CHA LUGHA, sehemu ya Lugha ya Kiarabu, haijchapishwa, 2004.

طارق محمود محمد، المسرح السياسي المعاصر المصري منذ 1980 حتى 2000، شهادة الماجستير، جامعة عين شمس، كلية الألسن، قسم اللغة العربية، غير منشورة، 2004.

MORAD HASAN ABDELAAL, ATHARI ZA KIARABU NA KIGENI KATIKA TAMTHILIA YA SALAH ABDULSABUR, TASNIFU YA MASTA, CHUO KIKUU CHA ALIXANDRIA, KITIVO CHA FASIHI, SEHEMU YA LUGHA YA KIARABU NA LUGHA ZA KIMASHIRIKI, HAIJACHAPISHWA, 1997.

مراد حسن عبدالعال، الأثر العربي والاجنبي في مسرح صلاح عبد الصبور، رسالة ماجستير غير منشورة، جامعة الاسكندرية، كلية الآداب، قسم اللغة العربية واللغات الشرقية، 1997.

EBRAHIM FATHY, KAMUSI YA ISTILAHU ZA KIFASIHI, TAASISI YA KIARABU YA KUCHAPISHAJI, TOLEO LA KWANZA, 1986.

إبراهيم فتحي، معجم المصطلحات الأدبية ، المؤسسة العربية للناشرين المتحدين، الطبعة الاولى 1986م، ص 323.

Ebrahim Hamada, Kamusi ya istilahi ya kitamthilia nay a kidrama, Darulmaarif, 1985

إبراهيم حمادة، معجم المصطلحات الدرامية والمسرحية، دار المعارف، 1985

ABU ALHASAN SALLAM, MATINI YA TAMTHILIA KATIKA UFA SIRI, NUKUU, MAANDALIZI NA uandishi, toleo la pili, taasisi ya vitabu ya Alex, Egypt, 1993

أبو الحسن عبد الحميد سلام: حيرة النص المسرحي بين الترجمة والاقتباس والاعداد والتأليف، ط 2، مركز الإسكندرية للكتاب، مصر، 1993، ص 28-29.

Fatma Omrany, **tashititi katika tamthilia ya Ahmad Ridha Hoho**, tasnifu YA MASTA, CHUO KIKUU CHA QASDY MRBAH, KITIVO CHA FASIHI NA LUGHA, haijachapishwa, 2016.

فاطمة عمراني، **السخرية في مسرحيات أحمد رضا حوجو** ، مذكرة مقدمة لاستكمال متطلبات شهادة الماجستير، جامعة قاصدي مرباح – ورقلة كلية الآداب واللغات، 2016

TAMER FAYEZ, **HADITHI ZA JADI KWENYE TAMTHILIA YA KISASA YA KIMISRI: FASIHI LINGANISHI**, TUME KUU YA MAJUMBA YA UTAMADUNI, 2016.

تامر فايز، **الأسطورة في المسرح المصري المعاصر: دراسة في الأدب المقارن**، الهيئة العامة لقصور الثقافة، 2016.

## **VIAMBATANISHO**

### **KIAMBATANISHO NAMBA 1: HATUA KATIKA USANIFU UTAFITI**

#### **Hatua ya Kwanza**

Mtafiti katika hatua hii alifanya kazi ya kujenga wazo la utafiti ambalo lilimwezesha kupata udahili wa kusoma shahada ya Uzamivu ya Kiswahili ya Chuo Kikuu Huria cha Tanzania. Hatua hii ilihusisha kusoma machapisho mbalimbali pamoja na kuuliza maswali kwa wabobezi wa fasihi ya Kiswahili na Kimisri.

#### **Hatua ya Pili**

Hii ilikuwa ni hatua ya kuteua kazi za tamthilia ambazo zimeshughulikiwa katika utafiti huu. Kama inavyofahamika ni kwamba tamthilia zipo nyingi kutoka kwa waandishi mbalimbali na hivyo, kupata tamtiliya ya kushughulikia ni lazima kuwa na tafakuri ya kutosha kabisa ambayo huchukuwa muda.

#### **Hatua ya Tatu**

Kuteua mbinu ya usanifu wa utafiti na hapa ndipo tulipoteua mbinu ya uchunguzi kifani. Baada ya kubaini tamthilia ambazo tutazitumia kupata data za utafiti ndipo sasa tukachagua uchunguzi kifani ili kuweza kuzimakinikia vizuri tamthilia hizo kwa lengo la kupata data za utafiti.

#### **Hatua ya Nne**

Hii ni hatua ya kuandaa na kuteua mbinu za kukusanya na kuchambua data za utafiti ambapo mbinu za usomaji makini na upitiaji wa nyaraka ziliteuliwa na mbinu ya mkabala wa kimatelezo ikateuliwa kwa ajili ya kuchambua data.

**Hatua ya Tano**

Hii ni hatua ya mwisho ambayo imehusisha kuandika tasnifu na kuiwasilisha.

**KIAMBATANISHO NAMBA 2: MUONGOZO WA USOMAJI MAKINI****Hatua ya Kwanza**

Kusoma matini teule kwa mara ya kwanza kwa lengo la kupata picha ya jumla kuhusiana na matini hiyo. Hapa mtafiti anasoma matini hiyo zaidi ya mara moja mpaka pale anapona kwamba amelewa vizuri, yaani amepata picha ya jumla kuhusiana na matini hiyo.

**Hatua ya Pili**

Kuandaa shajara au daftari maalumu kwa ajili ya kukusanya data za utafiti. Shajara hilo hugawanywa katika sehemu kadhaa kulingana na malengo mahususi ya utafiti ili kila lengo liweze kupata data zinazohitajika.

**Hatua ya Tatu**

Hii ni hatua ya kusoma matini husika na kuanza kudondoa data kwa mujibu wa malengo mahususi ya utafiti kama ilivyoandaliwa kwenye shajara. Mtafiti atadondoa neno, sentensi au aya ambayo inatoa data na kuiandika katika shajara kwenye lengo husika.

**Hatua ya Nne**

Kurudia tena yale ambayo yamefanyika katika hatua ta tatu ili kujiridhisha kwamba data iliyokusanywa ni sahihi na inatosheleza mahitaji ya kila lengo mahususi la utafiti.

**Hatua ya Tano**

Kuzipangilia data vizuri tayari kwa ajili ya uchambuzi ambao utafanywa kwa kuzingatia mbinu ya mkabala wa kimaelezo kama ilivyoielezwa katika kipengele husika cha uchambuzi wa data.



### **KIAMBATANISHO NAMBA 3: MUONGOZO WA UCHAMBUZI WA DATA**

#### **Hatua ya Kwanza**

Kuunganisha data ambazo zinafanana na kutenganisha zile ambazo ni zinatofautiana.

Hii ni hatua muhimu kwani husaidia kufanya zoezi la uchambuzi wa data kutokuwa na marudiorudio ambayo hayahitajiki.

#### **Hatua ya Pili**

Kutoa mada za kupatiwa uchambuzi kwa mujibu wa malengo mahususi ya utafiti.

Hapa mtafiti huunda mada kuu na ndogo ambazo husaidia kupatiwa data ili kuweza kujibu maswali ya utafiti.

#### **Hatua ya Tatu**

Kuwasilisha data chini ya mada kuu au ndogo iliyoteuliwa na kisha kufanyiwa uchambuzi. Hapa data inawasilishwa kwa mfumo wa dondoo au nukuu kulingana na mpango wa utafiti husika.

#### **Hatua ya Nne**

Hii ni hatua ya kuhusisha data na nadharia iliyoteuliwa katika uchambuzi wa data.

Hatua hii ni muhimu kwani hutoa nafasi kwa matumizi ya nadharia katika uchambuzi wa data.

#### **Hatua ya Tano**

Kujadili matokeo ya utafiti.